

# Mwongozo wa Haki za Binadamu

Mwongozo wa Haki za Binadamu za Shirika la Nature Conservancy wa Kufanya Kazi na Wenyeji na Jamii za Eneo hilo

### Mwongozo wa Haki za Binadamu wa TNC

# Muhtasari wa Utendaji

## Muhtasari

Mwongozo wa Haki za Binadamu wa Shirika la Nature Conservancy wa Kufanya Kazi na Wenyeji na Jamii za Eneo hilo unatoa zana, rasilimali na mwongozo ili kuunga mkono kazi ya TNC ya:

- Kuheshimu na kukuza haki za binadamu za Wenyeji na jamii za eneo hilo
- Kupunguzia TNC hasara zinazoweza kutokea kwa sababu ya mambo yasiyojulikana zinazohusiana na haki za binadamu na uhifadhi
- Kuboresha kazi ya kuhifadhi kwa kujumuisha mbinu ya haki za binadamu

Mwongozo ni ya watunzaji wa TNC, wasimamizi na viongozi wakuu na unahusu pia kazi zote na mbinu za kimkakati – kuanzia miradi inayoanza mpaka mipango ya mkoa na utekelezaji wa sera. Ni muhumi hata kama TNC ni: mtoa huduma kwa IPLC, mshirika kamili wa IPLC, kiongozi wa mpango, au mwanachama wa mpango wa wadau wengi. Mwongozo husaidia kuimarisha na kuboresha mahusiano mapya na yanayoendelea kwa kuzingatia uzoefu, utaalamu, na kujitawala kwa IPLCs

Mwongozo una Kanuni tisa na Sera za Kulinda Maslahi ambazo zimetolewa kutoka kwa ahadi za TNC kwa sheria na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu:

- Uhuru wa Kuchagua na Kujiamulia Mwenyewe
- Kujihusisha Mapema na Mahusiano ya Ushirikiano:
- Kufanya Uamuzi baada ya Kuelewa
- Haki ya Kukataa kutoa Idhini
- Ushauri wa Maana
- Usawa
- Uhusishaji
- Uwajibikaji
- Nia Njema

Utafiti wa kubuni umebuniwa katika moduli ili kuonyesha na kusaidia kushughulikia hali ngumu ambazo zinaweza kutokea.

Mwongozo umetengenezwa na wafanyakazi wa TNC, wanachama wa IPLC, wadau wasio husika moja kwa moja na wataalamu wa haki za binadamu kwa miaka kadhaa. Ni mwandiko wa upesi wa hati, unaokusudiwa kubadilika wakati kujifunza kwetu na uzoefu unaendelea. Tutaendelea kufanya majaribio, kurudiarudia na kusasisha mwongozo huu.

## Wawasiliani

**Timu ya TNC ya Uhifadhi ya Ulimwenguni kwa Kushirikiana na Wenyenji na Jamii za Eneo hilo:**

Allison Martin

allison_martin@tnc.org

**Timu ya TNC ya Utofauti Ulimwenguni, Usawa na Uhusishaji:**

Laurel Chun

lchun@tnc.org

**Timu ya TNC ya Wanasheria wa:**

Ulimwenguni: Johnny Wilson

jwilson@tnc.org

# Yaliyomo


Muhtasari wa Utendaji 2

Utangulizi 5
Utangulizi wa Utafiti wa Wenland 14
Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi 16

Moduli ya 1: Kujifunza na Majadiliano ya Mwanzo 20
1A. Utafiti wa Wenland: TNC katika Wenland (Tukio la 1) 37
1B. Utafiti wa Wenland: TNC katika Wenland (Tukio la 2) 40
1C. Utafiti wa Wenland: Tatizo la Udongo jalidi 43
1D. Utafiti wa Wenland: Kujitawala kwa Wen 46
Kiolezo: Mpango wa Kujihusisha 49

Moduli ya 2: Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa 58
2A. Utafiti wa Wenland: Muungano wa Mashauriano 79
2B. Utafiti wa Wenland: Idhini na Haki ya Kukataa kutoa Idhini 82
Mti wa Uamuzi wa FPIC Je Mchakato wa FPIC unahitajika? 85
Utafiti wa Wenland: Bajeti ya Kubuni 86
Kiolezo: Mpango wa Ushauri wa FPIC 90

Moduli ya 3: Utatuzi wa Mgogoro 99
3A. Utafiti wa Wenland: Utatuzi wa Mgogoro 117
Kiolezo: Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro 120

Moduli ya 4: Utekelezaji 132
4A. Utafiti wa Wenland: Utekelezaji 141

Moduli ya 5: Kuandika hati 144
5A. Utafiti wa Wenland: Kuandika hati 153

Moduli ya 6: Ufuatiliaji, Tathmini & Marekebisho 156
6A. Utafiti wa Wenland: Ufuatiliaji, Tathmini & Marekebisho 167
Kiolezo: Viashiria vya Haki za Binadamu 170

Kiambatisho cha I: Ahadi za TNC 177

Kiambatisho cha II: Faharasa ya Maneno Muhimu 180

Kiambatisho cha III: Je Mchakato wa FPIC unahitajika 185

Kiambatisho cha IV: FPIC – Maswali ya Mara kwa Mara 186

Kiambatisho cha V: Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni 190

Kiambatisho cha VI: Orodha za kukagulia 193

Kiambatisho cha VII: Hati za Kuhifadhi 194

Kiambatisho cha VIII: Violezo 195

Kiambatisho cha IX: Shukrani 196






## Mwongozo wa Haki za Binadamu wa TNC

# Utangulizi

Kwenye utangulizi:

Elewa kwa nini mbinu ya hifadhi inayozingatia haki za binadamu ni muhimu

Jifunze wakati na jinsi ya kutumia mwongozo huu

Kagua Kanuni Tisa na Sera za Kulinda Maslahi

Soma utangulizi wa utafiti wa Wenland unaoelezea mambo muhimu yaliyo kwenye Mwongozo

**Utangulizi wa Utafiti wa Wenland:**

Karibu Wenland

Mazo kwamba ustawi wa watu wote unategemea mifumo mizuri ya ikolojia, na kwamba afya ya mifumo hii ya ikolojia inategemea ustawi wa wale ambao wameisimamia kwa vizazi vingi.

Leo hii, wenyeji na jamii za eneo hilo wanadhibiti angalau asilimia 25 ya ardhi za ulimwengu,[1] asilimia 17 ya kaboni ya misitu duniani[2] na sehemu kubwa zenye maji safi na makao ya viumbe vya baharini.

Ujuzi unaoendelea wa kiikolojia umekita mizizi katika tamaduni za Wenyeji wengi na Jamii za eneo hilo, pamoja na kujihusisha sana na mahali na kujitolea bila kusita kwa ajili ya kulinda ardhi na maji yao. Ushahidi unaonyesha kwamba IPLCs kuongoza usimamizi kunasababisha matokeo mazuri zaidi ya kuhifadhi, yanayodumu.[3] Kwa hivyo kuunga mkono uongozi wa IPLC, ni mojawapo wa njia zenye athari kubwa za kulinda maeneo muhimu, kushughuilikia mabadiliko ya hali ya hewa na kuwa na siku zijazo ambapo watu na maumbile yanastawi.

Lakini kwa muda mrefu IPLCs wamekuwa wakiwekwa pembeni na kutengwa katika maamuzi yanayoathiri maeneo yao, tamaduni, riziki na ustawi. Uhusiano wao na ardhi zao, maji na maliasili zimedharauliwa au kutothaminiwa na watendaji wengine, ikiwa ni pamoja na mashirika ya kuhifadhi. Matokeo mabaya yanayosababishwa na kuhifadhi yamejumuisha:

- unyakuzi wa ardhi
- kulazimishwa kuhama
- kutokubaliwa kujitawala
- kutoweza kupata riziki
- kupoteza utamaduni na maeneo takatifu
- kutotambuliwa kwa mamlaka zao
- kunyimwa haki na fidia, ikiwa ni pamoja na kurejeshewa gharama na fidia.[4]

IPLCs na hasa wenyeji ambao ni wanawake, wamelipa gharama (na wamepokea aida chache) za juhudu za kuhifadhi zinazopuuza ujuzi wao, mtazamo, uongozi na haki.

Mapambano dhidi ya ukoloni na ukandamizaji wa kimuundo yanaendelea, ingawa IPLCs wamekusanya nguvu ya pamoja katika mazingira ya kisiasa ya ndani na ya kimataifa katika miongo ya hivi karibuni. Miaka thelathini iliyopita, wazo la haki zinazotambuliwa za wenyeji halikusikika sana. Mnamo 2007, haki hizi zilithibitishwa na mataifa 144 katika **Azimio ya Umoja wa Kimatifa kuhusu Haki za Wenyeji**. Ilipofika 2016, kila taifa ambalo lilikuwa limepinga UNDRIP mnamo 2007 lilikuwa limebadilisha mawazo, na kutambua ubora wa haki za wenyeji katika sheria ya kimataifa na ya ndani. Wenyeji wamesimama pamoja katika hali mbaya sana, na kupigania na kulinda haki hizi, ikiwa ni pamoja na haki ya kujiamulia mwenyewe na kiwango cha Idhini ya Kujitolea, YInayotolewa Mapema a awali na Baada ya kuelewa.

TNC imejitolea kutumia mbinu inayozingatia haki za binadamu katika uhifadhi, kuunga mkono wenyeji wanapolinda na kutekeleza haki zao.

Kujitolea huko kunaonekana katika Maono, Maadili, Kanuni ya Mwenendo ya TNC na mbinu ya msingi ya uhifadhi. Tunatambua umuhimu wa Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa. Kuheshimu na kukuza haki za binadamu za IPLCs ni wajibu wa kimaaadili na hali inayowezesha uhifadhi endelevu na ustawi wa binadamu. Uhifadhi wa ushirikiano unasaidia kazi ya IPLCs ya kulinda tamaduni zao, riziki na kujihusisha na mahali – inayohakikisha siku zijazo ambapo maumbile na watu wanafanikiwa.

## Madhumuni

TNC inafanya kazi na wenyeji na jamii za eneo hilo katika nchi 24, ikiwa na mifano mizuri ya mbinu zinazozingatia haki katika uhifadhi zilizokita mizizi katika ushirikiano wa muda mrefu. Ili itumie mbinu hii mara kwa mara katika mipango na jiografia, TNC imeandaa Mwongozo huu wa Haki za Binadamu wa Kufanya Kazi na Wenyeji na Jamii za Eneo hilo kama nyenzo kwa watendaji na viongozi wa TNC.

### Madhumuni ya Mwongozo

Mwongozo huu una moduli zinazohakikisha kwamba TNC:

- Inaheshimu na inaunga mkono haki za IPLCs, zinazoambatana na viwango vya kimataifa na Maadili na Kanuni ya Mwenendo ya TNC
- Inapunguza hasara zinazoweza kutokea kwa sababu ya mambo yasiyojulikana wakati haki za binadamu na uhifadhi unazidi kunzingatiwa kimataifa

- Inaboresha matokeo ya uhifadhi kwa watu na maumbile kwa kuhusisha haki za binadamu katika desturi yetu ya uhifadhi

Mwongozo ni hati inayoendelea kuhaririwa na kusasishwa itakayobadilika kulingana na tutakayopitia katika kushirikiana na IPLCs. Inatoa rasilimali na zana zinazolenga kudhibiti hali ngumu, lakini haina majibu yote. Wafanyakazi wanapaswa kuwasiliana mara kwa mara na washirika, wataalam wa nje na miongoni mwao kwa ajili ya ushauri unaotegemea hali husika na kushiriki mafunzo. Kwa mwongozo unaoendelea, Mtandao wa TNC wa Sauti  Shupavu, Chaguo na Hatua; Timu ya TNC ya Wenyeji na Jamii za Eneo la Ulimwengu; na Timu ya TNC ya Utofauti Ulimwenguni, Usawa na Uhusishaji zinapatikana.

## Muundo

Mwongozo huu una moduli sita, ambayo kila moja inaangazia Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi ambazo ni msingi kwa kila moduli.

**Moduli kwa tazamo la haraka**

**1.Kujifunza na Majadiliano ya Mwanzo**
Tambua IPLCs wailioathirika na uwashirikishe kwa njia zinazoheshimu haki ya wenyeji ya kujitawala na kujenga uhusiano sawa

**2. Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa (FPIC)**
Omba na udumishe idhini ya mpango kupitia ushauri wa maana na kujifunza pamoja

**3. Utatuzi wa Mgogoro**
Kubaliana kuhusu njia za kitamaduni za kushughulikia kutoelewana kwokwote, migogoro au mizozo

**4. Utekelezaji**
Tumia Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi na mapendekezo yaliyo kwenye Mwongozo huu wakati wa kutekeleza mpango

**5. Kuandika Hati**
Andika hati kwa njia zinazojumuisha, zilizo wazi na ambazo IPLCs wanaweza kufikia na pia zinazokidhi mahitaji ya TNC

**6. Ufuatiliaji, Tathmini & Marekebisho**
Fuatilia desturi za kufuata Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi na mapendekezo yaliyo kwenye Mwongozo huu

Kila moduli inafuata muhtasari sawa:

- Utangulizi — mambo ambayo wafanyakazi wanaweza kutarajia kujifunza
- Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi — maadili, kanuni na viwango vinavyoongoza kazi yetu
- Mwongozo — taarifa, zana, violezo na rasilimali

- Utafiti wa Kubuni — hadithi inayofanya tufurahie kujifunza
- Orodha ya kukagulia — orodha ya fomu-fupi ya shughuli zinazopaswa kufanywa

## Jinsi ya Kutumia Mwongozo huu na Inapotumika

**Je IPLCs ni akina nani?**

"Wenyeji na jamii za eneo hilo" inamaanisha watu na jamii wenye uhusiano mkubwa na mandhari yao ya asili, ambayo wanategemea kwa ajili ya ustawi wa utamaduni, wa kiroho, kiuchumi na kimwili. Wakazi wa asili na wahamiaji ambao wana uhusiano wa karibu na mandhari vile vile huchukuliwa kuwa IPLCs.

TNC inatambua haki za watu wote wenyeji kama ilivyoorodheshwa katika sheria ya kimataifa[5] Katika Mwongozo huu, "IPLCs" na "jamii" zinatumiwa kumaanisha wenyeji wote na jamii za eneo hilo.

Mwongozo huu umeandikwa kwa ajili ya watendaji na viongozi wa uhifadhi wa TNC, na inatumika katika kazi zote zinazoweza kuathiri wenyeji na jamii za eneo hilo.

Upeo unazidi Mfano wa IPLC wa TNC katika Ajenda ya Uhifadhi wa Pamoja. Timu za mradi zinapaswa kukagua Moduli ya Kujifunza na Majadiliano ya Mwanzo ili zielewe ikiwa IPLCs wanaweza kuathiriwa na kazi zao, hata katika mipango ambayo inaweza kuonekana kana kwamba itatoa athari kama hizo.

Hali ya uhusiano wa wafanyakazi wa TNC na IPLCs itakuwa tofauti kulingana na hali husika. Angalia kisanduku "Jinsi ambavyo Huenda TNC Ijihusihe na IPLCs" kwa mifano.

**Jinsi ambavyo Huenda TNC Ijihusihe na IPLCs**

Majukumu TNC katika mpango:

- TNC ni mtoa huduma au mshauri wa kiufundi katika mpango unaoongozwa na IPLC
- TNC inaunda mpango kama mshirika kamili na IPLCs
- TNC inaongoza mpango unaohusisha IPLCs
- TNC inashiriki katika mchakato mkubwa wa wadau wengi unaohusisha IPLCs

Aina ya mipango:

- Miradi ya eneo husika
- Mikakati ya kimpango, ya mkoa au inayozingatia nchi
- Sera

Hatua za kujihusisha na IPLCs:

- Ushirikiano na Uhusishaji uliopo
- Ushirikiano na uhusishaji mpaya au wa siku zijazo [6]

TNC inapaswa kujitahidi kuunda uhusiano wa heshima, usawa na IPLC, na kazi hii inachukua muda. Ingawa kujihusisha kwa TNC kutaonekana tofauti katika hali tofauti, jukumu la kujumuisha na kukuza Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi na desturi katika Mwongozo huu halibadiliki.

Mwongozo unahusu mipango mipya pamoja na iliyopo. Mipango mipaya inapaswa kuanza kwa Moduli ya Kujifunza na Majadiliano ya Mwanzo. Mipango inayoendelea tayari inaweza kutumia Mwongozo kutambua athari zinazoweza kutokea, hasa pale ambapo zinaweza kuwa hazikuonekana haraka, kwa mfano, mpango wa sera ya kitaifa inayolenga uhifadhi.

Moduli zinafuata mtiririko wa kimantiki, ingawa watumiaji wanaweza kujiunga katika moduli yoyote. Katika hali ya mpango uliopo na uhusiano wa muda mrefu wa IPLC, timu inaweza kuweza kwenda haraka kwenye Moduli ya Utatuzi wa Mgogoro ikiwa ushirikaino wao ni imara lakini hauna mchakato uliokubaliwa wa kusuluhisha migogoro. Sehemu za Orodha za Kukagulia na Hati za Kuhifadhi na violezo vilivyotolewa katika Kiambatisho cha VIII zina sehemu kuu za kila moduli kwa ajili ya kurejelewa kwa urahisi.

Ni muhimu kusisitiza baadhi ya sehemu za msingi za Mwongozo:

- Hatua ya Kwanza ya Moduli ya Kujifunza na Majadiliano ya Mwanzo Inafaa sana wafanyakazi ambao hawajui sana masuala ya haki za binadamu
- Moduli ya Kuandika hati: Inaweza kutumika pamoja na Moduli ya Kujifunza na Majadiliano ya Mwanzo kuandikia vifaa vilivyokamilishwa tayari kwa mipango iliyopo
- Moduli ya Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa: Muhimu kwa wote, kwa kuwa FPIC ni mchakato unaoendelea na hitaji la shirika la mpango wowote

Mwongozo huu unazingatia jinsi ambavyo TNC inapaswa kushirikiana na IPLCs, kuanzia na kanuni ya KujihusishaMapema: kujihusisha na kusikiliza IPLCs kabla ya kuamua mipango yoyote iliyowekwa. TNC inaamini katika faida za pamoja za kushirikiana na IPLC katika uhifadhi, lakini ni shirika la nje linalohusiana na IPLCs, ambao wamevumilia enzi za ukoloni na athari zake mbaya.

Kufuata mwongozo wa Kujihusisha Mapema kutasaidia kuhakikisha kwamba juhudi za TNC za kujihusisha haziweki hali kuwa shida na TNC kama suluhisho. Badala yake TNC inapaswa kusaidia katika kuzingatia mtazamo wa IPLC na kujiamulia mwenyewe kuanzia mwanzo.

TNC kufanya mashirika mengine yawajibike katika kanuni na desturi zilizo kwenye Mwongozo huu pia ni muhimu na inafaa. Mashirika haya yanaweza kuwa:

- wafadhili
- wakandarasi
- wasambazaji
- washirika wengine

TNC inapaswa kuangalia kwa uangalifu maeneo ambayo taasisi hizi zinaweza kuwa na athari za haki za binadamu kwa IPLCs na kisha kukagua kujitolea kwa shirika hilo katika haki za binadamu na mifumo inayotumia kutekeleza ahadi hiyo. Ambapo kujitolea au mifumo haipo, na ambapo TNC inaweza kuwa na ushawishi, TNC inapaswa kuzingatia kusaidia shirika hilo kuboresha desturi lake la haki za binadamu. Ikiwa athari mbaya haziwezi kuepukika, na tathmini za kuaminika zinaonyesha kwamba athari hizo zinaweza kutokea, TNC inapaswa kuzingatia kukomesha uhusiano na shirika hilo.[7]



## Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi

Mwongozo umetengenezwa kwa Kanuni tisa na Sera za Kulinda Maslahi, ambavyo vinapaswa kuongoza kazi zote za TNC na IPLCs.

Kanuni na Sera hizi za Kulinda Maslahi zimeondolewa kwenye ahadi zilizopo, ikiwa ni pamoja na:

- Maadili yetu
- Kanuni yetu ya Mwenendo
- ahadi yetu kwa Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji, hasa vifungu 18-19 na 32 (ushiriki na FPIC), 23-26 na 29 (haki za ardhi na uhifadhi), 31 (haki za kitamaduni), na 40 (utatuzi wa mgogoro)
- mahitaji ya Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa kama ilivyoainishwa katika UNDRIP
- Mkutano wa ILO (Nambari 169) kuhusu Wenyeji na Watu wa Kikabila, na mamlaka nyingine
- Kanuni Zinazoongoza Mpango wa Uhifadhi wa haki za Binadamu
- Muundo wa Uhifadhi 2.0 Mwongozo wa Hati

Kanuni na Sera za Kulinda Masalahi hujulisha na kuongoza mbinu ya TNC inayozingatia haki za binadamu katika uhifadhi na vimetajwa kama msingi wa kila moduli. Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi pia ni zana ya kutathmini na hutoa msingi wa orodha za kukagulia zilizo mwishoni mwa kila moduli.

Hakuna chochote katika Mwongozo huu kinachopaswa kuzuia majukumu yoyote ya haki za binadamu ambayo TNC imejitolea au inayofuata. Badala yake**, Mwongozo huu unafafanua maadili, njia na desturi ambazo TNC inaheshimu kujitolea kwetu katika kuheshimu na kukuza haki za binadamu za wenyeji na jamii za eneo hilo.**

### Kanuni Tisa na Sera za Kulinda Maslahi

Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi

**Uhuru wa Kuchagua na Kujiamulia Mwenyewe:**
Kuheshimu haki za wenyeji za Kujiamulia wenyewe na kujitawala, bila kuwalazimisha hata kidogo au kuwatishia kwamba kutakuwa na matokeo mabaya.

Imeungwa mkono kwa kufanya mazungumzo ya heshima na IPLCs na kuelewa athari za kihistoria na za leo za ukoloni, ukandamizaji na kutokuwa na usawa wa nguvu.

**Kujihusisha Mapema na Mahusiano ya Ushirikiano:**
Kujihusisha mapema kwa IPLCs katika mpango wowote unaoweza kuwaathiri.

Imeungwa mkono kwa kuzingatia Uongozi wa IPLC na kushiriki ipasavyo katika kubuni na kupanga maamuzi, na kujenga uaminifu.

**Kufanya Uamuzi baada ya Kuelewa:**
Kusaidia IPLC kufikia taarifa yote kuhusu shughuli ambazo zinaweza kuwaathiri, katika mazingira, lugha na miundo inayokidhi mahitaji yao.

Inaungwa mkono kwa kuwekeza wakati na rasilimali ili wafanyakazi wa IPLC na TNC wapate na waboreshe ujuzi, na kujitolea katika kutathmini athari kwa bidii, mawasiliano wazi, kuheshimu njia nyingi za kujua na kujifunza pamoja kama msingi wa kufanya uamuzi.

**Haki ya Kukataa kutoa Idhini:**
Kuheshimu haki ya wenyeji ya kukataa kutoa idhini ya mipango ambayo wanaona kwamba inaweza kuwaathiri sana.

Inaungwa mkono kwa kuheshimu uamuzi wa wenyeji wa kusema “ndiyo” au “hapana,” pamoja na “ndiyo, lakini kwa masharti” na “hapana, lakini tuendelee kujadili.”

**Ushauri wa Maana:**
Kuheshimu haki ya IPLCs ya kushiriki kikamilifu katika mchakato kamili wa ushauri kuhusu mpango wowote unaoweza kuwaathiri.

Inaungwa mkono kwa kushauriana na taasisi na wawakilishi wa IPLCs, na kupea wafanyakazi wakati na rasilimali za kutosha.

**Usawa:**
Ahadi ya kutenda kwa haki na kuheshimu kanuni ya maadili ya IPLC, maoni ya ulimwengu na maamuzi.

Inaungwa mkono kwa kugawana nguvu, fursa, rasilimali na faida.

**Uwajibikaji:**
Ahadi ya kuwa wazi, kuwajibikia makosa na kuyarekebisha, kutatua migogoro kwa haki, na kufuatilia na kuboresha shughuli na mbinu.

Inaungwa mkono kwa kuanzisha mikakati ya kutatua mgogoro kabla ya shida kutokea, kutekeleza na kusasisha mipango kwa kushirikiana, na kuandikisha kazi hiyo kwa njia za utamaduni.

**Nia Njema:**
Ahadi ya uaminifu wa bodi nzima, heshima, unyenyekevu, huduma na Uadilifu Bila Lawama.

Inaungwa mkono kwa kusikiliza, kutumia mafunzo kutoka kwa majadiliano yanayoendelea, kutafuta mawazo ya usawa na kufuatalia malengo ya ushirikiano wa usawa.

# Utangulizi wa Utafiti wa Kubuni

Mwongozo huu una utafiti wa kubuni uliotengenezwa ili tufurahie masuala muhimu. Maelezo ya ukweli na msingi wa utafiti wa kubuni umetambulishwa hapa chini na umezungumziwa katika moduli katika mfululizo wa matukio ya "Tuseme" yaliyobuniwa na "Mawazo & Mwongozo."




**Utangulizi wa Utafiti wa Wenland**
**Karibu Wenland**

Wenland ni kisiwa kikubwa kilicho chini ya Aktiki, kinachomilikiwa na jimbo la Ulaya la Albania. Nusu ya kaskazini ya kisiwa hicho kuna udongo jalidi kubwa mno, ambapo hakuna watu wengi sana. Mwishoni mwa karne ya 19, watu wa Wen, ambao walikuwa wahamaji Ulaya, walihamishwa kwa nguvu katika kisiwa hicho kama sehemu ya kuongezeka kwa utaifa na kutovumiliana kote Ulaya.

Tazama Utafiti

## Maelezo

[1] Garnett, S.T., Burgess, N.D., Fa, J.E. et al. A spatial overview of the global importance of Indigenous lands for conservation. Nat Sustain 1, 369–374 (2018).

https://doi.org/10.1038/s41893-018-0100-6

[2] Frechette et al. 2018 A Global Baseline of Carbon Storage in Collective Lands: Michango ya Wenyeji na Jamii ya Eneo hilo katika Kupunguza Mabadiliko ya Tabianchi.

https://rightsandresources.org/wp-content/uploads/2018/09/A-Global-Baseline_RRI_Sept-2018.pdf

[3] The Nature Conservancy. 2017 Strong Voices, Active Choices: Mfumo wa Mtaalamu wa TNC wa Kuimarisha Matokeo kwa Watu na Maumbile. Arlington, VA.

https://www.nature.org/en-us/what-we-do/our-insights/perspectives/strong-voices-active-choices/

[4] Tauli-Corpuz, Victoria. 2016 Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wenyeji. Uhifadhi na haki za wenyeji. Ripoti kwa Bunge:
http://unsr.vtaulicorpuz.org/site/index.php/en/documents/annual-reports/149-report-ga-2016

[5] Mkakati wa TNC wa Ulimwengu wa Wenyeji na Jamii za Eneo hilo (2016).

[6] Kujihusisha mpya kunaweza kutokea kutokana na mpango mpya au maafikiano mapya ya zinazoweza kuwa athari za mpango uliopo

[7] Baadhi ya mawazo yaliyo kwenye aya yalitolewa kutoka kwa Ofisi ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa ya Kamishna Mkuu. Kanuni Zinazoongoza Biashara na Haki za Binadamu: Utekelezaji wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa "Linda, Heshimu na Rekebisha" (haswa Kanuni ya 17). (2011):

https://www.ohchr.org/documents/publications/guidingprinciplesbusinesshr_en.pdf




# Karibu Wenland

## Utangulizi wa Utafiti wa Wenland

**Wenland ni kisiwa kikubwa kilicho chini ya Aktiki. Jimbo la Ulaya la Albian lilidai kwamba inamiliki Wenland katika kipindi cha upanuzi wa Albian mnamo miaka ya 1600.**

Kihistoria, watu wa Wen walikuwa wahamaji, na ardhi zao za jadi zinaenea Ulaya kote kuanzia kabla ya enzi za Kirumi. Mwishoni mwa karne ya 19 wakati wa kuongezeka kwa utaifa usiovumilika Ulaya, watu wa Wen walilazimishwa kuhamia Wenland. Walikaa kwenye sehemu ya kusini mwa kisiwa hicho, lakini wahamiaji wa Albania walipoanza kusafiri kwenda pwani ya kusini mwa Wenland na kukaa huko, watu wa Wen walisukumwa kwa kasi kaskazini kwenye eneo la udongo jalidi, linalojulikana kama Wend.

Mnamo 1934, serikali ya Albania ilitoa tangazo ikitangaza Wend kama nchi ya Wen. Walifadhili maendeleo ya kujitawala kwa Wen, lakini Bunge halikuridhia tangazo hilo. Serikali ya kisasa ya Albania haitambui tangazo hilo kuwa la kisheria, labda ilichochewa na raia wa Albania, ambao wengi wao wanapinga vikali wazo la nchi ya Wen. Hakuna mtu ambaye ameingilia kati ya umiliki wa Wen na utumiaji wa Wend, kwa hivyo watu wengi wa Wen hawatoi maoni na wanaepuka suala hilo.

Mnamo miaka ya 1970, kampuni za mafuta zilianza shughuli za upelelezi pwani bila kushauriana na watu wa Wen. Wafanyakazi wengi wa Albania walihamia kaskazini na leo hii miji mikubwa zaidi huko Wend ina nusu ya watu wa Albania na nusu ya watu wa Wen. Miji hii ina uchumi jumuishi na maeneo ya kazi, lakini ubaguzi wa kijamii na mivutano ya kikabila inaendelea. Vijiji vichache tu vya watu wa Wen-pekee vimetawanyika kote Wend.

Kuna vikundi vitatu tofauti vya Wen vya kijamii na vya ukoo: Wenna, Wenebe, na Wennec. Kwa pamoja, wanaitwa Kambi, ambayo inahusu kambi walizojenga walipofika Wend mwishoni mwa miaka ya 1800. Kambi za Wenna na Wenebe sasa ziko katika miji mikubwa, huku Wennec ikiwa na vijiji vidogo ambavyo vinajitegemea zaidi. Kwa kawaida Kambi hizo tatu hushirikiana lakini wakati mwingine zimeendeleza ushindani. Kambi za Wen huzungumza lahaja tofauti za Wennish, ingawa wote wanazungumza Kialbania, pia. Wanaijiji wa Wennec ndio wenye ujuzi mdogo sana katika Kialbania, huku Wenna na Wenebe wakiwa na ufasaha.

Jambo moja ambalo ni sawa kwa watu wote wa Wen ni kujifafanua wenyewe na kuishi kwao — na uhusiano na — watu wa Wend. Wanasimulia jinsi ambavyo watu wengi wasiohesabika walikuja Wend katika milenia, lakini ni watu tu wa Wen ndio waliwasikiliza na kujifunza kuishi nao kwa maelewano. Watu wa Wen wana ujuzi mwingi wa mazingira na wamejitolea kuilinda.

Vivyo hivyo, wamejitolea kulinda utamaduni wao, pamoja na lugha yao, mavazi ya kitamaduni na sherehe. Sherehe ya msimu wa kiangazi huleta watu wa Wen kutoka Kambi zote tatu kwenda kwenye sehemu takatifu kote Wend kwa mwezi wa sherehe, uzamaji katika shughuli za kitamaduni na ushauri kati ya Kambi.

Watu wa Wen wanadumisha taasisi zao za kujitawala, lakini wao ni raia wa Albian na wako chini ya mamlaka ya serikali ya wilaya ya Wenland.

# Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi



## Utangulizi

Shirika la Nature Conservercy linawaza kuhusu ulimwengu ambao utofauti wa maisha unastawi, na watu wanahifadhi maumbile kwa sababu yao wenyewe na uwezo wake wa kutimiza mahitaji yetu na kuboresha maisha yetu. Tunaongozwa na wazo kwamba ustawi wa watu wote unategemea mifumo ya ikolojia yenye afya, na kwamba afya ya mifumo hii ya ikolojia inategemea ustawi wa wale ambao wameyasimamia kwa vizazi vingi.

Leo hii, wenyeji na jamii za eneo hilo wanadhibiti angalau asilimia 25 ya ardhi za ulimwengu,[1] aslimia 17 ya kaboni ya misitu duniani[2] na sehemu kubwa zenye maji safi na makao ya viumbe vya baharini.  Ujuzi unaoendelea wa kiikolojia umekita mizizi katika tamaduni za IPLC, pamoja na kujihusisha sana na mahali na kujitolea bila kusita kwa ajili ya kulinda ardhi zao na maji. Ushahidi unaonyesha kwamba usimamizi unaoongozwa na wenyeji na jamii za eneo hilo unasababisha matokeo mazuri zaidi ya kuhifadhi, yanayodumu.[3] Kwa hivyo kuunga mkono uongozi wa IPLC, ni mojawapo wa njia zenye athari kubwa za kulinda maeneo muhimu, kushughuilikia mabadiliko ya hali ya hewa na kuwa na siku zijazo ambapo watu na maumbile yanastawi. Lakini kwa muda mrefu IPLCs wamekuwa wakiwekwa pembeni na kutengwa katika maamuzi yanayoathiri maeneo yao, tamaduni, riziki na ustawi. Uhusiano wao na ardhi zao, maji na maliasili zimedharauliwa au kutothaminiwa na watendaji wengine, ikiwa ni pamoja na mashirika ya kuhifadhi. Matokeo mabaya yanayosababishwa na kuhifadhi yemejumuisha:

- unyakuzi wa ardhi
- kulazimishwa kuhama
- kutokubaliwa kujitawala
- kutoweza kupata riziki na kupoteza utamaduni na maeneo takatifu
- kutotambuliwa na mamlaka zao
- kunyimwa haki na fidia, ikiwa ni pamoja na kurejeshewa gharama na fidia.[4]

Wenyeji na jamii za eneo hilo, na hasa wenyeji ambao ni wanawake, wamelipa gharama (na wamepokea faida chache) za juhudu za kuhifadhi zinazopuuza ujuzi wao, mtazamo, uongozi na haki. Mapambano dhidi ya ukoloni na ukandamizaji wa kimuundo yanaendelea, ingawa IPLCs wamejenga nguvu kubwa katika mazingira ya kisiasa ya ndani na ya kimataifa katika miongo ya hivi karibuni. Miaka thelathini iliyopita, wazo la haki zinazotambuliwa za wenyeji halikusikika sana. Mnamo 2007, haki hizi zilithibitishwa na mataifa 144 katika **Azimio ya Umoja wa Kimatifa kuhusu Haki za Wenyeji**. Ilipofika 2016, kila taifa ambalo lilikuwa limepinga UNDRIP mnamo 2007 lilikuwa limebadilisha mawazo, na kutambua ubora wa haki za wenyeji katika sheria ya kimataifa na ya ndani. Wenyeji wamesimama pamoja katika hali mbaya sana, na kupigania na kulinda haki hizi, ikiwa ni pamoja na haki ya kujiamulia mwenyewe na kiwango cha Idhini ya Kujitolea Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa.

TNC imejitolea kutumia mbinu inayozingatia haki za binadamu katika uhifadhi, kuunga mkono wenyeji wanapolinda na kutekeleza haki zao.

Kujitolea huko kunaonekana katika Ndoto, Maadili, Kanuni ya Mwenendo ya TNC na mbinu ya msingi wa uhifadhi. Tunatambua umuhimu wa Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa. Kuheshimu na kukuza haki za binadamu za IPLCs ni wajibu wa kimaadili na hali inayowezesha uhifadhi endelevu na ustawi wa binadamu. Uhifadhi wa ushirikiano unasaidia kazi ya IPLC ya kulinda tamaduni zao, riziki na kujihusisha na mahali – inayohakikisha siku zijazo ambapo maumbile na watu wanafanikiwa.

## Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi

Mwongozo umetengenezwa kwa Kanuni tisa na Sera za Kulinda Maslahi, ambavyo vinapaswa kuongoza kazi zote za TNC na IPLCs. Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zimeondolewa kwenye ahadi zilizopo, ikiwa ni pamoja na:

- Maadili yetu
- Kanuni yetu ya Mwenendo
- ahadi yetu kwa Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji,
- hasa vifungu 18-19 na 32 (ushiriki na FPIC), 23-26 na 29 (haki za ardhi na
- uhifadhi), 31 (haki za kitamaduni), na 40 (utatuzi wa mgogoro)
- mahitaji ya Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa kama ilivyoainishwa katika UNDRIP
- Mkutano wa ILO (Nambari 169) kuhusu Wenyeji na Watu wa Kikabila, na mamlaka nyingine
- Kanuni Zinazoongoza Mpango wa Uhifadhi kuhusu haki za Binadamu
- Muundo wa Uhifadhi 2.0 Mwongozo wa Hati (CbD 2.0)

Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi hujulisha na kuongoza mbinu ya TNC inayozingatia haki za binadamu katika uhifadhi na vimetajwa kama msingi wa kila moduli. Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi pia ni zana ya kutathmini na hutoa msingi wa orodha za kukagulia zilizo mwishoni mwa kila moduli.

Hakuna chochote katika Mwongozo huu kinachopaswa kuzuia majukumu yoyote ya haki za binadamu ambayo TNC imejitolea au inayofuata. Badala yake, **Mwongozo huu inarasimisha na kufafanua maadili, njia na desturi ambazo TNC inaheshimu ahadi ya kuheshimu na kukuza haki za binadamu za wenyeji na jamii za eneo hilo.**

### Kanuni Tisa na Sera za Kulinda Maslahi

**Uhuru wa Kuchagua na Kujiamulia Mwenyewe:**
**Ni nini:** Kuheshimu haki za wenyeji za kujiamulia mwenyewe na kujitawala, bila kuwatishia kwamba kutakuwa na matokeo mabaya au kuwalazimisha.
**Jinsi ya kuunga mkono:** Imeungwa mkono kwa kufanya mazungumzo ya heshima na IPLC na kuelewa athari za kihistoria na za leo za ukoloni, ukandamizaji na kutoikuwa na usawa wa nguvu.

**Kujihusisha Mapema na Mahusiano ya Ushirikiano:**
**Ni nini:** Kujihusisha mapema kwa IPLCs katika mpango wowote unaoweza kuwaathiri.
**Jinsi ya kuunga mkono:** Zingatia uongozi wa IPLC na kushiriki ipasavyo katika kubuni na kupanga maamuzi. Jenga uaminifu kadri siku zinavyokwenda.

**Kufanya Uamuzi baada ya Kuelewa:**
**Ni nini:** Kusaidia IPLC kufikia taarifa yote kuhusu shughuli ambazo zinaweza kuwaathiri, katika mazingira, lugha na miundo inayokidhi mahitaji yao.
**Jinsi ya kuunga mkono**: Wekeza wakati na rasilimali ili wafanyakazi wa IPLC na TNC wapate na waboreshe ujuzi. Jitolee katika kutathmini athari kwa bidii, mawasiliano wazi, kuheshimu njia nyingi za kujua na kujifunza pamoja kama msingi wa kufanya uamuzi.

**Haki ya Kukataa kutoa Idhini:**
**Ni nini:** Kuheshimu haki ya wenyeji ya kukataa kutoa idhini ya mipango ambayo wanaona kwamba inaweza kuwaathiri sana.

**Jinsi ya kuunga mkono:** Inaungwa mkono kwa kuheshimu uamuzi wa wenyeji wa kusema "ndiyo" au "hapana," pamoja na "ndiyo, lakini kwa masharti" na "hapana, lakini tuendelee kujadili."

**Ushauri wa Maana:**
**Ni nini:** Haki ya IPLCs ya kushiriki kikamilifu katika mchakato kamili wa ushauri kuhusu mpango wowote unaoweza kuwaathiri.
**Jinsi ya kuunga mkono:** Shauriana na taasisi na wawakilishi wa IPLCs, na uwape wafanyakazi wakati na rasilimali za majadiliano.

**Usawa:**
**Ni nini:** Ahadi ya kutenda kwa haki na kuheshima kanuni ya maadili ya IPLC, maoni ya ulimwengu na maamuzi.
**Jinsi ya kuunga mkono:** Kugawa nguvu, fursa, rasilimali na faida.

**Uhusishaji:**
**Ni nini:** Ahadi ya kusikiliza na kuthamini sauti tofauti na michango.
**Jinsi ya kuunga mkono:** Tumia mabaraza, vikao na michakato isiyo na ubaguzi, inayozingatia utamaduni na inayopatikana ili kutafuta michango kutoka kwa vitambulisho vyote vya kijamii.

**Uwajibikaji:**
**Ni nini:** Ahadi ya kuwa wazi, kuwajibikia makosa na kuyarekebisha, kutatua migogoro kwa haki, na kufuatilia na kuboresha shughuli na mbinu.
**Jinsi ya kuunga mkono:** Anzisha mikakati ya kutatua mgogoro kabla ya shida kutokea, tekeleza na usasishe mipango kwa kushirikiana, na uandike kazi hiyo kwa njia za utamaduni.

**Nia Njema:**
**Ni nini:** Kujitolea kwa uaminifu wa bodi nzima, heshima, unyenyekevu, huduma na Uadilifu Bila Lawama.
**Jinsi ya kuunga mkono:** Sikiliza. Inaungwa mkono kwa kusikiliza, kutumia mafunzo kutoka kwa majadiliano yanayoendelea, kutafuta mawazo ya usawa na kufuatalia malengo ya ushirikiano wa usawa.

## Muundo ya Mwongozo

Mwongozo huu una moduli sita, ambayo kila moja inaangazia Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi ambazo ni msingi kwa kila moduli.

**Moduli kwa Tazamo la haraka:**

**1.Kujifunza na Majadiliano ya Mwanzo**
Tambua IPLCs waliothiriwa na uwashirikishe kwa njia zinazoheshimu haki ya wenyeji ya kujitawala na kujenga uhusiano sawa

**2.Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa (FPIC)**
Tafuta na udumishe idhini ya mpango kupitia ushauri wa maana na kujifunza pamoja

**3.Utatuzi wa Mgogoro**
Jitayarishe kushughulikia kutoelewana kwokwote, migogoro au mizozo kwa kutumia njia za kitamaduni

**4.Utekelezaji**
Tumia Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi na mapendekezo yaliyo kwenye Mwongozo huu wakati wa kutekeleza mpango

**5.Kuandika Hati**
Andika hati kwa njia zinazojumuisha, zilizo wazi na ambazo IPLCs wanaweza kufikia na pia zinazokidhi mahitaji ya TNC

**6.Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho**
Fuatilia desturi za kufuata Kanuni na Viwango na mapendekezo yaliyo kwenye Mwongozo huu

## Maelezo

[1] Garnett, S.T., Burgess, N.D., Fa, J.E. et al. A spatial overview of the global importance of Indigenous lands for conservation. Nat Sustain 1, 369–374 (2018). Nat Sustain 1, 369–374 (2018). https://doi.org/10.1038/ s41893-018-0100-6

[2] Frechette et al. 2018 A Global Baseline of Carbon Storage in Collective Lands: Michango ya Wenyeji na Jamii ya Eneo hilo katika Kupunguza Mabadiliko ya Tabianchi.Indigenous and Local Community Contributions to Climate Change Mitigation. https://rightsandresources.org/ wp-content/uploads/2018/09/A-Global-Baseline_RRI_Sept-2018.pdf

[3] The Nature Conservancy. 2017 Strong Voices, Active Choices: Mfumo wa Mtaalamu wa TNC wa Kuimarisha Matokeo kwa Watu na Maumbile. Arlington, VA. file:///C:/Users/allison_martin/ Downloads/Strong_Voices_Active_Choices_FINAL.pdf

[4] Tauli-Corpuz, Victoria. 2016 Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wenyeji. Uhifadhi na haki za wenyeji. Ripoti kwa Bunge: http:// unsr.vtaulicorpuz.org/site/index.php/en/documents/annual-reports/149-report-ga-2016



## Moduli ya 1:

# Kujifunza & Majadiliano ya Mapema

Katika moduli hii:

Jifunze jinsi ya kutambua IPLCs wanaoweza kuathiriwa kupitia ukusanyaji wa data bila malipo na mahojiano

Tambua uwezo wa wafanyakazi wa IPLCs wanaojihusisha

Tengeneza Mpango wa Kujihusisha kabla ya mradi wowote kuanza

Kubaliana kuhusu njia bora ya kuanza mazungumzo

**Tafiti za Wenland:**

1A. TNC katika Wenland (TUKIO LA 1)

1B. TNC katika Wenland (TUKIO LA  2)

1C. Tatizo la Udongo Jalidi

1D. Kujitawala kwa Wen

## Utangulizi

Moduli hii inatoa mwongozo, vidokezo, na zana ambazo wafanyakazi TNC wanaweza kutumia: (1) tambua Wenyeji na Jamii za Eneo hilo ambao wanaweza kuathiriwa na shughuli za uhifadhi; (2) amua njia ya usawa na inayofaa zaidi, ya kushughulikia na kuzungumza na IPLCs hao; na (3) kuelewa vizuri miundo yao ya kijamii na kisiasa, malengo, matarajio na rasilimali wanazotegemea.

Ingawa kazi nyingi za TNC zinajumuisha miradi inayotegemea mahali, moduli hii inatumika kwa kila aina ya shughuli, ikiwa ni pamoja na miradi ya ardhini; miradi ya kiwango cha mazingira; mikakati ya kimipango, ya mkoa au inayozingatia nchi; na mipango ya sera. Kwa hivyo ni muhimu kuchambua athari zinazoweza kutokea kwa IPLCs hata kama sio dhahiri sana kwamba IPLCs wataathiriwa, kama katika kujihusisha katika sera ya kitaifa. Ikiwa uchambuzi unafunua athari zinazoweza kutokea, wafanyakazi wa TNC wanapaswa kuendelea kupitia moduli.

Mchakato huu unaweza kuonekana kuwa unatumika zaidi katika hali ambazo TNC ina wazo la mradi na kisha inaendea IPLCs kutafuta msaada. Hata hivyo, miradi ya TNC inaanza kwa njia nyingi. Wakati mwingine TNC hutambua IPLC mmoja au wengi ambao ni wasimamizi muhimu wa maliasili katika jiografia fulani na kuwaendea ili kupanga mipango kwa pamoja. Au IPLC anaweza kuendea TNC kwa msaada wa mpango wa uhifadhi. Katika hali hizi, moduli bado itakuwa na vidokezo na zana muhimu za jinsi ya kuendelea. Kwa mfano, ikiwa IPLCs ndio wanaendea TNC, unaweza kuacha mchakato wa kutambua IPLCs walioathiriwa. Lakini TNC bado inapaswa kutumia vidokezo vilivyo katika moduli hii ili kujifunza kuhusu miundo ya utawala wa IPLCs, michakato ya kufanya maamuzi na rasilimali ambazo IPLC wanaona kwamba ni muhimu zaidi. Utaratibu huu pia utasaidia kutathmini na kuimarisha ushirikiano uliowekwa.

## Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi

Utangulizi unajumuisha majadiliano ya Kanuni zote na Sera za Kulinda Maslahi vinavyotumika katika ushirikiano wa usawa. Nne ni muhimu sana katika kujenga uhusiano katika majadiliano ya mwanzo.

### Kanuni na Sera Muhimu za Kulinda Maslahi ya Majadiliano ya Mwanzo

**Kujihusisha Mapema na Ushirikiano:**
TNC inapaswa kuunga mkono jukumu kuu la IPLC katika kubuni mpango na uamuzi, badala ya kupelekea IPLC mpango kamili kwa ajili ya stempu ya idhini.

**Usawa:**
Haki na kujenga uaminifu unapaswa kuwa mstari wa mbele, ili kuhakikisha kwamba IPLC wanafikia nguvu, fursa na rasilimali kikamilifu.

**Uhusishaji:**
Mazungumzo yasiyokuwa ya ubaguzi yanahitajika na yanapaswa kuhusisha michango kutoka kwa vitambulisho vyote vya kijamii. Utoaji unapaswa kufanywa kwa ajili ya ufikiaji na vikao na michakato salama ya kimwili na kihisia.

**Uwajibikaji:**
Uwajibikaji unaweza kuhakikishwa wahusika wakiwajibika katika matendo yao, wakirekebisha makosa yao, wakijenga uaminifu na kuboresha mbinu wanapoendelea.

**Nia Njema:**
Kuonyesha imani nzuri, heshima, unyenyekevu na Uadilifu Bila Lawama kuanzia hatua ya kwanza ni muhimu sana katika kujenga uaminifu. Inaweza kuwa ngumu kuzuia makosa katika suala hili ikiwa yamefanywa mapema.

# Mwongozo

## Hatua ya Kwanza: Tambua Wenyeji Wanaohusika & Jamii za Eneo hilo

Ili utambue IPLCs wanaohusika, awamu tatu zifuatazo zinahitajika kwa kiwango cha chini:



1. **Ukusanyaji wa Awali wa Data Bila malipo**



2. **Mahojiano ya Awali ya Mtaalamu**



3. **Utafiti wa Awali wa Nyanjani**

1. **Ukusanyaji wa Awali wa Data Bila malipo**
   Timu ya TNC inachunguza taarifa zilizopo hadharani kuhusu IPLC wanaoweza kuathiriwa na maswala husika.
2. **Mahojiano ya Awali ya Mtaalamu**
   Timu hiyo inaongeza mafunzo yake na wataalamu ambao wamejihusisha na IPLCs kwa muda mrefu sana.
3. **Utafiti wa Awali wa Nyanjani**
   Timu inazungumza na viongozi na wawakilishi wa IPLC ili kujifunza jinsi ya kujishughulisha na IPLC bila kuingia katika kiini cha mashauriano, ambayo inapaswa kutokea baada ya Mpango wa Kujihusisha kutengenezwa.

Wafanyakazi wanapaswa kuunda faili kwa kumbukumbu ya baadaye na kuhifadhi taarifa inayofaa kutoka kwa rasilimali zifuatazo:

Kwa **Ukusanyaji wa Awali wa Data Bila Malipo,** wafanyakazi wanapaswa kuzingatia rasilimali zilizotajwa katika moduli hii, pamoja na yafuatayo:

- Utafutaji wa mtandaoni (kwa mfano, Google Scholar, HeinOnline, LexisNexis, ProQuest) kwa kutumia majina ya vikundi, mikoa, miji, majengo ya ukumbusho, viongozi au watu mashuhuri na matukio ya kihistoria. Hifadhi nakala muhimu kwa ajili ya wenzako na washiriki wa siku zijazo.
- Rasilimali za serikali: Tengeneza orodha ya mashirika ya serikali yenye kiwango chochote cha mamlaka ya kijiografia au mada (kwa mfano, idara za utunzaji wa mazingira, maliasili, uhifadhi, nishati, mambo ya ndani, maendeleo, mambo ya wenyeji, mambo ya wenyeji wa Australia, mambo ya kitamaduni) na tovuti za wakala wa utafutaji wa ripoti, kujihusisha kwa wadau wa shirika, na taratibu zinazofaa za udhibiti.
- Rasilimali za asasi za kiraia: Tengeneza orodha ya asasi za kiraia zenye historia yoyote ya ushiriki wa kijiografia au mada, kuanzia mashirika makubwa ya kimataifa ya rika mpaka vikundi vidogo vya maslahi vya eneo hilo, na uangalie tovuti kwa ajili ya ripoti, utetezi, ushahidi wa michakato ya zamani ya kujihusisha kwa wadau. IPLC pia wanaweza kuwa na tovuti, kurasa za Facebook na rasilimali nyingine za habari mtandaoni.
- Rasilimali za wataalamu na za kitaaluma: Tambua majina ya wasomi muhimu kutoka kwa utaftaji hapo juu. Vinjari bios za nyanja katika vyuo vikuu vya eneo hilo. Wasiliana na wakutubi wa kumbukumbu katika vyuo vikuu vya enepo hilo.

Kwa **Mahojiano ya Awali ya Mtaalamu**, wafanyakazi wa TNC wanapaswa:

- Kuandika hati ya kila mahojiano.
- Kuuliza kuhusu upeo wa kazi ya mtaalamu na kujihusisha na IPLCs, na pia matokeo yoyote au hitimisho.
- Kuuliza ni nani mwingine anayejua anayefanya kazi na IPLCs kwenye masuala husika. Kuandika ramani ya watu na mashirika wanaohusiana.
- Kuuliza kuhusu rasilimali muhimu wanazotegemea kujihusisha na IPLCs.
- Kuuliza ikiwa wako tayari kutoa maoni kuhusu maswali au mashaka yaliyotambuliwa kutoka kwa Data Uliokusanya Bila Malipo.
- Kurekodi maslahi ya mtaalamu au msomi au utayari wa kuulizwa maswali katika siku zijazo.

Kwa **Utafiti wa Awali wa Nyanjani**, wafanyakazi wa TNC wanapaswa kukumbuka:

- Lengo sio kukimbilia kwenye kiini cha mradi au maswala muhimu. Lengo ni kuelewa kwamba IPLCs ni akina nani na kukusanya taarifa ya Mpango wa Kujihusisha.
- Ni muhimu kuweka maelezo kwenye kila mahojiano.
- Katika mazingira ya ugomvi, kitendo tu cha kuzungumza na watu fulani kinaweza kutafsiriwa kama kuegemea upande fulani. Ni bora kuwasiliana na vyama rasmi vya IPLC au taasisi kwanza, kwa mfano, chama kikuu cha utawala cha IPLC, au idara ya usimamizi wa maliasili. Ikiwa kuna mashaka, nenda polepole. Sisitiza kwamba TNC wanasikiliza tu na wanawakaribisha wadau wote na wamiliki wa haki bila vizuizi.

### Kidokezo: Kutegemea Utaalamu wa Ndani

Wafanyikazi wa TNC wanaweza kushauriana na Timu ya Watu wa Asili ya Jamii na Jamii za TNC, ambao wana utajiri wa rasilimali za ndani na wanaweza kuwaunganisha wafanyakazi na wenzao ulimwenguni kote katika Mfumo wa Sauti Shupavu, Chagua na Hatua.

### Rasilimali: LandMark Mapping Platform

LandMark ni jukwaa la kuchora ramani ambalo hutoa habari kuhusu haki za ardhi na maliasili za IPLC kote ulimwenguni, iliyoundwa na Taasisi ya Rasilimali za Dunia na washirika.

- LandMark hutoa habari kamili kuhusu sehemu nyingine za ulimwengu (Amerika Kusini na Asia ya Kusini mashariki) kuliko kwingine (Afrika).

**Masuala Muhimu: Uwezo wa Wafanyakazi wa TNC**

Ni muhimu kwamba wafanyakazi wa TNC wanaoshiriki katika kujihusisha wa hatua ya mapema wawe na uzoefu, mafunzo na uwezo wanaohitaji. Uhusishjai unaozingatia utamaduni sio otomatiki kwa kila mtu. Mara tu unapojifunza, ustadi wa mbinu tofauti za kitamaduni zinahitaji kufanywa na kuhimizwa. Ukurasa wa Mafunzo Tofauti kwenye intaneti ya CONNECT ya TNC ina rasilimali kadhaa kwenye mada kama vile kulinganisha tofauti na kuwezesha uhusishaji.

**Masuala Muhimu: Je akina nani huchukuliwa kama IPLCs?**

Hapa hakuna ufafanuzi mmoja wa wenyeji au IPLCs. Hata hivyo, ufafanuzi mwingi unarejelea seti ya mambo ambayo IPLC wengi hupitia kwa kawaida ulimwenguni. "Kulingana na UN njia bora zaidi ni kutambua, badala ya kufafanua wenyeji. Hii inategemea kigezo cha msingi cha kujitambulisha kama ilivyoainishwa katika hati kadhaa za haki za binadamu. "[1]

Mambo ya kawaida ambayo IPLC wameshuhudia ni:

- Kujitambulisha kama wenyeji kama mtu binafsi na kukubaliwa na jamii kama mwanachama wao
- Mwendelezo wa kihistoria na jamii za kabla ya ukoloni au kabla ya walowezi
- Kujihusisha sana na eneo na maliasili
- Mifumo tofauti ya kijamii, kiuchumi au kisiasa
- Lugha tofauti, utamaduni na imani
- Kuwa sehemu ya vikundi visivyo na nguvu vya jamii
- Kujitolea katika kudumisha na kuendeleza mazingira na mifumo ya mababu zao kama watu na jamii tofauti

Ni muhimu pia kutambua athari mbaya ambazo ukoloni umekuwa nazo - na zinaweza kuendelea kuwa nazo - kwa IPLCs. Mambo haya yanajumuisha:

- Mateso mabaya wakati wa enzi za ukoloni na baada ya ukoloni
- Kuhamishwa kwa nguvu
- Idadi ya watu waliangamaizwa na vurugu au magonjwa
- Watoto walioibiwa katika shule za bweni

Kwa kuwa wamepitia mambo haya, na wanajua utofauti wa wenyeji, na mara nyingi mamlaka huepuka kufafanua jamii kama "wenyeji." Mojawapo ya kesi muhimu za wenyeji za haki za ardhi *(Saramaka People vs. Suriname)* zilitumia kanuni za haki za wenyeji kwa jamii ya wazao wa Kiafrika wanaoishi Amerika Kusini. Jamii ilianzishwa na watu watumwa ambao walitoroka na wakaunda utamaduni uliojitegemea na uhusiano mkubwa na ardhi iliyowadumisha. Katika visa vingine vingi, wenyejji waliondolewa kwa nguvu kutoka nchi zao za jadi bado wanapigania kuirudisha.

TNC na mashirika mengine mengi ya uhifadhi na maendeleo huchagua kuongeza faida za ulinzi zinazohitajika na wenyeji kulingana na sheria kwa ajili ya jamii nyingi za eneo hilo walioathirika. Kwa sababu ya aina ya kazi ambayo TNC inafanya, lengo letu ni kwa jamii zilizo na uhusiano mkubwa na mazingira yao ya asili.

**Rasilimali: Laha ya Wenyeji wa UN**

Kwa taarifa zaidi kuhusu neno "wenyeji," angalia Jukwaa la Kudumu la UN kwenye Laha ya Masuala ya Wenyeji

**Rasilimali: Muktadha wa Neno "IPLC" katika TNC**

Kwa muktadha wa neno "IPLCs," angalia Mfumo wa VCA (ukurasa wa 6). TNC hutumia neno **wenyeji na jamii za eneo hilo** kurejelea watu na jamii ambazo zina uhusiano mkubwa na mandhari yao ya asili, ambayo wanategemea kwa ajili ya ustawi wa kitamaduni, kiroho, kiuchumi na kimwili. Wakazi wa asili na wahamiaji ambao wana uhusiano wa karibu na mandhari vile vile huchukuliwa kuwa IPLC. TNC inatambua haki za pamoja za watu wa kiasili kama ilivyoainishwa katika sheria za kimataifa. Katika Mwongozo huu, "IPLCs" hutumiwa kurejelea watu wote ambao ni wenyeji na jamii za eneo hilo.

**Suala Muhimu: Upeo wa Uchunguzi**

IPLC ambao wanaweza kuathiriwa na mpango huo lazima watambuliwe. Ikiwa mpango huo unategemea mahali, mchakato wa kitambulisho unajumuisha kupanga ramani za mipaka ya mradi na kuamua ikiwa kuna IPLC ambao wanaishi, wanatumia au wanathamini ardhi, maji na rasilimali zilizo ndani au karibu na mipaka hiyo. Wapangaji wanapaswa kuzingatia wafugaji wa kuhamahama au wawindaji / wakusanyaji ambao wanaweza wasiwepo kwa sasa, lakini ambao hutumia ardhi hiyo wakati mwingine. Kwa kazi ambayo haifanywi mahali au inayoweza kutekelezeka kwa urahisi, kama vile mipango ya sera, bado ni muhimu kutambua IPLC ambao wanaweza kuathiriwa.

Ramani ya mipaka ya mpango (ikiwa ni ya kijiografia, sera au inahusiana na mkakati) inapaswa kujumuisha maeneo ambayo shughuli zitatokea au athari zitaonekana. Kulindwa kwa vyanzo vya maji ya mto kunaweza kuathiri jamii ya mto, au usimamizi wa maeneo ya nyasi katika eneo moja unaweza kuathiri maeneo ya nyasi katika eneo lingine ikiwa itabadilisha mifumo ya malisho ya wafugaji wa kuhamahama.

Upeo wa uchunguzi haupaswi kuhusu tu matumizi ya ardhi ya leo; matumizi ya kihistoria yanapaswa kujumuishwa. Wala uchunguzi haupaswi kuhusu tu ardhi ambayo IPLCs zina hakimiliki au haki za matumizi zilizoandikwa rasmi. IPLCs nyingi zitakuwa na haki za kukaa kimila au kutumia haki ambazo hazitambuliki na serikali.

Inaweza kuwa ngumu kujua ikiwa jamii zitaathiriwa na mpango, kwa hivyo wafanyakazi wanapaswa kuwa na mtazamo mpana. Shughuli kwenye kipande cha ardhi zitaathiri jamii iliyo na haki miliki ya ardhi, na inaweza kuathiri jamii nyingine ambazo zina haki zisizotambuliwa kisheria lakini zinachukulia kwamba ardhi ni takatifu au wanaitumia kwa madhumuni ya kidini au mengine. Kuzingatia zaidi ya masilahi ya kisheria na kiuchumi ni muhimu; kwa kuzingatia masilahi ya kitamaduni, kiroho, kiafya na, na mahitaji ya kujikimu huhakikisha uchunguzi mzuri.

**Rasilimali: Ramani ya Ardhi ya Asili Inayoweza kutafutwa ya Wilaya**

Ardhi ya Asili inajumuisha ramani inayoweza kutafutwa, inayohusisha watu wa maeneo ya jadi, lugha na mikataba kote ulimwenguni.

**Suala Muhimu: Kukinzana kwa Maoni ya IPLC au Madai ya Haki**

Ni kawaida kupata IPLCs wawili au wengi wanaodai umiliki wa jadi, ufikiaji au kutumia haki za ardhi moja. Huenda jamii ilitumia ardhi hiyo kwa sherehe za kidini, huku nyingine ikiwa na historia ndefu ya kulisha ng'ombe huko. Au kunaweza kuwa na kutokubaliana kuhusu mipaka. Ni muhimu kutambua IPLCs wote wanaohusika na kuelewa asili tofauti ya kila dai.

Wafanyakazi wanaweza kuamua kuwa madai yanayopingana au yanayoshindana ni mengi sana au yanaleta utata kwa mradi kusonga mbele. Katika visa vingine, kusaidia jamii kufanya kazi pamoja licha ya madai ya kushindana na kuwaleta pamoja ili wafuatilie malengo ya uhifadhi kunaweza kusababisha mpango wenye nguvu na matokeo endelevu zaidi. Hata hivyo, TNC haipaswi kuwa mwamuzi wa mizozo kati ya jamii. Hilo ni jukumu ngumu na gumu ambalo halihusu utaalam wa TNC.

**Rasilimali: Zaidi kuhusu Madai ya Ushindani wa Kitaifa**

Kwa wafanyakazi ambao wanataka kujifunza mengi kuhusu kuwezesha mazungumzo kati ya IPLCs na madai yaliyopo, Mwongozo wa Wawezeshaji wa Ulinzi wa Ardhi ya Jamii ya Namati una sura mzuri zinazohusu Kulinganisha Mipaka na Kutatua Migogoro ya Ardhi (kurasa za 151-166). Sura hizi zinahusu mada kama vile jinsi ya kuunda timu kutoka kila jamii ili iongoze katika kusuluhisha migogoro, jinsi ya kutoa mafunzo ya utatuzi wa migogoro na upatanisho, na jinsi ya kuchagua mpatanishi mzuri.

**1A. Utafiti wa Wenland**

**TNC katika Wenland (TUKIO LA 1)**

TNC ina ofisi kadhaa katika Albania upande wa bara na katika miji ya Albania huko Wenland.

Tumeweza na tumeshiriki katika mipango kadhaa ya uhifadhi wa Albania tangu mwishoni mwa miaka ya 1980. Mradi wetu pekee katika Wend hadi sasa ulikuwa upunguzaji wa uhifadhi wa pwani uliofadhiliwa na wafadhili wa kibinafsi mnamo 1997.

Tazama Utafiti

## Hatua ya Pili: Mpango wa Ushauri na Mchakato

**Kiolezo: Mpango wa Kujihusisha**

Tazama Kiolezo cha Mpango wa Kujihusisha

IPLC wanapotambuliwa, mchakato wa kuandaa Mpango wa Kujihusisha utasaidia kuamua njia za kujihusisha zinazofaa kitamaduni na sawa. Kujifunza kuhusu mila, miundo ya kijamii, uhusiano wa kijinsia, nguvu na tabaka katika IPLC ni muhimu. Lengo kuu la hatua hii ni kuhakikisha kwamba TNC inafanya kazi na taasisi za utawala za IPLC na inaheshimu mila, sheria, kanuni na mila zao za kijamii. Kwa kufanya hivyo, wafanyakazi wanapaswa pia kutumia mbinu inayojumuisha na inayotambua na kushirikisha vikundi vyote vya kitambulisho cha kijamii.

Lazima TNC ihusishe IPLCs katika mazungumzo na mashauriano kwa njia ambayo inaheshimu na kuchangia katika uhuru wa IPLC, na inaunga mkono vipaumbele na maono yao kwa siku zijazo. Hii inahitaji kuelewa hali za kihistoria na za sasa na kujitolea katika kujifunza pamoja na kuheshimiana.

**Kujihusisha Mapema na Mahusiano ya Ushirikiano:**
TNC lazima ichukue muda kuelewa kabisa mtazamo wa IPLC kabla ya kuwa na maoni kuhusu mpango. Moduli ya Kujifunza na Majadiliano ya Mwanzo inapendekeza Mazungumzo ya Awali na Mpango wa Kujihusisha unaozingatia utafiti ambapo pande zote zinakubaliana kuhusu atakayeshiriki na jinsi ambavyo majadiliano yatafanywa. Mbinu hiyo inapaswa kuendelezwa katika mashauriano rasmi, kujifunza historia, kufanya uamuzi na idhini. IPLC wanaweza kuondoa idhini wakati wowote, na hawapaswi kamwe kupiga kura ya kukubali au kukataa

pendekezo ambalo wanaweza kukubali kwa kiwango fulani pekee. Badala yake, pendekezo linapaswa kutengenezwa na IPLC au kwa kushirikiana na TNC.

**Kufanya Uamuzi baada ya Kuelewa:**
Ili waweze kutathmini athari, lazima IPLC wapate taarifa yote kuhusu shughuli zinazowaathiri, kwa mpangilio, lugha na muundo unaokidhi mahitaji yao.

**Usawa:**
Haki na kujenga uaminifu unapaswa kuwa mstari wa mbele, ili kuhakikisha kwamba IPLC wanafikia nguvu, fursa na rasilimali kikamilifu.

**Uhusishaji:**
Ushirikiano, kufanya uamuzi na mazingatio ya idhini hayapaswi kuwa yenye ubaguzi. Michango kutoka kwa vitambulisho vyote vya kijamii inapaswa kujumuishwa na vitu vipaswa kutolewa kwa ajili ya ufikiaji na vikao na michakato salama ya kimwili na kihisia.

**Haki ya Kukataa kutoa Idhini:**
Wenyeji wanaweza kukataa kutoa idhini ya mipango ambayo itawaathiri wakati wowote. Hii ni kweli hata ikiwa mchakato wa kina, wa gharama kubwa wa mashauriano umeshatokea. Mara nyingi pingamizi nyingine zinaweza kutatuliwa kuzuia kukataliwa kabisa kwa mpango huo. Kwa sababu hiyo, pamoja na majibu ya "ndiyo" na "hapana" kwa ombi la idhini, majibu ya "ndiyo, lakini kwa masharti" na "hapana, lakini tuendelee kujadili" yanapaswa kutolewa.

## Kuelewa FPIC

Ufafanuzi wa FPIC, msingi wa kisheria wa FPIC, na gharama na faida za kupata FPIC iliyojadiliwa hapa chini ni uchambuzi wa kina, ambayo ni jambo jipya katika moduli nyingine zilizo kwenye Mwongozo huu. FPIC ni jambo ngumu, lenye utofauti ndogo na muhimu katika kujihusisha kwa IPLC. Ikiwa unataka kujifunza mengi kuhusu historia na mabadiliko ya FPIC, angalia Kiambatisho cha IV Maswali yanayoulizwa Mara kwa Mara ya FPIC.

### Ufafanuzi wa FPIC

Wenyeji wana haki ya kujiamulia wenyewe. Uhuru wao dhidi ya vitambulisho vyao, utamaduni na vipaumbele vya maendeleo hutegemea uwezo wao wa kujitawala, kuishi katika ardhi zao, kudumisha utamaduni wao na kujikinga dhidi ya ushawishi usiofaa wa jamii inayowazunguka ya wakoloni au inayotawala. FPIC ni kiwango cha kimataifa cha upimaji wa kisheria kwa kujihusisha na IPLCs - na maamuzi yanayoathiri IPLCs – ili kuhakikisha kwamba tunaheshimu haki yao ya kujiamulia wenyewe.

FPIC inahakikisha kwamba wenyeji wanaweza kutoa au kukataa kutoa idhini ya mipango inayowaathiri. Lakini FPIC haihusu tu kutoa au kukataa kutoa idhini. Ni mchakato unaoendelea wa kulinda haki ya wenyeji ya kujiamulia wenyewe, kuruhusu majadiliano ya maana na uhuru wa kufanya maamuzi bila vitisho.[1]

TNC imejitolea kutekeleza FPIC sio tu kwa ajili ya kutii maagizo ya Umoja wa Mataifa, bali pia kwa sababu mbinu zinazozingatia haki za binadamu za uhifadhi ni: (a) iliyofungamana na Kanuni yetu ya Mwenendo na Heshima kwa Watu, Jamii na Tamaduni; na (b) ni muhimu kwa uhifadhi mzuri, wa kudumu. FPIC ni muhimu katika kujenga uhusiano sawa ambao umejikita katika uaminifu na kuleta matokeo mazuri endelevu kwa watu na maumbile.

Mamlaka nyingine zimebadilisha "C" iliyo katika FPIC kumaanisha "kushauriana" badala ya "idhini." Kwa kiwango fulani, hii inaweka mkazo unaofaa katika mashauriano, mkazo wa TNC, unaojionyeshwa katika kanuni ya msingi ya Ushauri wa Maana. Kuondoa neno "idhini," hata hivyo, kunaweza kuashiria kusita kukubali haki ya kukataa kutoa idhini. Kwa upande mwingine, TNC inatambua na kuheshimu haki hiyo katika usemi wake kamili.

**Kufafanua Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa.**

**Ya Kujitolea**
Kujitolea kunamaanisha idhini inayotolewa bila kulazimishwa, vitisho au ujanja. Kujitolea sana kwa TNC kwa dhana hii kunaonyeshwa katika Uhuru wa Kuchagua na Kujiamulia Mwenyewe, ulioelezewa katika Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi.

**Inayotolewa mapema**
Inayotolewa mapema inamaanisha kwamba idhini inapaswa kuombwa sio tu mapema kabla ya idhini yoyote au kuanza kwa shughuli, lakini katika hatua za mwanzo za maendeleo ya mradi, kabla ya maamuzi muhimu kufanywa. Lengo hili linaweza kuwa ngumu kufikia katika utekelezaji, kwa hivyo mipango makini na kujizuia kunahitajika katika hatua za mwanzo za mpango huo. Soma zaidi katika sehemu ya Kujihusisha Mapema na Mahusiano ya Ushirikiano.

**Baada ya kuelewa**
Baada ya kuelewa inamaanisha kwamba IPLC anaweza kufikia taarifa yote muhimu kuhusu kusudi la mradi huo, ukubwa, upeo na kipindi cha muda wake, wanaoweza kuwa washiriki, na tathmini ya athari. Athari zinazoweza kutokea ni pamoja na za mazingira, haki za binadamu, za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kitamaduni. Taarifa inapaswa kutolewa katika miundo na lugha zinazozingatia utamaduni, inayokidhi mahitaji ya watu kutoka vitambulisho tofauti vya kijamii. Wakati wa kutosha lazima utumike kujifunza kuhusu masuala ya msingi, kufuatilia, na kuruhusu mazungumzo ya IPLC na kati ya IPLC na TNC.

**Idhini**
Idhini inamaanisha uamuzi wenye mamlaka na halali wa pamoja uliofanywa na IPLC, kwa kutumia michakato yake ya kawaida ya kufanya uamuzi. TNC inaheshimu kabisa haki ya wenyeji ya kukata kutoa idhini. IPLC wanaweza kusema “ndiyo,” “hapana,” “ndiyo, lakini kwa masharti,” na “hapana, lakini tuendelee kujadili” katika shughuli zozote zilizopendekezwa.

**Rasilimali: Kuelewa FPIC kwa Kina**

Kwa mjadala wa kina zaidi kuhusu kila kipengee cha FPIC, angalia kurasa za 15 na 16 za mwongozo wa FAO Idhini ya Kujitolea Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa: Haki za wenyeji na desturi nzuri za jamii za eneo hilo.

## Msingi wa Kisheria wa FPIC

Kiwango cha FPIC kimebadilika katika miongo iliyopita. Sasa ni sehemu ya mikataba mingi ya kimataifa, kama vile Azimio la UN kuhusu Haki za Wenyeji – UNDRIP – na Mkataba wa Tofauti ya Kibaolojia.

Imetajwa pia katika sera za serikali na taasisi za kimataifa, sheria ya kesi ya korti za kitaifa na mahakama za haki za binadamu za kimataifa, mamlaka ya majukwaa ya wadau na wa kimataifa (kama vile Baraza la Usimamizi wa Misitu), viwango vya hiari katika sekta binafsi, pamoja na ahadi za NGOs kama TNC.

Kujitolea kwa TNC kwa FPIC kunatokana na vyanzo hivi vya sheria na mwongozo, ambavyo vinatambua jukumu la msingi la FPIC katika kulinda haki ya wenyeji ya kujiamulia mwenyewe. UNDRIP haswa inahitaji serikali ishiriki katika FPIC na TNC inaamini kwamba watendaji wasio wa serikali wanashiriki jukumu hili pia

**Rasilimali: FPIC katika Sheria ya Kimataifa**

Kwa muhtasari kamili wa vyombo muhimu vya sheria vya kimataifa ambavyo vimetaja FPIC na kusaidia katika kuunda mabadiliko yake, angalia Kiambatisho cha 2 katika Baraza la Usimamizi wa Misitu FSC miongozo ya utekelezaji wa haki ya idhini ya kujitolea, inayotolewa mapema na baada ya kuelewa ) (2012).

FPIC imetazamwa kama kanuni ya kisheria iliyoundwa kulinda haki maalum za wenyeji. Lakini FPIC pia inatumika katika kujihusisha na jamii za wenyeji ambao wanachama wao hutambulika kidogo kama wenyeji, ambao hawajidai kuwa wenyeji, au ambao hawatambuliki na serikali kama wenyeji, lakini ambao wanadumisha vitambulisho tofauti na tamaduni zilizohusiana na ardhi ambazo wamemiliki au kutumia kwa vizazi. TNC imechukua mbinu hii kwa kufanya Mwongozo na taratibu zake, itifaki na mwongozo utumike na jamii za eneo hilo pamoja na wenyeji.[2]

## Gharama na Faida za FPIC

Wafanyakazi wanapaswa kufahamu na kujitayarisha kushughulikia gharama na faida za mchakato wa FPIC. Hata hivyo, FPIC sio ya hiari, bila kujali gharama na faida. Kwa kweli, gharama za awali za mchakato kamili wa FPIC mara nyingi husababisha matokeo mazuri na endelevu kwa watu na maumbile, ambayo inaweza kupunguza jumla ya gharama kwa muda. Kwa madhumuni ya kupanga, bajeti ya FPIC inapaswa kujumuisha wafanyakazi na wakati wa IPLC wa kujenga uhusiano na gharama za kufanya mikutano inayojumuisha, kukusanya na kusambaza taarifa, na kuwasiliana na IPLC. Bajeti ya ufafanuzi wa hali mbili tofauti zinawasilishwa katika utafiti wa kesi ya Wenland. Matoleo ya baadaye ya Mwongozo huu yatajumuisha mwongozo zaidi kuhusu gharama na upangaji wa bajeti ya FPIC.

**Utafiti wa Wenland: Bajeti ya Kubuni**

Bajeti ya Kubuni

Mchakato wa FPIC unahitaji muda, rasilimali na kujitolea. Wengine wanaweza kuhisi kwamba FPIC ni ngumu sana au inachukua muda mwingi na kwamba itaacha kazi ya uhifadhi ikiingiliwa na mizozo ya kiutaratibu au kisiasa. Wengine wanaweza kuona kwamba mchakato ni wazi sana na hauna uhakika. Mashaka yote yanaeleweka.

Hata hivyo, ni hadithi tofauti, katika shughuli. Vipengele vya FPIC ni kubwa lakini pia ni rahisi na yenye ufanisi. Mchakato wa FPIC ukipata vizuizi vikali, labda viliibuka wakati fulani katika kipindi cha mpango.

FPIC husaidia kila mtu kutarajia masuala ambayo yangegharimu zaidi ikiwa zingeshughulikiwa baadaye katika mchakato, ikiepuka makosa ambayo yangesababisha madhara yasiyoweza kurekebishika.

IPLC wanatarajia mchakato wa FPIC, zaidi na zaidi. Kwa kuikubalia kikamilifu, TNC inaweza kuweka uhusiano wake kwa uaminifu, usawa na ushirikiano wa kweli. Na faida za baadaye ni kubwa. Hatari za kupuuza FPIC pia ni kubwa. Hatari hizi ni pamoja na kuzuiliwa au kuondolewa kwa msaada na wamiliki wakuu wa haki au wadau pamoja na hatari ya sifa.

Uwezekano kwamba idhini inaweza kukataliwa, ikizuia kuendelea kwa mpango ambayo TNC inajali sana, lazima ikubalike kwa unyenyekevu na kuthamini kwa upana muktadha wa ulimwengu. Hatari mahususi zaidi zinapaswa kuzingatiwa, kama uwezekano kwamba utekelezaji wa FPIC katika eneo ambalo serikali ya jimbo au serikali ya eneo hilo ina uhasama kwa wenyeji inaweza kuongeza hatua za kulipiza kisasi zinazoelekezwa kwa jamii ya eneo hilo au kwa TNC kwa kuunga mkono haki zao.[3] Moduli hii itasaidia wafanyakazi kujifunza na kujiandaa kwa hatari hizi, huku pia ikiangazia faida za muda mfupi na mrefu za njia inayozingatia haki za binadamu kwa uhifadhi.

**Rasilimali: Mazungumzo ya ziada ya FPIC**

Kwa orodha ya changamoto zaidi za kuzingatia wakati wa kutekeleza FPIC, angalia ukurasa wa 178 katika: Lewis, Jerome. "Jinsi ya kutekeleza idhini ya kujitolea, inayotolewa mapema baada ya kuelewa." Kujifunza kwa Kushiriki na Utendaji, 65 (2012): 175-178.

## Hatua Muhimu katika Mchakato wa FPIC

Hatua muhimu za mchakato wowote wa FPIC zinapaswa kuwa sawa katika kuweza kubadilishwa na kazi ya uhifadhi ya TNC ulimwenguni, huku pia ikitoa mwongozo thabiti na muhimu. Hatua hizi za FPIC zinachukulia kwamba wafanyakazi wameshatumia Moduli ya Kujifunza na Majadiliano ya Mwanzo ili kutambua na kuanza mazungumzo na IPLC ambao wanaweza kuathiriwa na mpango. Katika hali ya uhusiano wa muda mrefu wa IPLC na miradi iliyopo, wafanyakazi wanapaswa kutumia Moduli ya Kujifunza na Majadiliano ya Mwanzo na Moduli ya Kuandika Hati ili kurekodi vidokezo muhimu vya ushirikiano.

Kuanzia hatua hiyo, mchakato wa FPIC unajumuisha hatua zifuatazo:

- Hatua ya Kwanza: Jenga Uwezo wa ndani wa FPIC
- Hatua yaPili: Kuandaa Mpango wa Ushauri
- Hatua ya Tatu: Pata Idhini

# Mwongozo

### Hatua ya Kwanza: Jenga Uwezo wa ndani wa FPIC

TNC lazima ijenge uwezo wetu wa ndani kabla ya kushirikiana na wawakilishi wa IPLC. Baadhi ya hii ingetokea wakati wafanyakazi walimaliza Moduli ya Kujifunza & Majadiliano ya Mwanzo, lakini uwezo wa wafanyakazi unapaswa kupitiwa tena na kuimarishwa ikiwa inahitajika.

Timu ya TNC inapaswa kujumuisha watu ambao wana uzoefu wa kushirikisha jamii katika mazingira nyeti ya kitamaduni. Huenda hii isiwe kawaida kwa kila mtu. Ukurasa wa Mafunzo Tofauti iliyo kwenye wavutindani wa TNC's CONNECT hutoa rasilimali kuhusu kukubali utofauti na kukuza uhusishaji.

Timu ya TNC inapaswa kujumuisha utaalamu katika lugha maalum, historia na tamaduni za IPLC, na washirika wa nje au washauri wanapaswa kushirikishwa ikiwa utaalamu huu hauwezi kupatikana ndani. Washauri hawa wanaweza kujumuisha watu ndani ya IPLCs, NGOs za eneo hilo au wasomi wanaojulikana na wanaoheshimiwa na IPLCs.

Mwishowe, wafanyakazi wa TNC wanapaswa kuwa wanyenyekevu, wazi katika kujifunza utamaduni na mawasiliano, na kujitolea katika usawa na uhusishaji. Wafanyakazi wanapaswa pia kuwa washirika wa kweli na walio tayari kuwajibikia makosa yetu.

**Kidokezo: Fanya Mpango wa Mafunzo ya Kushirikiana**

Ikiwa Kitengo cha Biashara cha TNC kimefanya kazi na IPLC wengine, Kitengo cha Biashara kinaweza kuzingatia mpango wa mafunzo ya kushirikiana, ambapo wawakilishi kutoka kwa ushirikiano wa IPLC uliopita huletwa pamoja na wale wa ushirikiano unaowezekana. Wanaweza kuuliza maswali kuhusu uaminifu wa TNC, mbinu na kujitolea kwa muda mrefu. Mipango hii inaweza kujenga uaminifu na kukumbusha pande zote kwamba mchakato bora wa FPIC hauendelezi tu mpango maalum, inaunga mkono ndoto kubwa ya IPLC ya kujiamulia wenyewe.

**Masuala Muhimu: Upeo wa Uwezo Unaohitajika**

Hapa chini kuna orodha ya uwezo unaoweza kuhitajika kwa ajili ya mchakato wa FPIC. TNC inapaswa kuamua ni ustadi gani ambao tayari inayo ndani na inayopaswa kutolewa nje. Timu inapaswa kuwa na uwezo wa:

- Kuendeleza ushirikiano wa usawa unaotegemea imani na ushirikiano
- Kuwezesha mashauriano, pamoja na wanawake na wanachama wa vitambulisho vingine vya kijamii
- Kushirikiana na IPLC ili ielewe matumizi ya ardhi, maji na maliasili, pamoja na zinazoweza kuwa tofauti katika jinsia, umri, ufikiaji, n.k.
- Kuwakilisha TNC na itoe ahadi za kisheria kwa niaba yake
- Kufanya tathmini ya athari za mazingira, uchumi, kijamii na haki za binadamu
- Kujumuisha taarifa ya kiufundi na kisayansi na ujuzi wa wenyeji IPLC wakiamua kupeana taarifa hiyo
- Wasiliana na viongozi wa IPLC na maafisa wa serikali (jua kwamba: Wawakilishi wa TNC wanapaswa kuwa na mamlaka na cheo ndani ya TNC kilicho sawa na ya viongozi au maafisa wa IPLC)
- Kuelewa (a) sheria au kanuni za serikali au za eneo hilo, na (b) sheria ya kimataifa ya haki za binadamu, haswa matarajio ya haki au majukumu ambayo IPLC wanaweza kuwa nayo. Haya yanaweza kuhusiana na ardhi, hali ya mazingira, kufikia taarifa, kujitawala au hakimiliki
- Kuchambua, kutoa taarifa na kutoa ushauri kuhusu faida za kiuchumi na hatari za fursa za maendeleo

- Kuunda na kudumisha rekodi zinazohakikisha uwazi na uwajibikaji
- Kutoa msaada au kujenga uwezo wa kazi zozote muhimu za utawala, kwa mfano, usimamizi wa kifedha

**Suala Muhimu: Mfumo wa Sheria za Eneo hilo**

Wafanyakazi wanapaswa kuelewa mfumo wa kisheria wa nchi mwenyeji wa kujihusisha na IPLC. Je nchi ina sheria au kanuni zozote kuhusu FPIC, umiliki wa ardhi, matumizi ya kimila, matumizi ya rasilimali au haki nyingine za IPLCs? Kujua sheria, kanuni na viwango vinavyohusika kutasaidia wafanyakazi kuhakikisha mchakato wa FPIC unaofikia matarajio. Baadhi ya mambo yaliyoelezewa katika moduli hii ambayo yameambatana na desturi bora ya kimataifa yanaweza kuzidi mahitaji ya kisheria ya eneo hilo au kitaifa.

**Rasilimali: Kutafuta Sheria za Eneo hilo kuhusu FPIC**

Klambatisho cha 5 cha mwongozo wa FAO "Idhini ya Kujitolea Inayotolewa Mapema na Baada ya Kuelewa: Haki ya wenyeji na desturi nzuri kwa jamii za eneo hilo" inajumuisha mfumo unaofaa wa kutafuta sheria za eneo hilo kuhusu FPIC.

Mifano ya taarifa inayofaa kuhusu mfumo wa kisheria:

- Msaada wa nchi kwa UNDRIP
- Sheria za kitaifa zinazounga mkono FPIC au michakato inayofanana
- Ufafanuzi wa mashirika ya haki za binadamu na haki za wenyeji kuhusu michakato ya FPIC nchini

## Hatua ya Pili: Mpango wa Ushauri na Mchakato

**Kiolezo: Mpango wa Ushauri**

Tazama Kiolezo cha Mpango wa Ushauri

Majadiliano ya mapema yanapaswa kufuata Mpango wa Kujihusisha kutoka katika Moduli ya Kujifunza & Majadilaino ya Mwanzo. Hii inakusudiwa kuzungumzia jinsi ambavyo TNC itawasiliana na IPLC katika miundo, lugha, na vikao vinavyofaa. Wakati TNC na IPLC wako tayari kuendelea katika mchakato wa mashauriano ya FPIC, Mpango wa Kujihusisha uliopo unapaswa kuendelezwa zaidi kuwa Mpango wa Ushauri.

Wakati Mpango wa Kujihusisha ulilenga hasa "nani" na "vipi," Mpango wa Ushauri wa FPIC unalenga sana

"nini." Je mambo muhimu ya majadiliano ni gani? Je shughuli gani zinapendekezwa? Je mambo gani yanaweza kuwa athari, gharama na faida kwa TNC na IPLC? Mpango wa Ushauri unaweza kuwa mfupi na rahisi, na muundo unapaswa kukubaliwa na TNC na IPLC.

Yaliyomo na lengo la Mpango wa Ushauri hutegemea IPLC na mpango maalum. Mwongozo mfupi tu ndio unaweza kufupishwa, kwa hivyo timu ya TNC inapaswa kufanya kazi na IPLC ili kutathmini na kupea kipaumbele athari za haki za binadamu au palipo na mashaka kuhusu mpango huo. Ushauri unapoendelea na ujifunzaji mpya unatokea, majadiliano haya yanapaswa kubadilika na kuongezeka.

Kuna aina nyingi tofauti za mchakato wa aina hii: tathmini ya athari, uchambuzi wa hatari, hatua za kuepuka makosa na tathmini ya walengwa ni mbinu kadhaa zilizoainishwa na wataalamu na watendaji.

**Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu**

Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu (HRIA) ni njia ya kufanya uchambuzi wa muundo wa athari na mashaka yanaoweza kutokea yanayohusu mpango. Rasilimali nyingine kuhusu HRIA zimebainishwa hapa chini. Kuna aina nyingi za modeli na mbinu, ambazo zinaweza kufaa katika mahitaji ya mpango. Kwa mfano, tathmini ya walengwa inalenga maoni yaliyopo katika jamii.

Kampuni ya ushauri wa haki za binadamu NomoGaia inaelezea mchakato wake wa msingi kama tathmini ya hatari, ambayo ni ndogo kuliko tathmini kamili ya athari. Uchunguzi wa hatari unachambua:

1. Haki au haki zilizoathiriwa
2. Vikundi vyote vyenye haki
3. Ukali wa athari inayoweza kutokea
4. Uwezekano wa athari inayoweza kutokea au suala la haki
5. Sababu za msingi za hatari
6. Hali na kiwango cha kujihusisha na mpango au shughuli

Hatua za Kuepuka Makosa za Haki za Binadamu, zilizofafanuliwa katika Kanuni za UN Zinazoongoza za Biashara na Haki za Binadamu ni mbinu nyingine inayotumiwa sana HRDD inakusudia "kutambua, kuzuia, kupunguza na kuelezea jinsi ambavyo [kampuni] zinashughulikia athari mbaya za haki za binadamu." Vipengele vinne ni:

1. Kutathmini athari halisi na zinazoweza kutokea za haki za binadamu'
2. Kujumuisha matokeo ya tathmini na kutekeleza hatua za kupunguza athari
3. Kufuatilia majibu na matokeo
4. Kuwasiliana na wadau wote na wamiliki wa haki kuhusu jinsi ambavyo athari zinashughulikiwa

Hakuna mbinu moja inayofaa kwa kila tukio. Kulingana na hali maalum, timu ya TNC inapaswa kuchagua moja na kuendelea chini ya Kanuni za Kujiamulia Mwenyewe, Uhusiano wa Kushirikiana na Nia Njema. Timu ya TNC inapaswa kuendelea kufanya utafiti na kushauriana na wataalamu, alafu kushiriki mambo inayojifunza na IPLC katika mazungumzo na ushirikiano, bila kufanya hitimisho thabiti mpaka mtazamo wa IPLC ujumuishwe kabisa.

Tathmini ya athari na maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mashaka yatatumika katika kipindi chote cha mpango wa kubuni Mpango wa Utatuzi wa Migogoro, kuchagua maeneo ya kuzingatia kwa utekelezaji (angalia Moduli ya Utekelezaji) na kuunda viashiria vya ufuatiliaji, tathmini na marekebisho (tazama Moduli ya Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho).

**Desturi nzuri za Mchakato wa Kuthibitisha Athari za Haki za Binadamu**

**Pea kipaumbele (kwa kitengo ikiwa inahitajika)**
Ushauri unapaswa kuwa wa kina, lakini watu wanaweza kupoteza msukumo ikiwa kuna taarifa nyingi tofauti. Ikiwa kuna masuala mengi, weka kipaumbele kwa kategoria ili uruhusu mbinu yako iwe ya kina na fupi.

**Wasikilize IPLC**

Kipaumbele kinapaswa kutoka katika vyanzo viwili:

1. Je IPLC wanajali sana kuhusu nini? Athari inayoweza kutokea inaweza kuwa kipaumbele ikiwa itaathiri kitu kinachothaminiwa na IPLC.
2. Je athari muhimu zaidi ya mpango katika suala la mabadiliko ya kijamii, kitamaduni, mazingira, uchumi au udhibiti ni gani?

**Tarajia kwamba tathmini itabadilika**
Hakikisha unaacha nafasi ya sehemu zote za tathmini—ikiwa ni pamoja na maoni ya IPLC kuhusu mambo muhimu zaidi—kubadilika kukiwa na taarifa mpya na IPLC kuwa na taarifa zaidi kuhusu athari za mpango huo.

**Fikiria mitazamo na matokeo kadhaa**
Eneo lolote la mashaka litakuwa na athari dhahiri ya awali. Tathmini ya kimfumo inavumbua athari na inazingatia athari za muda mfupi na mrefu, mitazamo tofauti, biashara na kulipa sehemu ya ushuru. Timu za TNC zinapaswa kuzingatia mpango huo kwa upana na matokeo yake kwa kuzingatia haki zilizoainishwa katika UNDRIP, kama vile kujiamulia mwenyewe, haki za eneo na ulinzi dhidi ya kuondolewa kwa nguvu, haki za utamaduni na ulinzi dhidi ya kulazimisha wenyeji wafanane nao, na haki za kujitawala na usaidizi wa kifedha na kiufundi.

Mbali na tathmini ya athari, Mpango wa Ushauri unapaswa kujumuisha:

- Kupanga ratiba - muhtasari wa mahali na wakati mashauriano yatatokea.
- Bajeti - makadirio ya gharama ambazo kila chama kitapata wakati wa mchakato wa mashauriano na jinsi ambavyo IPLC watalipwa fidia kwa ushiriki wao.
- Hatua muhimu – Hii inahakikisha kwamba majadiliano yanaendelea ipasavyo na yanaendelea kwa kasi nzuri kwa watu wote, na kwamba TNC na IPLC wanaendelea kujitolea kwa mchakato huo.
- Kuandika hati – Moduli ya Kuandika hati inatoa vidokezo na zana zinazofaa za kuhakikisha hati kamili, thabiti, na za kitamaduni. Maswali ya kuzingatia:
  - Je nani ataandika nini?
  - Je mikutano, simu na hatua nyingine katika mchakato huo zitarekodiwa na kuelezewa vipi?
  - Je kumbukumbu za mkutano zitahifadhiwa wapi na zitapeanwa vipi?
  - Je mipango ya hati za FPIC zinaambatana na mahitaji yoyote ya kuandika hati ya TNC kwa ajili ya mpango huo?
  - Je hati zinahifadhiwa katika muundo ambao unapatikana kwa urahisi kwa wafanyakazi

(ambao wanaweza kuja na kuondoka katika kipindi cha mpango) na ushirikishwe kwa urahisi na kuhifadhiwa na washiriki wa IPLC?

### Rasilimali: Mwongozo wa Ziada wa FPIC

Ukurasa wa 43 ya miongozo ya utekelezaji wa FSC FPIC inajumuisha orodha muhimu ya mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa Mpango wa Ushauri unaoelezea jinsi vyama vitawasiliana na kushauriana.

Kwa orodha ya masuala ya kuzingatia wakati wa kuunda Mpango wa Ushauri, angalia matobo yaliyo kwenye ukurasa wa 21 wa Miongozo ya FPIC ya shirika la Conservation International.

Orodha nyingine nzuri ya vitu ambavyo vinapaswa kujumuishwa katika mfumo wa FPIC uliokubaliwa unaweza kupatikana katika Sehemu ya 1.3, ukurasa wa 38, wa Miongozo ya utekelezaji wa FSC FPIC.

Asili ya Usawa na Jarida la Biomaterials Endelevu zina mwongozo kuhusu ushahidi unaokubalika wa michakato ya FPIC katika Kuwezesha FPIC Kupitia Viwango vya Hiari, Ripoti ya Mradi, Julai 2018.

### Rasilimali: Rasilimali za Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu

Mwongozo wa UN Global Compact kwa Tathmini na Usimamizi wa Athari za Haki za Binadamu ni chanzo cha msingi cha kutekeleza HRIA. Karatasi ya ukurasa mmoja ya haki za msingi za binadamu iko kwenye ukurasa wa 62 wa HRIAM.

NomoGaia: Tathmini ya Hatari ya Haki za Binadamu: Mwongozo wa Watendaji na Mwongozo wa Mfanyabiashara wa Tathmini ya Hatari ya Haki za Binadamu.

Biashara kwa Wajibu wa Jamii: Kufanya Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu.

Chombo cha "Kupata Ni Sawa" cha Oxfam kwenye Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu kina taarifa, tafiti na kijenzi cha hifadhidata inayoweza kubadilishwa.

Kwa mwongozo unaofaa wakati unashirikiana na IPLCs katika tathmini ya athari wakati wa mchakato wa mashauriano, angalia Mkataba wa Utofauti wa Biolojia Akwé: Miongozo ya Hiari ya Kon. Sehemu ya IV ya miongozo hiyo inajumuisha taarifa kuhusu kujumuisha tathmini za athari za kitamaduni, za mazingira na za kijamii katika mchakato mmoja na masuala na maswali ya kuzingatia katika kila sehemu.

### Suala Muhimu: Idhini kama Mchakato

Hata kama IPLC anapenda kushirikiana na TNC, ***mchakato wa FPIC hauwezi kufupishwa au kuharakishwa.*** Mkutano mmoja wa mwanzo labda hautoshi kufanikisha kanuni ya Kufanya Uamuzi Baada ya kuelewa. TNC na IPLC wanapaswa kushughulikia makubaliano maalum, wazi (yaliyoandikwa) ambayo yanakubaliwa rasmi na taasisi za IPLC. Makubaliano haya yanaweza kufichua masuala ambayo hayakuwasilishwa kwenye mikutano ya mwanzo ambayo yanahitaji kushughulikiwa.

Kwa hivyo TNC inapaswa kudumisha mbinu thabiti na kamili hata kukiwa na msisimko halali kuhusu makubaliano ya pande zote. Mchakato wa FPIC ni wa kurudiarudia, na kasi na maendeleo yatategemea watu wanaohusika na hali ya kila mpango. Hakuna kanuni ya watu wote kuhusu idadi ya kufanya mikutano, wala mara ngapi. Kwa mfano, mikutano ya jamii ya kilimo ambayo hufanyika kila wiki au kila mwezi inaweza kuhitaji kucheleweshwa wakati wa msimu wa uvunaji. Hiyo inaweza kuwa kweli katika mikutano ya jamii ya wafugaji ambayo inahitaji kusafiri kutafuta nyasi wakati wa ukame. TNC haipaswi kulazimisha mikutano ikiwa hii itatokea. Badala yake, mchakato unapaswa kubadilishwa kila wakati ili kukidhi mahitaji ya IPLC.

Katika mikutano ya baadaye, lengo moja linapaswa kuwa kufikia makubaliano kwamba kipengee cha "kuelewa" kwa FPIC kimetimizwa. Mipango ya uhifadhi inaweza kuwa ngumu, kwa hivyo kunaweza kuwa na migogoro ya mara kwa mara au kubadilisha masuala husika hapo mbeleni. Wafanyakazi wanapaswa kukumbuka kwamba mchakato huo unahusu kujielimisha kuhusu jinsi ambavyo IPLC wanaona mpango huo kwa kuwa inahusu kushiriki maoni ya TNC. Mara nyingi, mchakato wa kina au hata mgumu wa FPIC unatoa timu yenye nguvu, yenye usawa katika utekelezaji.

### Kidokezo: Jitayarishe kwa Mchakato wa Kurudiarudia wa FPIC

Idhini inahitaji mchakato wa kurudiarudia unaojumuisha kuwasilisha mpango huo, kuuliza maoni kutoka kwa IPLC, kurekebisha vigezo kulingana na maoni na kutafuta makubaliano ya kuendelea. Mazungumzo haya kati ya TNC na IPLC mara nyingi hujikita kwenye rasilimali zinazostahili kulindwa, jinsi zinapaswa kulindwa, fidia ya uharibifu wowote wa rasilimali, na makubaliano kuhusu kugawana faida.[4] Ikiwa mpango huo unajumuisha kujenga uwezo, majadiliano yanaweza kuzingatia upeo na madhumuni yake, watu ambao watapewa, na matarajio kuhusu majukumu ya washiriki wa IPLC.

### Rasilimali: Mada za Majadaliano

Kwa orodha ya kina ya mada zinazojadiliwa wakati wa mchakato wa FPIC, na suluhisho zinazoweza kupatikana za kutatua mgogoro wakati wa majadiliano hayo, angalia matobo yaliyo kwenye ukurasa wa 56 na 57 wa Mwongozo wa FSC wa Kutekeleza Haki ya Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na ya Baada ya kuelewa Kwa masuala yanayohusu migogoro, angalia pia Moduli ya Utatuzi wa Mgogoro ya Mwongozo huu.

### Suala Muhimu: Kuhakikisha Uhusishaji

Uhusishaji umeripotiwa mara kwa mara kama suala muhimu la kuzingatia. Katika hatua hii, TNC inapaswa kujumuisha mafunzo yake ya mapema ili kufanya uchambuzi wa kijinsia na IPLC ili kupata mpango kuhusu Mwendeleo wa Kuunganisha Jinsia na kukuza desturi zinazofaa za kufuatilia na usaidizi, kama vile Hatua za Kufikia Malengo ya Kijinsia. Kwa maelezo ya kina kuhusu Kuunganisha Jinsia ya Shirika la CARE na hatua za kuunganisha usawa wa kijinsia,

angalia Mwongozo wa TNC wa Kujumuisha Usawa wa Kijinsia katika Uhifadhi.

Mbali na jinsia, TNC inapaswa kuchambua masuala mengine yoyote ya uhusishaji. Mchakato wa FPIC unahitaji kujengwa kwa ufahamu, marekebisho na kuunga mkono usawa wa vitambulisho vyote vya kijamii. Angalia Kiambatisho cha II – Faharasa ya Maneno Muhimu kwa orodha ya vitambulisho vya kijamii vya kufikiria.

**Suala Muhimu: Uwezo wa Jamii**

Wakati mfumo wa ushirikiano na usawa unaoendelea, wahusika wote wanapaswa kutathmini mahitaji ya uwezo wa IPLC, jinsi ambavyo TNC ilitathmini uwezo wake katika Hatua ya Kwanza. Ujuzi wa IPLC wa dhana ya FPIC lazima iamuliwe kwanza. Kisha tathmini: kiwango cha kujitolea kwao kwa mchakato; fidia ya wakati wao; uwezo wao wa kutuma, kupokea na kuhifadhi taarifa kwa ufanisi; na uwezo wao wa kuhudhuria au kupanga mikutano. **Tathmini ikifichua kwamba IPLC wanaweza kufaidika na usaidizi wa mtu asiyehusika moja kwa moja, ikiwa ni pamoja na ushauri kutoka kwa mshauri wa kisheria waliomchagua ili kuhakikisha kwamba wanaelewa gharama na faida na vipengee vya sheria vya mpango huo, TNC inapaswa kuzingatia bajeti.**

Katika kuamua jinsi ambavyo taarifa itapeanwa, timu zinapaswa kuelewa lugha inazopendelewa (zinazopendelewa) na IPLC, viwango vya uwezo wa kusoma na kuandika, na jinsi ambavyo IPLC wanapendelea kupokea taarifa: kwa mdomo, kwa macho kwenye picha au video, kwa maandishi, kupitia vielelezo au michoro, au njia nyingine.[5] Taarifa inaweza kuhitaji kupeanwa kwa njia tofauti na vikundi tofauti. Angalia Moduli ya Kuandika hati ya Mwongozo huu kwa taarifa zaidi.

**2A. Muungano wa Mashauriano wa Utafiti wa Wenland**




FrostLock imefanya mkutano wa mashirika ya asasi za kiraia, mashirika ya serikali ya kitaifa ya Albania na Wenland na Halmashauri za Wen kwa ajili ya mashauriano kuhusu uwezekano wa kupeleka teknolojia yake katika udongo jalidi wa Wenland.

Tazama Utafiti

## Hatua ya Tatu: Uwasilishaji wa Mwisho na Kutafuta Idhini

Watu wanapoelewa pamoja kuhusu ushirikiano uliopendekezwa, kama kawaida TNC itaandaa Uwasilishaji wa mwisho au Muhtasari, au itashirikiana na IPLC kwa mchakato kama huo. Muhtasari utajumuisha matokeo ya mwisho, makubaliano yaliyofikiwa, na matarajio muhimu au mawazo ya msingi. Wakati wa mashauriano, wakati mwingine wahusika huzungumza tu wanapofikiria au kuongea kwa masharti, kwa kuwaza au kwa muda, ambayo inaweza kusababisha kutoelewana kuhusu yanayokubaliwa na yasiyokubaliwa katika mpango wa jumla wakati wa kuendelea mbele. Uwasilishaji wa Mwisho

utaelezea nia na uhakikisho wa TNC kwa njia thabiti ambapo uamuzi wa IPLC wa idhini unaweza kuzingatiwa. Muhtasari au uwasilishaji pia unaweza kufaa kwa ajili ya Kuandika hati, kama ilivyojadiliwa katika Moduli ya Kuandika hati.

Uwasilishaji wa mwisho au Muhtasari unaweza kuchukua aina nyingi. Inapaswa kubadilishwa ili ikidhi mahitaji na mapendeleo ya IPLC, na iwasilishwe kwa lugha na muundo unaopendelea wa IPLC. Inaweza kuwa ya mdomo, sherehe au sehemu ya utaratibu wa kitamaduni au desturi ambayo IPLC watachagua. Katika visa hivi, TNC inapaswa kuzingatia kuweka toleo la maandishi la Uwasilishaji wa Mwisho kama sehemu ya Mpango wake wa Kuandika hati. Uwasilishaji wa Mwisho unapaswa kutolewa kwa kufuata kabisa taratibu na matarajio ya IPLC na taasisi zao za uongozi.

**Masuala Muhimu: Kuwekea Idhini Ukumbusho**

Idhini ya IPLC, ikitolewa, inapaswa kuwekewa ukumbusho katika Makubaliano ya Idhini. Wahusika wote lazima wakubaliane kuhusu itakavyotekelezwa. TNC inaweza kutaka kuandika idhini kwa njia moja (kumbukumbu zilizoidhinishwa za mkutano wa uamuzi au kauli iliyoandikwa ya idhini, kwa mfano) na IPLC wanaweza kutaka kuiandika kwa njia nyingine (sherehe au utaratibu, kwa mfano). TNC inapaswa kuheshimu njia inayopendelewa na IPLC, huku pia ikitaka kukidhi mahitaji yake ya shirika.

Ikiwa TNC inahisi kwamba maelezo fulani ya idhini yanahitaji kuandikwa (angalia zana zinazofuata hapa chini kwa mambo ya kawaida ya Makubaliano ya Idhini Yaliyoandikwa), na viwango vya lugha zilizoandikwa na IPLC vinaunga mkono jambo hili, TNC inaweza kuomba Makubaliano ya Idhini uliotiwa saini kabla ya kutoa rasilimali zake.

Hata hivyo, TNC inapaswa kuepuka kutimiza matakwa yake ya hati, kwa kuwaomba viongozi wa IPLC watie saini kwenye hati ambazo hawawezi kusoma. Ambapo hakuna lugha iliyoandikwa, au uwezo mdogo wa kusoma na kuandika, ni bora kwa TNC kurekodi idhini ya mdomo kwa ruhusa na kuihifadhi pamoja na hati iliyoandikwa inayoelezea kwamba TNC imeelewa idhini lakini haionekani kuwa ya lazima kwa IPLC. Angalia Moduli ya Kuandika hati kwa taarifa zaidi.

**Rasilimali: Vipengele vya Makubaliano ya Idhini**

Mwongozo wa FAO Idhini ya Kujitolea Inayotolewa Mapema na ya Baada ya kuelewa: Haki ya wenyeji na desruri nzuri kwa jamii za eneo hilo inajumuisha orodha nzuri ya mada ambayo inapaswa kuzungumziwa na vifungu vinavyopaswa kujumuishwa katika Mkataba wowote wa Idhini.

Vipengele vya kawaida vya Makubaliano ya Idhini ni pamoja na lugha inayoainisha maeneo ya kijiografia ambayo hayaruhusiwi, njia za kuhesabu na kutoa fidia yoyote ambayo italipwa kwa jamii, njia za kutatua migogoro, na mipango ya ufuatiliaji na tathmini.

**Suala Muhimu: Kudumisha Idhini**

Idhini ikishatolewa, utekelezaji unaweza kuanza. Shughuli za utekelezaji zinapaswa kuchunguzwa mara kwa mara dhidi ya Makubaliano ya Idhini ili kuhakikisha

kwamba masharti ya idhini bado yanatimizwa. Ni muhimu pia kupitia tena Makubaliano ya Idhini maamuzi makuu yanapotokea, wawakilishi wa TNC au IPLC wanapobadilika au awamu mpya katika mpango huo zinapotarajiwa. TNC na IPLC wanapaswa kufuatilia Makubaliano ya Idhini kupitia majadiliano ya ufuatiliaji na ukaguzi. Muundo, idadi ya marudio na kuandika hati za majadiliano haya kunapaswa kukubaliwa mapema. Utaratibu huu wa kudhibitisha idhini inayoendelea unapaswa kuimarisha ushirikiano wa IPLC na TNC kadri mpango unavyoendelea na hali inavyobadilika.

**Suala Muhimu: Nani Anazungumza kwa niaba ya Jamii**

Wakati mwingine ni vigumu kujua ni nani kutoka IPLC aliyeidhinishwa kutoa idhini. Je mtu, kikundi cha watu au shirika gani huongea kwa niaba ya IPLC na kusema "ndiyo" au "hapana"? Je iwapo IPLC wanatofautiana kimawazo? Kwa matumaini TNC itakuwa imezoea michakato ya kufanya uamuzi ya IPLC iliyo katika Hatua ya Kwanza na Hatua ya Pili. Lakini kukiwa na migogoro au mkanganyiko, TNC lazima ijifunze mengi kuhusu mbinu za kufanya uamuzi za IPLC, ikitumia utaalamu wa jamii na nje ipasavyo. TNC inapaswa kujaribu kufikia makubaliano mapana kuhusu kufanya uamuzi hata kama kuna tofauti kubwa kuhusu uamuzi wa mwisho. Kisha, wafanyakazi wanapaswa kuwaambia IPLC jinsi wanavyopanga kuendelea.

Ikiwa wafanyakazi wa TNC hawawezi kuthibitisha makubaliano kwa ujasiri, wanapaswa kusitisha mchakato huo na kutafuta maoni na ushauri kutoka kwa Timu ya TNC ya Ulimwengu ya Wenyeji na Jamii na eneo hilo na wafanyakazi wenzao walio katika Mfumo wa VCA.

**Suala Muhimu: Idhini dhidi ya Ushauri**

IPLC wana uhuru wa kusema "ndiyo" au "hapana," na pia "ndiyo, lakini kwa masharti" na "hapana, lakini wacha tuendelee kujadili" kama jibu la Uwasilishaji wa Mwisho. Wanaweza pia kuonyesha kwamba wamekataa kutoa idhini kwa kukataa kushiriki katika majadiliano mengine. IPLC wakikataa kushiriki, wafanyakazi wanapaswa kuheshimu chaguo hilo na wasiendelee kuwasiliana nao. IPLC wakikubali sehemu nyingine za mradi na kukataa nyingine, TNC lazima ielewe sehemu zinazokubaliwa na zisizokubaliwa. Kusikiliza IPLC kwa ukaribu na kujumuisha mashaka na maoni yao katika Makubaliano ya Idhini kutasaidia sana katika kuhakikisha mafanikio ya mpango huo.[6]

Mchakato wa FPIC wa TNC unaweza kutofautiana na michakato fulani ya serikali inayoendeshwa na FPIC ambayo ni ya michakato ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa, ambayo serikali ina mamlaka kamili kuhusu uamuzi. Angalia Kiambatisjo cha IV – Maswali ya Mara kwa Mara ya FPIC kwa muhtasari wa tofauti kati ya mashauriano na idhini. Michakato hii inaweza kuwa halali na inayolingana na tawala za kisheria zinazoheshimu haki za IPLC. TNC, hata hivyo, kama watendaji wengi wasio wa serikali, imejitolea kutofuata mpango isipokuwa ikiwa Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa itatolewa na IPLCs wote walioathiriwa.

Ahadi hii haimalizi majadiliano kuhusu idhini; hali ngumu bado zinaweza kutokea. Kwa mfano, iwapo IPLC mmoja aliyeathiriwa sana anatoa idhini na anataka kuendelea, huku IPLC ambaye hajaathiriwa sana anakataa kutoa idhini? Je iwapo IPLC ambaye ameathiriwa kidogo na mradi muhimu anakataa kutoa idhini? Je iwapo IPLC anadai kwamba ataathiriwa na kudai mchakato wa FPIC, lakini wafanyakazi wa TNC au waangalizi wengine hawaamini kwamba madai ya athari yanaaminika?

Hakuna majibu rahisi. Kila hali lazima ishughulikiwe kulingana na hali hiyo. Lakini wafanyakazi wa TNC wanapaswa kuamini kwamba makubaliano yanawezekana katika hali nyingi. Misheni ya TNC ni kuhifadhi ardhi na maji ambayo viumbe vyote vinategemea. IPLCs hushiriki maadili haya kwa undani zaidi kuliko wengi kwa sababu vitambulisho vyao mara nyingi vimeunganishwa bila usawa na ulimwengu wa asili. Maneno ya maadili hayo wakati mwingine yanaweza kuwa tofauti sana na, pamoja na mifumo kandamizi iliyokita mizizi, usawa wa nguvu, na urithi wa ukoloni, inaweza kusababisha migogoro, kama ilivyotokea mara nyingi kati ya vikundi vya uhifadhi na IPLCs hapo zamani. FPIC inatoa njia yenye matumaini, na ya kuaminika zaidi, ya siku zijazo zenye matokeo tofauti.

**2B. Utafiti wa Wenland**
**Idhini na Haki ya Kukataa kutoa Idhini**




Kuna mashaka kuhusu FrostLock na teknolojia yake, lakini Baraza la Wen linasema watatoa idhini. Wanatambua kuwa uzito wa hali hiyo — kwa udongo jalidi na kwa sayari — unahitaji hatua hata kama matokeo hayana uhakika.

Tazama Utafiti

## Orodha ya kukagulia ya FPIC



### Hatua ya Kwanza: Jenga Uwezo wa Ndani

☐ Hakikisha kwamba timu ya TNC ina ustadi unaohitajika au inaweza kuzipata nje.

- Zingatia Ukurasa wa Mafunzo Tofauti wa TNC kama rasilimali kuhusu mada kama vile kulinganisha tofauti na kuunda uhusishaji
- Timu ya TNC inapaswa kujumuisha utaalamu katika lugha, historia na tamaduni za IPLCs wanaohusika, na kujitolea katika kushirikiana na kujifunza utamaduni na mawasiliano

☐ Tengeneza Mpango wa Kuandika hati.

- Fanya kazi kwa kushirikiana na IPLC ili mutengeneza mpango huo
- Kukubaliana kuhusu atakayeandika mambo fulani na kwa muundo gani
- Tambua mshiriki wa timu ya TNC ambaye atahifadhi rekodi kulingana na mahitaji ya TNC

☐ Elewa sheria ya nchi mwenyeji kuhusu mahitaji ya FPIC, ukikumbuka kwamba TNC imejitolea kwa mchakato ambao unaweza kuzidi mfumo wa kisheria wa eneo hilo.

### Hatua ya Pili: Mpango wa Ushauri na Mchakato wa FPIC

☐ Shirikiana na IPLC katika kuunda Mpango wa Ushauri unaojumuisha:

- Mbinu iliyokubaliwa ya tathmini ya athari, ijumuishe athari za haki za binadamu za shughuli zinazopendekezwa (inapaswa kusasishwa wakati majadiliano ya mashauriano yanaendelea):
  - Athari nzuri
  - Athari mbaya, pamoja na ukali, uwezekano na sababu za hatari
  - Upunguzaji uliopendekezwa wa athari mbaya zilizoelezewa hapa juu
  - Mpango wa kufuatilia majibu na matokeo na wa kuwasiliana kuhusu jinsi ambavyo athari zinashughulikiwa
- Kupanga ratiba
- Kuandika bajeti
- Hatua kuu
- Kuandika Hati

☐ Fanya mikutano katika maeneo na wakati ambao IPLC watachagua, ikiwa ni pamoja na mikutano ya ziada au vifungu vya vitambulisho tofauti vya kijamii, ikiwa ni lazima.

☐ Andika hati ya mawasilisho yaliyotolewa na TNC, IPLCs na wengine ili urekodi matokeo na makubaliano.

## Orodha ya kukagulia ya FPIC (Inaendelezwa)



### Hatua ya Tatu: Uwasilishaji wa Mwisho na Kutafuta Idhini

- [ ] Fanya uwasilishaji wa mwisho au muhtasari unaoelezea nia na uhakikisho wa TNC kwa njia thabiti ambapo uamuzi wa IPLC wa idhini unaweza kuzingatiwa.

  - Tengeneza uwasilishaji kulingana na muktadha na matarajio ya IPLC
  - Katika hali ya mdomo, sherehe au desturi nyingine za kimila, TNC inaweza kutaka kuzingatia kuhifadhi hati zilizoandikwa kwa ajili ya rekodi zake:
    - Andika waliohudhuria
    - Andika kumbukumbu
    - Hifadhi rekodi ya maandishi ya uwasilishaji

- [ ] Idhini ikitolewa:

  - Kukubaliana kuhusu njia ya kutoa idhini
  - Hakikisha kwamba mashaka na maoni ya IPLC yamejumuishwa katika Makubaliano yoyote ya Idhini
  - Andika walioshiriki katika mikutano ya Makubaliano ya Idhini
  - Unda mpango wa wakati na jinsi ya kukagua tena Makubaliano ya Idhini

## Hati za Kuhifadhi

**Angalia Moduli ya Kuandika hati kwa muktadha wa ziada na mazingatio ya hati**

☐ Maandalizi ya Ushauri

- Orodha ya uwezo unaohitajika kwa mchakato wa FPIC ukionyesha jinsi timu ya TNC inakidhi mahitaji haya
- Muhtasari wa sheria inayofaa ya mwenyeji kuhusu FPIC
- Mahitaji ya uwezo wa IPLC, ikiwa ni pamoja na kujuana na FPIC, uwezo wa kutuma, kupokea na kuhifadhi taarifa na uwezo wa kuandaa na kuhudhuria mikutano

☐ Mpango wa Ushauri, ulioundwa kwa kushirikiana na IPLC, unaoshughulikia mambo yafuatayo kiasi:

- Sehemu muhimu za majadiliano
- Kuandika ratiba
- Kuandika bajeti
- Hatua kuu
- Kuandika Hati
  - Fafanua wazi atakayeandika mambo fulani
  - Hakikisha kwamba mikutano yote, simu na hatua nyingine zilizo katika mchakato zinajulikana na zimeelezewa
  - Eleza kuhusu jinsi ambavyo dakika za mkutano zitahifadhiwa na kupeanwa
  - Angalia utangamano wa mipango hii ya hati na mahitaji ya hivi karibuni ya utunzaji wa rekodi ya TNC kwa shughuli ya FPIC
  - Hakikisha kwamba hati zinatunzwa katika muundo ambao wafanyakazi wanaweza kupata kwa urahisi na unashirikiwa kwa urahisi na kuhifadhiwa na washirika wa IPLC
- Taarifa inayotokana na Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu, ikiwa ni pamoja na athari halisi na zinazoweza kutokea, mapendekezo ya kupunguza athari, mpango wa kufuatilia majibu na matokeo na kuwasiliana na wadau na wamiliki wa haki kuhusu jinsi athari zinavyoshughulikiwa
- Rekodi za jinsi ambavyo mpango uliundwa na kushirikiwa na IPLCs

☐ Vifaa vinavyoandika kuhusu mikutano, matukio, na shughuli zinazofanana (kumbukumbu, orodha ya waliohudhuria, nakala za vifaa vikuu vilivyosambazwa)

☐ Uwasilishaji wa mwisho au muhtasari unaoelezea nia na uhakikisho wa TNC kwa njia thabiti ambapo uamuzi wa IPLC wa idhini unaweza kuzingatiwa.

☐ Makubaliano ya Idhini (ikiwa idhini imetolewa) yanayonyesha muundo uliokubaliwa na unaojumuisha mashaka na mapendekezo ya IPLC, ambao walishiriki katika mikutano ya Makubaliano ya Idhini, na mpango wa wakati na jinsi ya kupitia tena Makubaliano ya Idhini

☐ Maelezo ya mikutano yanayopitia tena Makubaliano ya Idhini

## Maelezo

[1] Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa. (2016). Idhini ya Kujitolea na Inayotolewa Mapema Baada ya kuelewa: Haki ya wenyeji na desturi nzuri ya jamii za eneo hilo. Manual for Project Practitioners. Unapatikana: http://www.fao.org/3/a-i6190e.pdf

[2] Kwa TNC, "wenyeji na jamii za eneo hilo" inamaanisha watu na jamii ambao wana uhusiano mkubwa na mandhari yao ya asili, ambayo wanategemea kwa ajili ya ustawi wa kitamaduni, kiroho, kiuchumi na kimwili. Wakazi wa asili na wahamiaji ambao wana uhusiano wa karibu na mandhari vile vile huchukuliwa kama IPLCs. TNC inatambua haki za watu wote wenyeji kama ilivyoorodheswa katika sheria za kimataifa. Katika Mwongozo huu, "IPLCs" hutumiwa kurejelea watu wote ambao ni wenyeji na jamii za eneo hilo.

[3] FSC, supra, at 15.

[4] Jerome Lewis, supra, at 177.

[5] Conservation International, supra, at 22-23.

[6] FAO, supra, at 25.




# Muungano wa Mashauriano

## 2A. Utafiti wa Wenland

**FrostLock sasa imeweka umoja wa asasi za kiraia, mashirika ya serikali ya Wenland na Halmashauri za Wen zishiriki katika mashauriano kadhaa kuhusu uwezekano wa kupeleka teknolojia yake katika udongo jalidi wa Wenland. FrostLock itatumia ufadhili wake wa kuanzisha wa mwekezaji kulipia mashauriano, ambayo pia yatashughulikia masuala yanayohusiana na usimamizi wa Eneo la Usimamizi wa Uhifadhi ambalo FrostLock inafadhili.**

Serikali ya Wenland inapenda sana ajira na uwekezaji unaohusiana na kupelekwa kwa teknolojia hiyo. FrostLock imejitolea kwa ufuatiliaji mkali wa mazingira yake ya majaribio lakini inakubali kwamba teknolojia hiyo inatumia mbinu za kutoboa shimo kwenye ardhi kwa keekee kwa kutumia sindano ya mchanganyiko wa kemikali ya wamiliki kwa ajili ya kuvunja na kuimarisha.

**Kwa mfano**

*Mawazo na Mwongozo*

**1**

**Mchakato wa mashauriano unapoanza, mgawanyiko unaibuka kati ya Halmashauri za Wen, ambao wanataka mchakato kamili bila kujali kuhusu muda, na FrostLock na mashirika ya serikali, ambayo yanazingatia sana ufanisi na maendeleo ya kiuchumi. *Je TNC inapaswa "kuunga mkono" Halmashauri za Wen na kushawishi kwamba kuwe na mchakato kamili zaidi?***

*Kazi ya muungano ni bora ikiwa inatafuta mahali ambapo pana mwingiliano na kujenga makubaliano ya pande zote. TNC inapaswa kujitahidi kushirikiana zaidi katika huduma ya misheni yake Lakini pia kutakuwa na wakati ambapo "kuunga mkono upande mmoja" kunafaa na Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zinaonyesha kujitolea sana kwa taasisi ya TNC kwa michakato inayofaa iliyoundwa kulinda wenyeji katika kujiamulia wenyewe. TNC inapaswa pia kujua kuhusu usawa wa nguvu za kijamii na kwamba mirathi ya ukoloni inaweza kuwa imeacha IPLCs bila nguvu inayohitaji kwa hivyo kupunguza ukali kunahitajika. Tukio hilo linaonyesha aina ya hali ambapo TNC inapaswa kufikiria kutumia uwezo wake kusaidia Halmashauri katika kutafuta mchakato zaidi.*

| **Kwa mfano** | *Mawazo na Mwongozo* |
|---|---|
| **2**<br>**Mashauriano yakiendelea, mashaka ya TNC unakua. Kwa mfano, FrostLock inasisitiza kwamba masuala ya mazingira ni "ya kiufundi sana" kwa mashauriano ya umma, ambayo yanapaswa kuzingatia tu athari za kijamii. Licha ya mashaka ya awali, Halmashauri za Wen zinafanya majadiliano ya ndani na hatimaye zinaamua kwamba wanataka mchakato uendelee kwa njia ambayo FrostLock inapendekeza. *Je TNC inapaswa kuendelea kushawishi mchakato thabiti zaidi?*** | *Kama ilivyobainika, TNC imejitolea sana katika mchakato, lakini kujitolea huko kumeundwa kufuata kanuni ya Kujiamulia Mwenyewe ya Wenyeji. Ambapo Halmashauri zimefanya uamuzi kama huu, hata uamuzi ambao TNC haikubaliani nao, ahadi za TNC kwa Ushauri wa Maana na Kufanya Uamuzi baada ya Kuelewa zinaweza kuheshimiwa.* |
| **3**<br>**Mchakato unapoendelea, timu ya TNC inaamini kwamba mradi huo ni wazo baya sana kwa sababu ya: (a) hatari kubwa za kimazingira ambazo hazijashughulikiwa kikamilifu katika mashauriano; na (b) hatari za kijamii kwa watu wa Wen, kama vile ushawishi kuhusu utamaduni na mtindo wa maisha wa miji midogo ya Wen kutokana na kuwasili kwa wafanyakazi wengi wa mradi ambao si watu wa Wen. *Je, TNC inaweza kupinga mradi huo kwa mdomo hata kama Halmashauri za Wen zinaendelea kuunga mkono?*** | *Maoni na misimamo wa TNC si ya msingi kulingana na mtazamo wa IPLC, ambao umejikita katika haki ya IPLC ya kujiamulia mwenyewe hata kama maoni ya IPLC yanapingana na maoni ya watu wa nje wenye nia nzuri. TNC bado inaweza kutoa maoni na nafasi zake kwa njia inayosaidia IPLC, hata hivyo, kiwango ambacho TNC inaweza kutetea maoni yake bila kukiuka kanuni za Uhuru wa Kuchagua na Kujiamulia mwenyewe kutategemea hali ya suala hilo kwa kiwango fulani. Katika tukio hili, inaweza kuonekana kwamba TNC ina kesi yenye nguvu zaidi ya kupinga kutokana na kwamba maoni yake yanazingatia uzoefu wake wa masuala ya mazingira badala ya maoni ya kutawala watu kama watoto ya mambo bora kwa utamaduni na mtindo wa maisha wa Wen. Kwa hali yoyote, TNC inapaswa kuwa mwangalifu ili ihakikishe kwamba maoni yoyote ya nguvu yake au msimamo wake hauna mamlaka zaidi kwa maoni yake kuliko inavyofaa.* |

| **Kwa mfano** | *Mawazo na Mwongozo* |
| --- | --- |
| **4**<br>**Vinginevyo, timu ya TNC inaamini kwamba teknolojia ya FrostLock ndiyo njia pekee ya kushughulikia tishio hili kubwa la hali ya hewa na kulinda afya ya sayari. Hatahivyo, Halmashauri za Wen, zinazingatia kutohakikishiwa ajira kwa jamii zao. *Je TNC inaweza kuunga mkono mradi kwa mdomo hata kama watu wa Wen hawajashawishika?*** | *TNC ina haki ya maoni yake lakini inapaswa kuwajibika kwa sheria na matarajio ya taasisi na tamaduni za IPLC ambayo inafanya kazi nayo, na daima inapaswa kutenda ikizingatia Wenyeji Kujiamulia Wenyewe, Mahusiano ya Ushirikiano na Nia Njema. Hii inaweza kumaanisha kujizuia ingawa TNC imetekwa na hisia kali. Lakini ambapo uhusiano wa ushirikiano una msingi zuri na mshirika wa IPLC hawezi kushurutishwa, TNC inaweza kuwa na "nafasi" zaidi ya kutetea kwa nguvu bila kukiuka kanuni nyingine.* |
| **5**<br>**Wakati mchakato wa mashauriano unafikia mada ya Eneo la Usimamizi wa Uhifadhi, Halmashauri zinasema kwamba zinaamini TNC, jamii zinapoteza hamu ya mchakato huo, na TNC inapaswa tu "kutunza" maelezo yanayohusu mpango wa uhifadhi, ambao TNC ina utaalumu.y. Bila shaka, jamii zitapiga kura mwishoni na watakuwa na sauti kwa njia hiyo, bila kujali kuhusu mapendekezo ya TNC. *Je TNC inaweza "kuchukua uongozi" wa sehemu hii ya mchakato wa mashauriano?*** | *Labda haiwezi. Huku TNC ikiweza kuchukua jukumu kubwa kutokana na utaalamu wake na ombi la Halmashauri, FPIC lazima iwe msingi wa uamuzi kamili wa IPLC na uzoefu wa mashauriano. Mchakato wa "njia ya mkato" unaweza kukosa uhalali katika siku zijazo, haswa kuhusu jambo lenye athari kama eneo kubwa la Usimamizi wa Uhifadhi kwenye eneo la wenyeji.* |




# Idhini na Haki ya Kukataa kutoa Idhini

## 2B. Utafiti wa Wenland

**Wasiwasi upo kuhusu FrostLock na teknolojia yake, lakini Baraza la Wen linasema watatoa idhini.**

Wanasema kwamba wanatambua kwamba uzito wa hali hiyo—kwa udongo jalidi na kwa sayari—unahitaji hatua hata kama hakuna uhakika kuhusu matokeo. "Lazima tuchukue hatua. Tutashughulikia shida kadri zitakavyokuja," anasema kiongozi mmoja wa Wen.

| **Kwa mfano** | *Mawazo na Mwongozo* |
|---|---|
| **1**<br>**Viongozi wa Halmashauri za Wen wanaonyesha kwamba wanaweza kutoa idhini ya Wen kwa mradi bila kura za umaarufu.** ***Je TNC inapaswa kushawishi mchakato tofauti?*** | *Kwa kuwa hakuna shida iliyo wazi kabisa, TNC inapaswa kukubali kushindwa na Halmashauri za Wen kuhusu upeo wa mamlaka yao ya kuongea kwa niaba ya watu wa Wen. Hata hivyo, TNC inaweza kutaka kukagua kiwango cha ushiriki wa jamii katika mchakato wa mashauriano. Kuidhinisha mpango huu ni uamuzi mkubwa, na watu wa Wen wana muundo tata na mgawanyiko wa kijamii. Je Kanuni za Uhusishaji na Kufanya Uamuzi baada ya kuelewa zimezingatiwa katika Kambi zote tatu? Je Sera ya Kulinda Maslahi ya Haki ya Kukataa kutoa Idhini imelindwa? Ikiwa bado kuna mashaka, ombi la mchakato zaidi au dalili pana za usaidizi wa jamii inaweza kusaidia.* |

| Kwa mfano | *Mawazo na Mwongozo* |
| --- | --- |
| **2**<br>**Sawa na hapo juu, lakini uongozi wa Baraza unakubali wazi kwamba hawataki kuwasilisha hii moja kwa moja kwa watu wa Wen ambao wataogopa mradi huo. "Huu ni wakati wa uongozi," wanasema*. Je TNC sasa inapaswa kushawishi mchakato tofauti?*** | *Hali hii inazidisha shida, lakini uchambuzi huo huo unatumika. Watu wa Wen kujiamulia wenyewe kama ilivyoonyeshwa kupitia taasisi zao zilizoanzishwa lazima kuheshimiwe. Uamuzi kuhusu mambo yanayopaswa kupata kura za umaarufu dhidi ya uamuzi wa wawakilishi ni uamuzi wa kikatiba uliofanywa kwa njia tofauti na jamii zote. Kulazimisha maoni ya mgeni kuhusu jambo linalohitajika kunaweza kuwa kinyume na kujiamulia mwenyewe. Hivyo basi, TNC inaweza kutumia uwezo wowote wa kushawishi tulionao katika mchakato kupigania mashauriano zaidi na kufanya uamuzi baada ya kuelewa, huku bado ikidumisha heshima ya kujiamulia mwenyewe.* |
| **3**<br>**Baraza la Wen linasema kwamba hakuna hati rasmi au kumbukumbu inayohitajika ili kutoa idhini. Hata hivyo, wafadhili wa kisheria na wa TNC, wanasisitiza kuwa na hati za aina fulani kabla ya kuamua kuendelea na mpango huo. *Je TNC inapaswa kusisitiza kuwe na aina fulani ya hati ya idhini?*** | *Lazima TNC iendelee kuheshimu kujiamulia mwenyewe. Lakini tunaweza pia kuweka masharti katika uwezo wetu wa kushiriki zaidi, kujitolea, au kutoa ahadi za mtu asiyehusika moja kwa moja, kama ufadhili, kwa mahitaji yetu ya ndani, ikiwa ni pamoja na kuandika hati. Hata hivyo, ikiwa kupunguza ushiriki wa TNC kunaweza kutishia mradi wa jumla, msisitizo huu unaweza kuwa na athari ya kulazimisha, ambayo lazima izingatiwe. Ushawishi wa TNC lazima utekelezwe kwa kushirikiana na watu wa Wen ili kupata aina ya ukumbusho ambao unaridhisha pande zote (angalia Moduli ya Kuandika hati).* |
| **4**<br>**FrostLock pia inataka kukumbuka idhini hiyo na inapeana Halmashauri makubaliano ya idhini yaliyoandikwa na lwakili wake. FrostLock inasisitiza kwamba hati imepitia uhakiki wa kina katika idara ya sheria ya FrostLock na kwamba haiwezi kubadilishwa—na kwamba kampuni haiwezi kusonga mbele hadi itakapotiwa saini. *Je, TNC inapaswa kuunga mkono kusisitiza kwa FrostLock kwamba Halmashauri za Wen zisaini hati hii?*** | *Kuonyesha mashaka ulioelezewa katika #3, msimamo wa FrostLock unaweza kuwa wa kulazimisha, isiyo ya kushirikiana na isiyoheshimu uamuzi wa kujitawala. TNC inapaswa kushirikiana na FrostLock ili kupata mbinu ya kushirikiana zaidi.* |

| **Kwa mfano** | *Mawazo na Mwongozo* |
| --- | --- |
| **5**<br>**Vinginevyo hapo juu, ushauri unapohitimishwa, Halmashauri za Wen hazijatoa hakikisho lolote kuhusu kuunga mkono mradi lakini wanataka kujadiliana na jamii zao. Hata hivyo, serikali ya Albania inatangaza usaidizi wake, na FrostLock inatoa wito wa kukomesha mashauriano hayo, ikisema kwamba imetimiza mahitaji ya kisheria na kwamba hakuna mchakato zaidi unaohitajika kwa sababu watu wa Wen hawana haki ya turufu chini ya sheria ya Albania. FrostLock pia inasema kwamba watu wa Wen hawajakataa kutoa idhini rasmi, hawajafanya tu uamuzi. *Je TNC inaweza kuendelea kushiriki katika mradi huo?*** | *Lazima TNC itumie uwezo wetu wa kushawishi kupinga kusonga mbele bila FPIC kamili kutoka kwa watu wa Wen au kujiondoa ikiwa FPIC haijafikiwa. Hata kama TNC haiwezi kubadilisha ukweli wa hali hiyo, lazima tuzingatie kanuni zinazoongoza za FPIC, ikiwa ni pamoja na kuheshimu Haki ya Kukataa kutoa Idhini. Ukweli kwamba watu wa Wen hawakukana rasmi idhini haijalishi. Haki ya Kukataa kutoa Idhini ni Sera muhimu ya Kulinda Maslahi, lakini FPIC ni dhana pana na ya kukubali zaidi ambayo hairidhiki na ukosefu wa upinzani wazi.* |
| **6**<br>**Vinginevyo hapo juu, Halmashauri za Wenna na Wennec hutoa idhini wakati Baraza la Wenebe linapinga vikali. Kwa sababu watu wa Wen wamekuwa wakifanya kazi kulingana na makubaliano, hakuna mila au sheria zinazosema kwamba wengi wanashinda.** | *Hali hii inatafsiriwa vyema kama kufunua mapungufu na kutofaulu kwa Uamuzi wa Kufanya Uamuzi baada ya Kuelewa na Sera za Kulinda Maslahi ya Ushauri vya Maana. Kwa nini Halmashauri hazikubaliani? TNC inapaswa kushawishiwa na modeli ya makubaliano ya Wen na kuendelea na taratibu za mashauriano na utatuzi wa mgogoro hadi makubaliano yatakapofikiwa.* |

## Mti wa Uamuzi wa FPIC

# Je Mchakato wa FPIC unahitajika?




* Zingatia matumizi ya dhidi ya mkondo wa maji na katika mkondo wa maji, matumizi ya msimu, na matumizi ya jadi na ya kihistoria ya ardhi, maji na maliasili ambazo shughuli zinaweza kuathiri.

** TNC inapaswa kushirikiana na IPLCs, serikali, asasi za kiraia, wataalamu wa masomo, na wamiliki wengine wa haki na wadau kuamua kwamba shughuli zinazopendekezwa hazitaathiri IPLCs. TNC haipaswi kufanya uamuzi huu peke yake.

*** Mbali na kutathmini uwezo na kupeana habari kuhusu FPIC, TNC inapaswa kuthibitisha kwamba mwakilishi wa IPLC ana mamlaka ya kuwawakilisha IPLC kwa ujumla. Mwongozo wa Haki za Binadamu inapaswa pia kudhibitisha kuwa mwaliko ni wa kweli na haujatokana na kulazimishwa kwa kweli au kunakofirwa au kushurutishwa na TNC au wahusika wengine ili kukwepa mchakato kamili wa FPIC.

**** Usiendelee na majadiliano ikiwa makubaliano kuhusu Mpango wa Ushauri hayawezi kufikiwa.

### Utafiti wa Wenland:

# Bajeti ya Kubuni

Kabla ya Mazungumzo ya Awali, FrostLock inaomba TNC makadirio ya ukweli ya mchakato wa FPIC na TNC inajibu kwa mambo yafuatayo:

- Upeo na bajeti ya mchakato wa FPIC itaunganishwa sana na ukweli wa hali hiyo. Mwanzoni, TNC inaweza tu kutoa makadirio ya kiwango cha juu kwa tahadhari kwamba hali tofauti zinaweza kusababisha mahitaji na gharama tofauti sana.
- Hata hivyo TNC inatambua kwamba bajeti sahihi ni muhimu kwa ajili ya umakini na muundo na kuweka matarajio ya mchakato huo. TNC inakubali kushirikiana na Halmashauri za Wen ili kuandaa bajeti ya kina zaidi baadaye.
- TNC inatambua kwamba FPIC inapaswa kuwa na msingi wa haki na ufanisi na inahimiza wahusika wote watumie wakati na rasilimali kwa uangalifu. Wakati huo huo, maamuzi yaliyofikiwa katika mchakato wa FPIC yanaweza kuathiri haki za msingi za kujiamulia mwenyewe za watu wa Wen na kuhusisha masuala magumu ambayo yanahitaji kueleweka kikamilifu na wahusika wote—kwa hivyo mchakato huo unahitaji kuwa kamili na utahitaji juhudi.
- Kanuni inayoongoza ni kwamba kiwango cha jukumu la kushauriana ni ***sawia*** na hali na kiwango cha: a) zinazoweza kuwa ***athari*** kwa IPLC; na b) zinazoweza kuwa ***faida*** za kushirikiwa na IPLC. Kanuni hii ya uwiano ilijadiliwa katika kesi za msingi za ushauri wa *Delgamuukw dhidi ya British Columbia* nchini Kanada na *Sarayaku dhidi ya Ecuador* katika Korti ya Haki za Binadamu ya Marekani ya Kati, kati ya vyanzo vingine vingi.

Baada ya kushauriana na watendaji wa ndani na nje, TNC inatoa uchambuzi na makadirio yafuatayo:

- Kama ilivyoelezewa katika Hypo 1b, pendekezo la FrostLock lina vifaa viwili: a) usanikishaji wa mfumo wa kutoboa shimo kwenye ardhi kwa keekee na kuimarisha kwenye maeneo ya majaribio; na b) Eneo la Usimamizi wa Uhifadhi. Kwa sababu athari na faida za vitu hivi viwili ni tofauti sana, zinapaswa kuchambuliwa kando.
- Kuhusu maeneo ya majaribio ya teknolojia:
  - Maeneo haya yanaonyesha kiwango kikubwa cha athari, ikijumuisha ujenzi mzito na vifaa, sindano ya kemikali kwenye udongo jalidi, kuongezeka kwa umakini wa kitaifa na ulimwengu, athari za kijamii na kiuchumi, na mengi zaidi. Uchambuzi wa faida kwa Wen ni ngumu, lakini kwa FrostLock kupima kwa mafanikio (ambako hakujahakikishiwa) kunaweza kusababisha mabilioni ya dola katika mikataba ya teknolojia.
  - Uchambuzi wa athari/faida utafanana na miradi yenye athari kubwa, katika tasnia ya mafuta, gesi au madini. Gharama za FPIC zinapaswa kutathminiwa dhidi ya utendaji bora katika maeneo hayo. Gharama halisi zinaweza kuwa ***kubwa sana*** kwa sababu ya hali mpya ya teknolojia na isiyo ya kawaida.
  - TNC inaripoti kuwa gharama ya FPIC kwa miradi yenye athari kubwa, ni kuanzia $ 250,000 hadi $ 5,000,000. Baada ya kuzingatia uchumi wa eneo hilo, TNC inashauri FrostLock kwamba hali nzuri itakuwa

    $ 800,000 kwa mwaka mmoja, lakini inapaswa kuwa tayari kufadhili mpaka $ 1,500,000 ikiwa masuala magumu au yasiyotarajiwa yatatokea katika mchakato huo.
  - CMA inayopendekezwa ni kubwa katika upeo wa kijiografia, lakini kiwango cha athari inayowezekana ni cha chini sana kuliko maeneo ya teknolojia. Athari zinazoweza kutokea katika haki na maslahi ya watu wa Wen ambayo yanahitaji kuzingatiwa ni pamoja na: athari za modeli ya ngome ya uhifadhi; matumizi ya rasilimali asilia; umuhimu wa kitamaduni wa Wendbok; vikwazo vya uwindaji; na jukumu la ufuatiliaji na usimamizi wa mifugo.

- TNC inaripoti kwamba gharama ya FPIC ya miradi mikubwa, yenye athari ndogo ya uhifadhi ni $50,000 hadi $500,000. TNC inashauri FrostLock kupanga bajeti ya $200,000 kwa mwaka mmoja na inashauri kwamba gharama inaweza kuongezeka kwa $80,000 ikiwa masuala magumu yatatokea ambayo yanahitaji uchambuzi wa wataalamu.

Baada ya mazungumzo ya awali na Halmashauri za Wen kuhusu upeo na muundo wa mchakato wa FPIC, TNC inasaidia Halmashauri kuwasilisha rasimu zifuatazo za bajeti za FPIC kwa maeneo ya majaribio ya teknolojia na CMA. TNC inashauri kwamba nambari zinaweza kubadilika wakati taarifa mpya au masuala yanaibuka.

**Rasimu ya Bajeti ya FPIC ya Maeneo ya Majaribio ya Teknolojia:**

| Kategoria / Kipengee | Gharama | Maelezo |
|---|---|---|
| **Mshahara** | | |
| Wafanyakazi wa TNC waliopo | - | Imelipwa na TNC |
| Meneja Mwingine wa Mradi | - | Imelipwa na TNC |
| Mratibu wa Uhamasishaji Jamii | - | Imelipwa na TNC |
| **Usafirishaji** | | |
| Usafirishaji - FrostLock | - | Usafirishaji x Watu = 16<br>Gharama ya ndani kwa FrostLock |
| Usafirishaji - TNC (ya ndani) | $14,400 | Usafirishaji x Watu = 24 |
| Usafirishaji - TNC (kimataifa) | $9,000 | Safari x Watu = 6 |
| Usafirishaji – Uongozi na Ushirikiano wa Wen | $7,000 | Usafirishaji x Watu = 28 |
| Usafirishaji – Jamii ya Wen | $10,000 | Mfuko mkuu |
| **Mikataba/Washauri** | | |
| Mratibu wa Uhusiano wa Jamii | $40,000 | Mtu 1 x $5,000/mo x miezi 8 |
| Ushirikiano wa Jamii | $54,000 | Watu 3 x $3,000/mo x miezi 6 |
| Vifaa & Mratibu wa utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu | $65,000 | Mtu 1 (utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu) |
| Maandalizi ya Rasimu ya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (ESIA) kwa mapitio ya jamii na mabadiliko | $350,000 | Inajumuisha kukusanya data ya msingi, kutambua na kuchambua athari tofauti za jumla, kutambua machaguo ya kupunguza na ufuatiliaji. |
| Mapitio ya nje/maoni ya pili: Uchunguzi wa athari za jumla (kutegemea data ya ESIA) | $35,000 | Mara nyingi huchukuliwa kuwa kweli kutokana na kiwango kikubwa cha kuzidisha na/au kujishughulisha katika uchambuzi wa jumla |
| Ripoti ya Mtaalamu: Mapitio kamili ya fasihi kuhusu kutoboa shimo kwenye ardhi kwa keekee | $45,000 | - |
| Ripoti ya Mshauri: Modeli ya mbinu za utatuzi wa mizozo na suluhisho | $28,000 | - |

**Rasimu ya Bajeti ya FPIC ya Maeneo ya Majaribio ya Teknolojia (imeendelezwa):**

| Category / Item | Gharama | Maelezo |
|---|---|---|
| **Mikataba/Washauri** | | |
| Mradi wa Kukamilisha unaoongozwa na NGO la eneo hilo: Utafiti na Hifadhidata ya ujuzi | $30,000 | - |
| Tafsiri ya hati muhimu kwa Kialbania na Wen | $50,000 | - |
| Utofauti, Usawa na Mkufunzi wa Uhusishaji | $25,000 | - |
| **Vifaa, Bidhaa na Gharama nyingine za Moja kwa moja** | | |
| Bajeti ya Mazungumzo ya awali | $4,000 | - |
| Kutoa upeo - kikao cha kufanya kazi na ufuatiliaji | $8,000 | Siku 2, idadi ya watu kwenye kikundi 30+ |
| Vikao vikuu vya kufanya kazi vya FPIC (3) | $36,000 | Siku 3, idadi ya watu kwenye kikundi 150+ Nafasi, teknolojia, vifaa, chakula |
| Kikao cha Kuzingatia jambo maalum: Usawa wa kijinsia | $9,000 | Siku 1, idadi ya watu kwenye kikundi 40+ |
| Mikutano ya kufikia jamii (6) | $66,000 | Siku 6, vikundi 30-100 Nafasi, vifaa, chakula |
| Vikao vya mwisho vya mazungumzo | $15,000 | Siku 3, idadi ya watu kwenye kikundi 25+ Nafasi ya mahali poa raha |
| Makubaliano na Kufanya Sherehe | $30,000 | - |
| **Mawasiliano** | | |
| Bajeti ya vyombo vya habari/elimu kwa umma - Wenland | $50,000 | - |
| Bajeti ya vyombo vya habari/elimu kwa umma - Wenland | $125,000 | - |
| Kulengwa kwa jamii za Wen | $25,000 | - |
| Mfululizo mfupi wa video | $12,000 | - |
| Serikali ya Albania na huduma za mahusiano ya umma | $16,000 | - |
| Uhifadhi wa hati kidijitali na mfumo wa ufikiaji wa umma na huduma | $35,000 | - |
| **Gharama zisizo za Moja kwa moja (@30%)** | $342,480 | |
| **JUMLA** | **$1,484,080** | |

**Rasimu ya Bajeti ya FPIC kwa CMA:**

| Kategoria / Kipengee | Gharama | Maelezo |
|---|---|---|
| **Mshahara** | | |
| Wafanyakazi wa TNC waliopo | - | Imelipwa na TNC |
| Meneja Mwingine wa Mradi | - | Imelipwa na TNC |
| Mratibu wa Uhamasishaji Jamii | - | Imelipwa na TNC |
| **Usafirishaji** | | |
| Usafirishaji - FrostLock | - | Usafirishaji x Watu = 8 Gharama ya ndani kwa FrostLock |
| Usafirishaji - TNC (ya ndani) | $1,800 | Safari x Watu = 6 |
| Usafirishaji - TNC (kimataifa) | $1,500 | Safari x Watu = 1 |
| Usafirishaji – Uongozi na Ushirikiano wa Wen | $3,200 | Safari x Watu = 12 |
| Usafirishaji – Jamii ya Wen | $2,000 | Mfuko mkuu |
| **Mikataba/Washauri** | | |
| Mshauri wa Tathmini ya Athari za Jamii | $75,000 | Mtu 1 wa kudumu kwa miezi 8. Hutoa utaratibu wa ugavi na usafirishaji wa watu na vitu na kuandika maandishi ya CMA-ESIA |
| Ushirikiano wa Jamii | $6,000 | Watu 3 x $1,000 ada ya mara moja |
| Ripoti ya Mtaalamu: Uchambuzi wa huduma za maliasili | $15,000 | - |
| Ripoti ya Mtaalamu: Mwelekeo wa idadi ya watu wa Wendbok, usambazaji, na hali ya uhifadhi | $15,000 | - |
| Tafsiri ya hati muhimu kwa Kialbania na Wen | $20,000 | - |
| **Vifaa, Bidhaa na Gharama nyingine za Moja kwa moja** | | |
| Gharama za ukusanyaji wa data ya mazingira na matumizi ya ardhi, mkusanyiko, na kuhifadhi | $22,000 | - |
| Vikao vya Kusikiliza | $4,000 | Siku 4, idadi ya watu kwenye kikundi 30+ |
| Kikao Kikuu cha Kufanya Kazi cha FPIC | $6,000 | Siku 1, idadi ya watu kwenye kikundi 75+ Nafasi, teknolojia, vifaa, chakula |
| Vikao vya kuhamasisha Jamii | $4,000 | Siku 4, idadi ya watu kwenye kikundi 30+ |
| **Mawasiliano** | | |
| Utangazaji wa vikao | $500 | - |
| **Gharama zisizo za Moja kwa moja (@30%)** | $46,500 | |
| **JUMLA** | **$201,500** | |

**Kiolezo:**

# Mpango wa Ushauri

Kiolezo hiki ni mahali pa kuanza kutengeneza Mpango wa Ushauri ulioelezewa katika Hatua ya Pili ya Moduli ya FPIC ya Mwongozo. Wakati Mpango wa Kujihusiha ulio katika Moduli ya Kwanza unazingatia "nani" na "vipi" kuhusu majadiliano ya mwanzo, Mpango huu wa Ushauri unazingatia "nini" kuhusu majadiliano – masuala muhimu yatakayojadiliwa, shughuli zilizopendekezwa, athari zinazoweza kutokea, gharama na faida. Kiolezo hiki pia kinajumuisha maswali kadhaa kwa TNC na IPLC ya kuzingatia wakati wa kufanya Mpango wa Ushauri. Makubaliano kuhusu yaliyomo kwenye Mpango wa Ushauri yanapaswa kuandikwa kwa njia inayozingatia utamaduni, ambayo inaweza kujumuisha saini au herufi za kwanza kwenye mpango, kubadilishana barua pepe, kuinua mikono kwenye mkutano, utaratibu au sherehe

Kabla ya kuanza Mpango wa Ushauri, pitia tena Mpango wa Kujihusisha na uzingatie sehemu ambazo zimethibitisha kwamba ni muhimu kwa TNC na IPLC hadi sasa. Fikiria kuchukua na kuzidisha maudhui na mafunzo kutoka kwenye Mpango wa Kujihusisha, pamoja na kiolezo hiki.

Maudhui yaliyoandikwa kwenye fomu hii **hayatahifadhiwa** ikiwa yatajazwa kwenye kivinjari. Jifunze mengi

Mpango:____________________

KIpindi cha wakati: ____________________

Tarehe:____________________

Imesasishwa kuanzia: ____________________

| Imeidhinishwa na: | Shirika au kikundi: |
|---|---|
| Jina:__________ | Jina:__________ |
| Jina:__________ | Jina:__________ |
| Jina: __________ | Jina: __________ |

**1 Timu ya TNC na uwezo wa IPLC,** ikiwa ni pamoja na lugha, uzoefu na mafunzo yanayohitajika kwa ajili ya mchakato wa mashauriano. Tazama Maswali ya Kuzingatia hapa chini na Hatua ya Kwanza ya Moduli ya FPIC.

a. Mafunzo ya wafanyakazi wa TNC na warsha walizohudhuria, na mafunzo mengine:

b. Mahitaji mengine ya uwezo wa TNC

c. Mahitaji ya uwezo wa IPLC:

d. Jinsi ambavyo mahitaji ya uwezo wa TNC na IPLC yatatimizwa, kwa mfano, rasilimali za ndani au nje:

**2 Mambo ya kujadiliwa.** Mambo yaliyoorodheshwa katika (a) mpaka (c) hapa chini ni mifano tu

a. **Shughuli zilizopendekezwa**

i. Jukumu la TNC: ______________________________

ii. Jukumu la IPLC: ______________________________

iii. Jukumu (Majukumu) ya watendaji wengine wanaohusika: ______________________________

b. **Zinazowewza kuwa athari za haki za binadamu za shughuli zilizopendekezwa.** Athari zinapaswa kusasishwa wakati majadiliano ya mashauriano yanaendelea. Angalia mwongozo zaidi kuhusu Tathmini ya Athari za Haki za Binadamu iliyo katika Hatua ya Pili ya Moduli ya FPIC.

i. Zinazoweza kuwa athari nzuri na athari halisi:

______________________________

ii. Zinazoweza kuwa athari mbaya na athari halisi, ikiwa ni pamoja na ukali, uwezekano na sababu za hatari:

______________________________

iii. Zinazoweza kuwa athari mbaya na athari halisi, ikiwa ni pamoja na ukali, uwezekano na sababu za hatari:

______________________________

iv. Mpango wa kufuatilia majibu na matokeo na kuwasiliana kuhusu jinsi ambavyo athari zinashughulikiwa

______________________________

c. **Kushiriki Faida.** Orodhesha faida zinazotarajiwa na jinsi zitakavyoshirikiwa na wahusika. Angalia Hatua ya Pili ya Moduli ya FPIC.

i. ______________________________

ii. ______________________________

iii. ______________________________

**3 Njia ambazo majadiliano yatatokea,** zikielezea jinsi ambavyo vitambulisho tofauti vya kijamii vitajumuishwa ipasavyo

a. Idadi ya marudio na muda:

b. Mahali:

c. Muundo:

## 4 Bajeti

a. Gharama za kulipwa na TNC:

b. Gharama za kulipwa na IPLC:

**5 Hatua kuu.** Wakati wa mchakato wa mashauriano, wahusika huchunguza kwa makusudi, ili wahakikishe kwamba majadiliano yanaendelea kama ilivyotarajiwa hapo awali.

a. Tarehe iliyopangwa na halisi, washiriki (jina, cheo, shirika), mahali, mada itakayojadiliwa:

b. Tarehe iliyopangwa na halisi, washiriki (jina, cheo, shirika), mahali, mada itakayojadiliwa:

c. Tarehe iliyopangwa na halisi, washiriki (jina, cheo, shirika), mahali, mada itakayojadiliwa:

d. Tarehe iliyopangwa na halisi, washiriki (jina, cheo, shirika), mahali, mada itakayojadiliwa:

**6 Uwasilishaji wa Mwisho na Kuomba Idhini.** TNC inatoa matokeo ya mchakato wa mashauriano kwa njia inayozingatia uamuzi wa idhini ya IPLC.

a. Tarehe iliyopangwa na halisi ya uwasilishaji wa mwisho, washiriki (jina, cheo, shirika), mahali:

[Ambatisha hati za uwasilishaji, waliohudhuria na kumbukumbu za mkutano]

b. IPLC ikitoa idhini yake, taja:

i. Jinsi ambavyo idhini itatolewa:

ii. Nani alishiriki kwenye mikutano:

iii. Jinsi na wakati idhini itazingatiwa tena:

[Ambatisha nyaraka za uwasilishaji, waliohudhuria na kumbukumbu za mkutano]

## 7 Kuandika hati

a. Vipengele vya mchakato wa mashauriano ambavyo TNC itaandika:

b. Vipengele vya mchakato wa mashauriano ambavyo IPLC itaandika:

c. Njia za kuandika hati na kupeana:

d. Angalia mipango hii ya kuandika hati ili uone ikiwa inalingana na mahitaji ya hivi karibuni ya utunzaji wa rekodi ya TNC kwa shughuli ya FPIC:

e. Rekodi kuhusu jinsi ambavyo mpango uliundwa kwa pamoja, ukapeanwa na kuidhinishwa na IPLC:

### Maswali ya Kuzingatia katika Mpango wa Ushauri

- Je TNC na IPLC wamechunguza na wana mpango wa kushughulikia uwezo wao wa kushiriki vyema katika mchakato thabiti wa mashauriano?
    - Uwezo wa TNC, ikiwa ni pamoja na uwezo unaohitajika; angalia Hatua ya Kwanza ya Moduli ya FPIC kwa taarifa zaidi
    - Uwezo wa IPLC, ikiwa ni pamoja na kujuana na FPIC, uwezo wa kutuma, kupokea na kuhifadhi taarifa na uwezo wa kufanya na kuhudhuria mikutano.
- Je TNC na IPLC kwa pamoja wamechunguza athari za haki za binadamu au palipo na mashaka kuhusu shughuli zilizopendekezwa au wana mpango wa kufanya hivyo? Angalia Hatua ya Pili ya Moduli ya FPIC kwa mwongozo zaidi.
- Je hati zitahifadhiwa katika muundo ambao wafanyakazi wanaweza kupata kwa urahisi na inayoweza kupeanwa kwa urahisi na washirika wa IPLC?
- Je kuwasiliana na mashirika mengine ambayo yameshirikiana na IPLC kwa ajili ya kujifunza mengi kuhusu mchakato rasmi wa uamuzi wa IPLC na isiyo rasmi kunaweza kusaidia?
- Je umewauliza viongozi wa eneo hilo ikiwa wamewahi kushauriana na NGO nyingine hapo awali na, ikiwa wamewahi, je mambo mazuri na mabaya ya shughuli hizo za hapo awali ni gani?
- Je umewauliza IPLC ikiwa wana utaratibu au michakato ya ushauri ambayo wanapendelea kufuata?
- Je umechukua hatua gani kuhakikisha kwamba wawakilishi unaozungumza nao wanaaminiwa na jamii ambayo wanataka kuwakilisha?

PDF hii imetolewa hasa kwa ajili ya kuchapishwa au kutumiwa nje ya mtandao. Fomu hii haiwezi kujazwa kidigitali isipokuwa kama imepakuliwa na kufunguliwa katika programu ya PDF kama vile Adobe PDF Reader au Kihakiki (Mac OS). Kwa bahati mbaya, maandishi yaliyoandikwa kwenye fomu hii **hayatahifadhiwa** ukitumia kivinjari kama vile Chrome, Safari au Internet Explorer.



## Moduli ya 3:

# Utatuzi wa Mgogoro

Katika moduli hii:


Jifunze kuhusu utatuzi wa mgogoro, desturi na mikakati

Shirikiana katika kubuni mpango wa utatuzi wa mizozo unaoshughulikia utamaduni — kabla ya kuzuka kwa mzozo

Tambua watatuzi wa kuaminika na njia zingine za kutatua mizozo

Shughulikia malalamishi na ukamilishe kutatua mgogoro

**Tafiti za Wenland:**

3A. Utatuzi wa Mgogoro


## Utangulizi

Moduli hii inatoa mwongozo unaoweza kutumiwa na IPLC na wafanyakazi wa TNC katika hali mbili:

- kuweka matarajio na mikakati ya utatuzi wa mgogoro mradi unapoanza
- kudumisha mikakati hii ili kuwa mahusiano ya IPLC

Moduli hii haihusu tu udhibiti wa hatari au kujiandaa kwa ajili ya tukio baya zaidi Inaashiria uzingatiaji wa TNC wa sheria na viwango vya kimataifa kuhusiana na haki za wenyeji, ambapo haki ya kutoa na kushughulikia malalamishi imebainishwa wazi.

Taratibu za kuaminika za utatuzi wa mgogoro ni muhimu kwa sababu zinaweza kushughulikia masuala au matatizo ambayo huenda yakawa kizingiti kwa ufanisi wa mpango wowote. Endapo kuna mashaka, huenda usiwe na imani na unaweza kosa usaidizi. Vilevile, utatuzi wa mgogoro, sawa na Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema, na Baada ya kuelewa, ni mkakati wa kukuza uhusiano pamoja na kuwa

mkakati wa kudhibiti hatari.

Baadhi ya mgororo unaozuka kati ya wahusika wa mipango mbalimbali hauwezi kuepukika. Lakini migororo inapotatuliwa kwa uwazi, haraka na kwa heshima, ni fursa kwa wahusika kufahamiana, kuaminiana na kuendeleza ushirikiano baina yao. Migororo inatoa fursa kwa TNC kuonyesha uzingatiaji wake wa Maadili yetu, Kanuni za Maadili, na Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zilizoelezwa katika mwongozo huu.

Kabla ya mgororo kuzuka, IPLC na wafanyakazi wa TNC wanapaswa kujadili jinsi mizozo itakavyoshughulikiwa na kunakili maafikiano yao katika Mpango wa Utatuzi wa Mgororo. Mgogoro tofauti hutatuliwa kwa njia mbalimbali; Mwongozo huu unapendekeza njia tatu:

**Njia za Utatuzi wa Mgororo**

**Mazungumzo:**
Ya heshima, ya kusikilizana, yanayofanywa pindi mgororo unapozuka, yanayohusisha maoni ya kila mtu;

**Upatanisho:**

Mchakato maalum wa mazungumzo, unaotegemea watu au taasisi za kuaminika; na

**Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni:**
Utaratibu wa malalamishi unaosimamiwa na Ofisi ya Maadili na Utekelezaji ya TNC kwa madai ya ukiukaji wa Kanuni za Maadili au Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi.

Mara nyingi, migogoro inaweza kutatuliwa kupitia Mazungumzo au Upatanisho. Mchakato wa Utekelezaji Kanuni na Maadili unapatikana kwa IPLC kwa sababu mbili: (1) kuthibitisha kuwa wafanyakazi wa TNC wanawajibikia matendo yao; (2) kutoa njia mbadala na ya kina, ya kuzungumza na TNC na kupata watatuzi wa kuchunguza na kutatua migogoro ambao si sehemu ya timu ya mradi husika.

Wakati mwingine, njia tatu za utatuzi zilizobainishwa hufuata hatua baada ya nyingine na hutekelezwa kwa mfululizo. Unafanya Mazungumzo kisha Upatanishi ili kutatua mgogoro. Lakini unaweza kuruka hatua fulani; IPLC anaweza kwenda moja kwa moja kwa Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni iwapo inahitajika. Njia hizi tatu zinaweza kutumika wakati wowote.

Mazungumzo na Upatanisho unapaswa kutumika ili kufikia viwango na matarajio ya IPLC, sharti mbinu na desturi husika zitumike, na Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi kwenye Mwongozo zinapaswa kuzingatiwa. Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro unapaswa kuendelea kufanyiwa marekebisho mara kwa mara ili iendane na matarajio, hali halisi na uzoefu.

Mwongozo umetolewa hapa chini kuhusu utekelezaji wa mchakato wa utatuzi wa mgogoro kwa mujibu wa Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi. Wafanyakazi wa TNC wanaweza pia kuangalia utata uliopo kwenye utafiti wa kubuni wa Wenland ulio katika moduli hii.

## Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi

Utangulizi unajumuisha ufafanuzi kuhusu Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zinazotumika katika ushirikiano wa usawa. Nne ni muhimu sana katika utatuzi wa mizozo:

**Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zinazotumika katika Utatuzi wa Mgogoro**

**Nia Njema:**
Huenda kuwa mwenye nia nzuri ndiyo kanuni muhimu zaidi katika kutatua migogoro na IPLCs. Kuwa mwaminifu, mwenye heshima na mnyenyekevu na kuonyesha Uadilifu Kamili ni muhimu.

**Kujiamulia Mwenyewe:**
Mchakato shirikishi wa utatuzi wa mgogoro hukuza kuaminiana, huhimiza mazungumzo na unaonyesha jitihada za TNC katika kuwasaidia Wenyeji Kujiamulia Wenyewe na kuwa viongozi katika ya uhifadhi.

**Uwajibikaji:**
Njia za utatuzi wa mgogoro zinahusu uwajibikaji. Uwajibikaji sio kitu cha kuepuka au kuogopa; unapaswa kuchukuliwa kuwa fursa ya kujifunza na kujiimarisha. Huenda TNC isifaulu katika jambo inapolitekeleza kwa mara ya kwanza. Kujitahidi kuwa wenye kuwajibika kunaweza kugeuza makosa na kutokuelewana kuwa kiini cha ushirikiano thabiti zaidi.

**Usawa & Uhusishaji**
Taratibu za utatuzi wa mgogoro kote ulimwenguni zimegubikwa na upendeleo na ubaguzi. Desturi ya TNC ya utatuzi wa mgogoro sharti ionyeshe kwamba inaelewa athari na matukio ya zamani. Ni kwa kutambua dhuluma hizi tu ndipo tunaweza kutoa huduma na kutatua mizozo kwa njia jumuishi na ya usawa zaidi.

# Mwongozo

Mchakato mzuri wa utatuzi wa mgogoro huendeleza mazungumzo, unahakikisha uwazi, na hukuza uhusiano wa usawa kati ya washirika. Mchakato hauhitaji kuwa kitu cha kupendekezewa au jambo gumu la kutimiza matakwa. Taratibu za utatuzi wa migogoro zinaashiria kwamba utendakazi wa TNC unazingatia Maadili yetu, Kanuni za Maadili, na sheria na viwango vya kimataifa. Mchakato wa utatuzi wa mgogoro unaokubaliwa na wahusika wote ni mojawapo ya njia muhimu zaidi ambazo TNC inaweza kudumisha na kuhimiza haki za binadamu za wenyeji na jamii za eneo hilo.

## Utatuzi wa Mgogoro kama Haki ya Binadamu

Kuwa na utaratibu wa kutegemeka wa kutatua migogoro sio tu mkakati wa kudhibiti hatari au Mpango Mbadala mambo yakikwenda mrama. Ni haki ya binadamu.

Kwa muda, IPLC wamekumbwa na unyanyasaji, ukandamizaji wa kimfumo na kunyimwa haki. Mara nyingi madhara huchangiwa na taasisi kutotenda haki, kutowajibika, au kutosikiliza mashaka ya wanajamii. Sheria za kisasa zinasisitiza haki ya kuwasilisha malalamishi, suluhisho na kanuni za uwajibikaji kwa kiwango cha kufanywa kuwa haki muhimu katika sheria za kimataifa.

**Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji, Kifungu cha 40**

*Wenyeji wana haki ya kuwasilisha na kushughulikiwa malalamishi yao kwa njia ya usawa na haki kwa utatuzi wa migogoro na mizozo kati yao na Serikali au wahusika wengine, pamoja na kupata suluhu kuhusiana na ukiukaji wote wa haki zao za kibinafsi na kijumla. Uamuzi kama huo utazingatia utamaduni, itikadi, desturi na mifumo ya kisheria ya wenyeji wanaohusika na haki za binadamu za kimataifa.*

Haki ya kisheria inapatikana pia kwenye Mwongozo wa TNC wa Conservation by Design 2.0. Jitihada za utatuzi wa mgogoro zinatoka na nguzo zetu nne muhimu katika CbD 2.0—People in Conservation—inayosema, "Katika utendakazi wetu wote, sharti tuhakikishe kuwa watu wasiojiweza, wenye hali mbaya, na watu na jamii zilizotengwa (kwa mfano, jamii zenye mapato ya chini, wenyeji, jamii zinazotegemea mazingira yao, makabila yenye idadi ya chini, wanawake, watoto, wakongwe) hawajaathirika na tunajumuisha sera za kulinda maslahi ya jamii katika upangaji na utekelezaji wa miradi."

Maswali mawili kuhusu sera za kulinda maslahi ya jamii ni muhimu:

- Je, mradi unazingatia sheria za eneo hilo na za taifa, mikataba na makubaliano ya kimataifa, na sheria nyingine husika?
- Je, kuna mfumo wa uwajibikaji ambao ni wazi na amabao wadau wakuu wanawweza kupata ili kuwawezesha kusema mashaka na kuwasilisha malalamishi?[1]

CbD 2.0 pia inapendekeza kuwa timu zinazofanya kazi na wenyeji zitoe njia za usuluhishaji kupitia njia za kushughulikia malalamishi zinazoweza kupatikana, kubashiriwa, zenye uwazi, zinazofaa, zinazozingatia haki, mwafaka, na madhubuti.[2]

Ahadi sawa za uwajibikaji kupitia malalamishi na utatuzi wa mgogoro zinapatikana katika mifumo na taasisi kuu za kimataifa, kama vile Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Shirika la Kanuni za Biashara na Haki za Binadamu la Umoja wa Mtaifa, na mashirika sawa.[3]

## Utatuzi wa Mgogoro kama Mkakati Halisi

Taratibu za utatuzi wa mgogoro hazipaswi kuwa jambo gumu la kutimiza matakwa. Zikitekelezwa ipasavyo, taratibu hizo zinaweza kuruhusu TNC na IPLC kuokoa muda na kuangazia zaidi mpango wenyewe. Katika hali nzuri, watu wote wanaibuka kutoka kwenye mzozo wakiaminiana zaidi na wakiwa wenye kujitolea na kuhisi kuwa matatizo yameshughulikiwa haraka na kwa usawa.

BIla shaka, migogoro yote haitatuliwi hivi. Lakini Mpango Mwafaka wa Utatuzi wa Mgogoro unatosha kushughulikia hali nyingi tofauti. Ufafanuzi ulitolewa hapa chini unapendekeza njia bora, shirikishi (mazungumzo), pamoja na njia rasmi zaidi (upatanisho). Katika hali ambapo kuna kutoaminiana mwanzoni, kuwepo kwa taratibu maalum kunaweza kusaidia (Mchakato wa Utekelezaji wa Kanuni na Maadili ya TNC).

## Hatua ya Kwanza: Buni Mgogoro Mpango wa Utatuzi

Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro ni sehemu muhimu katika jinsi TNC inavyoheshimu haki za IPLC, inavyodhihirisha uwajibikaji na kudumisha uhusiano wa usawa. Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro ni muhimu sana katika kila hatua na inapaswa kujumuishwa katika utangulizi uliopendekezwa katika Moduli ya Mafunzo na Mazungumzo ya Mwanzo. Mazungumzo na makubaliano kuhusu mpango unapaswa kuwa sehemu ya mchakato wowote uliofafanuliwa kwenye Moduli ya FPIC.

Wafanyakazi wa TNC wanaohusika kwenye mipango iliyopo wanapaswa kutathmini utatuzi wa mgogoro wa siku za nyuma. Kisha wanapaswa kutafuta fursa za kuzungumzia suala hilo mradi ukiendelea. Wafanyakazi wa TNC wanapaswa kufafanua kuwa hii haimaanishi kuwa wanatarajia migogoro kuzuka. Badala yake, wanaijadili kama sehemu ya kuelewa zaidi desturi bora za utendakazi.ora za utendakazi.

Ili kubuni mpango, wafanyakazi wa TNC wanaweza kutumia matukio yao wenyewe, matukio ya timu nyingine za TNC, na mwongozo na rasilimali katika moduli hii. Wafanyakazi wanapaswa kupitia upya Tathmini ya Athari kwa Haki za Binadamu na machakato wa FPIC. Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro unapaswa kubaini njia wazi ya kushughulikia mashaka yoyote yaliyoko katika tathmini na michakato hii. IPLC wanaweza kuwa na taratibu na masharti yaliyopo yanayopaswa kuchunguzwa pamoja na kujumuishwa.

Kujadiliana kuhusu mgogoro kutasaidia TNC na IPLC kujifunza kuhusu maadili, matarajio, na mizozo ya zamani ya mtu mwingine, ambayo hujitokeza katika shughuli yoyote ya ushirikiano. Lakini mchakato wa kujadiliana na kuandaa mpango hauhitaji kuwa mgumu. Ikiwa TNC na IPLC wamekubaliana, mpango unaweza kuwa tu wa kuelezea chaguo zilizo hapa chini na jinsi zinavyopatikana. Huenda ikajumuisha vitu mahususi, kama vile majina ya wapatanishi wanaoaminika walioteuliwa mapema.

TNC inapendelea kutatua migogoro bila kuchukua hatua za kisheria. Hata hivyo, huenda kukatokea hali zinazosababisha kusikilizwa kwa kesi kortini. Endapo kuna uwezekano wa kuwepo kwa kesi, rejelea maelezo ya Kuhusisha Wakili wa Nje na SOP ya Kesi Zinazosikilizwa Kortini na uwasiliane na timu ya kisheria ya TNC.

### Mazungumzo

Njia bora zaidi ya kuzuia migogoro kuchipuka kuwa malalamishi ni kuingia katika kila uhusiano ukiwa tayari kujifunza, mwenye heshima na mwaminifu. Kuendeleza mawasiliano huwezesha TNC kuona matatizo yakiibuka na kuyashughulikia moja kwa moja. Watu wanapoaminiana na kuelewana mwanzoni mwa mpango, matatizo yanaweza kusuluhishwa kupitia majadiliano ya timu.

Ili kujifunza na kufanya mazoezi ya mazungumzo, angalia Ukurasa wa Mafunzo Tofauti kwenye CONNECT na Nyenzo za Usikilizaji na Mazungumzo ya Wenyeji na Rasilimali za Usimulizi zilizoorodheshwa kwenye sehemu ya Vidokezo na Zana katika moduli hii. Moduli ya Mafunzo & Majadiliano ya Mwanzo pia inajadili kwa kina kuhusu kudumisha uhusiano.

Mazungumzo wazi yanapaswa kuwa sehemu ya ushirikiano wowote wa IPLC. Lakini mizozo inaweza kuzuka kutokana na hali ngumu au mgongano wa maslahi—na hata wahusika waliozoea mazungumzo wazi wanaweza kukwepa kujadili mada hizi ngumu. Mazungumzo yanayohimizwa katika mwongozo huu ni mazungumzo ya hiari yaliyoundwa kushughulikia mgogoro maalum.

Hii inamaanisha kuwa mazungumzo sharti yapangwe mapema:

- Je, wahusika wote wanapatikana?
- Je, wahusika wamearifiwa mapema kuhusu majadiliano ili waweze kujiandaa?
- Je, tunazingatia muda, mahitaji na masharti yaliyowekwa na IPLC?

- Je, nyenzo muhimu za kujifunza zinapatikana?
- Je, hali za mazungumzo huhakikisha usalama wa kimwili na kihisia kwa wahusika?

Kuzingatia vigezo hivi ni muhimu, lakini haitaji kuwa rasmi. Isitoshe, kanuni za Nia Njema na Uhusiano wa Kushirikiana zinahitaji TNC kuingia katika mazungumzo iliwa tayari kusikiliza na kushughulikia mashaka. Isitoshe, kanuni za Nia Njema na Uhusiano wa Kushirikiana zinahitaji TNC kuingia katika mazungumzo tayari kusikiliza na kushughulikia malalamishi. La sivyo, mazungumzo yanaweza kusababisha watu wasiaminiane au yanaweza kupuuzwa.

## Upatanisho

Upatanisho ni utaratibu wa utatuzi wa mgogoro ambao huwa rasmi na maalum zaidi ikilinganishwa na Mazungumzo. Kimsingi, kutumika kwake kunategemea uelewa wa kina na udumishaji wa maadili na kanuni zilizopo za kitamaduni za utatuzi wa mgogoro.

Upatanisho unapaswa kutegemea taasisi na vikao vya IPLC, na sherehe za kitamaduni au desturi zilizobuniwa na IPLC, kwa kuzingatia masharti ya serikali au mfadhili (soma Suala Kuu: Je, kuna utaratibu wa kushughulikia malalamishi ulioidhinishwa na mfadhili au serikali ya nchi husika?).

Katika miktadha mingine, mchakato wa upatanisho wa nje unaweza kuwa wenye udhaifu, hivyo haipaswi kujumuishwa katika Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro. Lakini wakati mwingine, kuwa na mpatanishi wa nje anayeaminika kunaweza kukubalika au hata kupendelewa. Usuluhishi huchochea ushiriki wa kina, kuelewana na maafikiano kati ya wahusika, au inaweza kusaidia wahusika kuondoa hali ya kutokuaminiana iliyokuwepo hapo awali. Mchakato wa upatanisho unapaswa kupelekea matokeo, kama kuzingatia mapendekezo ya mpatanishi.

Upatanisho sio usuluhishaji, na upatanisho uliofafanuliwa kwenye mwongozo huu hautazingatiwa kuwa wa kisheria au hata wa kubana kisheria. Hata hivyo, mpatanishi anaweza kutoa mapendekezo ambayo wahusika hawapendelei, lakini wanaweza kusikiliza, kutokana na ahadi ya awali ya kuhusika katika mchakato wa upatanisho.

Ikiwa kutumia mpatanishi wa nje kunakubalika, TNC na IPLC wanapaswa kumtambua mtu huyo mapema. Anaweza kuwa msomi au mtaalamu binafsi au taasisi. Mpatanishi wa nje anapochaguliwa, jina lake na anwani yake zinapaswa kujumuishwa katika Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro.

## Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya Utangulizi ya moduli hii, mara nyingi, mgogoro inaweza kutatuliwa kwa njia ya Mazungumzo au Upatanisho. Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni unahakikisha kuwa TNC inawajibikia vitendo vyake, na inatoa njia mbadala kwa IPLC kutoa mashaka na kufikia nyenzo ili kuchunguza na kutatua migogoro. (Angalia Kiambatisho cha V ili upate maelezo zaidi kuhusu mchakato huu.)

Mchakato wa Maadili na Kufuata kanuni ni utaratibu mzuri wa kusikiliza, kujibu maswali au kuelekeza mashaka kwa wahudumu wa mpango wa TNC ili kupata ufafanuzi. Tunapopokea malalamishi, Ofisi ya Maadili na Kufuata Kanuni inaweza kushauriana na wafanyakazi wa mpango ili kupata maelezo au kuondoa kutokuelewana. Mra nyingi, suluhisho linalokubalika na pande zote linaweza kupatikana, na malalamishi yanaweza kutatuliwa.

Wafanyakazi wa TNC au wahusika wengine wanaweza kuwasiliana na Timu ya Maadili na Kufuata Kanuni wakati wowote kuwasilisha swali au mashaka mtandaoni kwenye Huduma ya Usaidizi, www.nature.org/tnchelpline. Huduma ya Usaidiz ya TNC inapatikana mtandaoni na kupitia simu,

ujumbe au barua saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki kwa lugha nyingi. Malalamishi yanaweza kuwasilishwa bila kumtambulisha aliyewasilisha na yatashughulikiwa kwa usiri kadiri iwezekanavyo, na yatafichuliwa tu kwa wanaohusika. Mtu anapopiga simu kwa Huduma ya Usaidizi, atazungumza na wakala wa nje atakayenakili malalamishi hayo na kuyashiriki na Timu ya Kufuata Kanuni na Maadili ya TNC. Mtu anapowasilisha malalamishi mtandaoni, malalmishi hayo hutumwa moja kwa moja kwa Timu ya TNC ya Maadili na Kufuata Kanuni (angalia Kanuni ya Maadili).

Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni unapaswa kufafanuliwa na maelezo kuhusu jinsi ya kuifikia yanapaswa kutafsiriwa katika lugha inayopendelewa na IPLC na kusambazwa katika eneo lote la mradi. Ikiwa IPLC hazungumzi mojawapo ya lugha zinazopatikana kupitia Huduma ya Usaidizi, huenda TNC ikahitaji kuajiri mtafsiri ili kusaidia kuwasilisha malalamishi. Malalamishi yaliyonakiliwa yanaweza kuwasilishwa kwa lugha yoyote.

Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni unapaswa kuwasilishwa kama chaguo katika Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro mwanzoni mwa mpango mpya au haraka iwezekanavyo katika ushirikiano unaoendelea.

**Kanuni Dhidi ya Kulipiza Kisasi**

Kwa kuwa kiufafanuzi utatuzi wa mgogoro hutokea penye mifarakano, huenda ikaandamana na uhasama, mfadhaiko na wakati mwingine fujo na kujitenga na wengine. Ulipizaji kisasi dhidi ya watu waliowasilisha malalamishi ni shida inayokabili taasisi mbalimbali katika ngazi zote. Hofu ya kisasi ni kikwazo kikubwa katika kuripoti matatizo, hasa kwa wale ambao wataathirika zaidi. Kama ilivyoelezwa kwenye Kanuni yetu ya Maadili, TNC haitaruhusu ulipizaji kisasi dhidi ya watu wanaouliza maswali au kuwasilisha malalamishi kwa nia njema kuhusu utovu wa nidhamu.

Mikakati ya kuzuia ulipizaji kisasi inapaswa kujumuishwa kwenye Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro na inaweza kujumuisha:

- Taratibu zinazoruhusu na kudumisha usiri wa utambulisho
- Taratibu zinazolinda usiri wa maelezo nyeti
- Taratibu za kulinda usalama wa kimwili na kisaikolojia wa washiriki na vikao vya uadilifu, ikiwemo kuheshimu mahitaji halali ya watu wengine ya kutokaribiana
- Ujumbe dhahiri kutoka kwa TNC na washirika wote wa mpango kuhusu kupigwa marufuku kabisa kwa ulipizaji kisasi
- Maonyo kuhusu athari za kulipiza kisasi

**Suala Kuu: Je, Kuna Utaratibu Maalum wa Kushughulikia Malalamishi Ulioidhishwa Mfadhili au Serikali ya Nchi Husika?**

Wafanyakazi wa TNC wanahitaji kujua ikiwa kuna utaratibu maalum wa kushughulikia malalamishi unaohitajika na serikali ya nchi husika au mdhamini anayefadhili mpango huo. Kwa mfano, IUCN na Kituo cha Mazingira Duniani cha Benki ya Dunia huhitaji waafadhiliwa kuzingatia utaratibu wa kushughulikia malalamishi yote.

Ikiwa utaratibu wa kushughulikia malalamishi umeidhinishwa, wafanyakazi wa TNC wanapaswa kubaini ni aina zipi za mizozo zinaweza kutatuliwa kwa utaratibu huu na ikiwa IPLC imekubali utaratibu huo utumike au iko tayari kuutumia. Kanuni ya Maadili ya TNC inahitaji uzingatiaji wa sheria za kieneo, ikijumuisha zile zinazohitaji mhusika kutumia utaratibu wa kushughulikia malalamishi. Kutozingatia utaratibu uliowekwa na mojawapo wa wafadhili wa TNC kutachukuliwa

kuwa TNC imekiuka makubaliano ya ufadhili kati yake na mdhamini.

Hivyo TNC inapaswa kuanza kwa kufahamu na kuzingatia taratibu hizi. IPLC ingependa kutumia, kama raia wa nchi hiyo, utaratibu wa kushughulikia malalamishi unaohitajika na nchi husika, lakini haitahitajika kuzingatia utaratibu wa mfadhili endapo hakuna makubaliano ya ufadhili kati yao.

IPLC ikikubali kutumia utaratibu unaohitajika wa kusuluhisha malalamishi, na utumike katika mizozo ambayo haijasuluhishwa kupitia makubaliano mengine ya kindani, utaratibu unaohitajika wa malalamiko unapaswa kufuatwa.

Iwapo IPLC haikubali kutumia utaratibu unaohitajika wa kusuluhisha malalamishi, mchakato huo huenda ukahitajika kusistishwa TNC ikiendelea kukusanya maelezo na hali zinazoifanya IPLC kutohusika. Ikiwa TNC na IPLC hazikubaliana kufuata mchakato wa kushughulikia malalamishi, huenda mchakato ukasitishwa.

Wakati mwingine, huenda TNC na IPLC wakawasilisha ombi maalum kwa serikali au mfadhili. Endapo utaratibu mbadala wa kushughulikia mashaka ya serikali au wafadhili umependekezwa mapema, inaweza kuungwa mkono na serikali au wafadhili, hasa ikiwa inahusisha utamaduni, inafaa, inapunguza gharama za usimamizi na inapelekea kuwepo kwa matokeo mazuri.

**Suala Muhimu: Kukubali Taratibu**

Kama tulivyojadili, TNC na IPLC wanapaswa kuelewa na kukubali mapema taratibu za utatuzi wa mgogoro. Kushughulikia mashaka ya IPLC mapema kutahimiza uhalali na matokeo mazuri ya taratibu. Pamoja na kutoshauriana, sifa ya desturi duni ya kutatua mgogoro ni pale ambapo watu wa nje wanasisitiza kutumia taratibu zao, ambazo huenda ni geni kwa IPLC. Kisha watu hao wa nje wanashangaa IPLC wanapokosa kutumia taratibu hizo au wanapokosa kukubali uhalali wa matokeo. Hali hii inasababisha uhasama kando na mzozo uliopo, badala ya uhusiano thabiti unaotokana na mchakato madhubuti wa utatuzi wa mgogoro.

Ufafanuzi kuhusu chaguo zilizopo inaelezea kuhusu jambo hili kwa kiwango fulani, kwa kuruhusu IPLC kuweka kando taratibu zozote ambazo hawapendi au zisizoeleweka. Vilevile, njia mbili za kwanza zilizopendekezwa katika mwongozo huu—Mazungumzo na Upatanisho—vinaegemea zaidi kuwa vigezo badala ya taratibu rasmi, hivyo inamaanisha kuwa zinaweza kutumika katika mifumo inayopendekezwa na IPLC.

IPLC zina njia zao za kufanya mazungumzo ya kukusudia na, mara nyingi, huendesha mchakato maalum na kumjumuisha mtatuzi wa nje kwa madhumuni ya upatanisho. Ni muhimu kwa mfanyakazi wa TNC kujifunza kuhusu jinsi IPLC wanavyochukulia na kushiriki katika michakato hii, kutegemea maelezo yaliyoshirikiwa na IPLC Kujumuisha pamoja mikakati ya TNC na IPLC knaweza kuwa muhimu katika kushirikiana na kuaminiana.

La muhimu zaidi, kuwa na njia ya utatuzi wa mgogoro inayojumuisha vigezo vya desturi iliyopo ya IPLC kunamaanisha kuwa kuna uwezekano mkubwa wa suluhu hizi kutumika migogoro inapozuka, na kuna uamuzi wowote utakuwa na uhalali zaidi kwenye IPLC.

Njia za utatuzi wa mgogoro zinaweza kutumika kwa namna mbalimbali:

Katika **Mazungumzo**, mhusika wa IPLC anapotaka kuwasiliana na mwenzake ili kuwasilisha malalamishi, je, kuna sheria au sera zilizopo za kuhakikisha hali ya kuheshimiana na kuhimiza mazungumzo? Mifano inaweza kuhusisha sera za kishirika, kama vile kuhusisha mhusika mahususi badala ya mlalamishi, na desturi, kama vile mazoea ya kushiriki chakula kabla au baada ya mazungumzo.

Katika **Upatanisho**, huenda mizozo na malalamishi ikashughulikiwa katika vikao visivyo vya kutoa uamuzi lakini vilivyopangwa mbele ya baraza za usimamizi za IPLC, mabaraza ya wazee au vikao kama hivyo. Mhusika fulani kwenye IPLC anaweza kuwa mpatanishi katika mizozo ya ndani ya jamii; kwa hivyo anaweza kosa kuwa na upendeleo, tofauti na jukumu la kuwa wakili wa IPLC, ambalo ni jukumu muhimu lakini tofauti.

Mpango unaotoa upatanisho unaoendeshwa na mtu kama huyo una uwezekano mkubwa wa kutegemewa na kuheshimiwa, kwa sababu mtu huyo anaaminika. Kunaweza pia kuwa na mtu wa nje anayeaminika ambaye amesaidia kutatua mizozo ya watu wa nje hapo mbeleni. Au huenda kuna jopo la watu wanaoaminika ambapo wahusika wanaweza kuteua mpatanishi miongoni mwao.

Njia zozote za kutatua mizozo zinazotumiwa na IPLC zinapaswa kukaguliwa. Mara nyingi, utumiaji wa taratibu kama hizi huweka matakwa kuwa TNC au wahusika wengine watashurutishwa na uamuzi wa taasisi ya IPLC na sio kuuchukulia kuwa ushauri tu. TNC inapaswa tu kukubali kuzingatia taratibu hizi wakati ina imani katika uwezo wetu wa kuzingatia uamuzi ulioafikiwa. Ni bora kukataa kwa upole kuzingatia taratibu hizi za kufanya uamuzi badala ya kuzizingatia lakini ukose kukubali matokeo.

Kwa kawaida, IPLC huelewa mtu wa nje anapokosa kuzingatia kikamilifu taratibu za kufanya uamuzi za IPLC. Mara nyingine hawaruhusu watu wanje kutumia taratibu zenyewe. Lakini makubaliano ya kutumia taratibu za IPLC ni kielelezo cha juu zaidi cha Nia Njema na Kujiamulia Mwenyewe. Hata ikiwa makubaliano haya yanahitaji kufanywa kuwa ya kushughulikia aina fulani za mizozo au hali mahususi, kwa mfano, baada ya kuteua mbinu nyingine husika, makubaliano ya kuzingatia taratibu za IPLC ni nyongeza muhimu katika Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro.

**Suala Muhimu: Uhusishaji**

Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro unapaswa kuchunguzwa vizuri ili kutathmin ikiwa kuna vizuizi vya ufikiaji kwa wanachama wa IPLC, na marekebisho na maboresho yanapaswa kufanywa ili kushughulikia vizuizi hivyo kadri iwezekanavyo. Kwa mfano, wanawake wanaweza kutojumuishwa katika taratibu IPLC za utatuzi wa mgogoro za ndani. Hata ikiwa Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro unajumuisha ushiriki wa wanawake, vizuizi vya kisaikolojia au kijamii huenda vikawazuia wanawake binafsi kushiriki.

Je, hili linaweza kushughulikiwa vipi kwa kuzingatia desturi ya IPLC ya Kujiamulia Mwenyewe?

Uwezekano unajumuisha kukuza ushiriki wa wanawake, kuitisha vikao tofauti au kuweka taratibu za kupokea maoni, au kutoa suluhisho kwa wanawake katika jamii. Ni muhimu kufahamu na iwapo vikundi vilivyotengwa vingependa kushiriki katika mchakato wa utatuzi wa mgogoro, kwa sababu wafanyakazi wa TNC huenda wakawa na mitazamo, matarajio au maadili ya nje tusipofahamu kikamilifu kuhusu yanayotukia.

## Hatua ya Pili: Tekeleza Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

**Kiolezo: Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro**

Tazama Kiolezo cha Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

Mgogoro unapozuka, wafanyakazi wa TNC sharti watumie njia za utatuzi wa mgogoro zilizowekwa mapema, kwa njia inayozingatia Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi—hasa Nia Njema, Kufanya Uamuzi wa Kibinafsi Uwajibikaji, Usawa & Uhusishaji. Utatuzi hautegemei kitendo kimoja pekee, bali vitendo anuwai wakati wa mgogoro.

Utekelezaji utategemea hali iliyopo, kwa hivyo mwongozo maalum unahitajika. Endapo kuna utata, wafanyakazi wanapaswa kushauriana na Mshauri wa Kisheria, Timu ya Kimataifa ya Wenyeji na Jamii za Eneo hilo na Timu ya Utofauti Ulimwenguni, Usawa na Uhusishaji wa Ulimwengu.

Sharti wafanyakazi waendelee kufuatilia michakato ya utatuzi wa mgogoro hadi wahusika wote watakaporidhika kuwa mizozo imetatuliwa. Hii ni muhimu kwa sababu mbili:

- Mgogoro wenyewe, ambao mara nyingi hutokana na suala muhimu, unaweza kujitokeza tena kwa njia tofauti na yenye ubishi zaidi endapo haujatatuliwa kikamilifu.
- Ufuatiliaji wa kindani huongeza kuaminika kwa Mpango wa Utatuzi wa Migogoro na uaminifu wa TNC kama mshirika.

Taratibu hazipaswi kuruhusiwa kuzuia utatuzi halisi. Huenda hii ikafanya mchakato wa utatuzi wa mgogoro kuchukuliwa kuwa ukwepaji wa tatizo, badala ya mbinu ya kukusanya maelezo ya kina, kusuluhisha matatizo na njia ya kudumisha uhusiano.

TNC na IPLC wanapaswa kuzingatia vigezo vifuatavyo katika utekelezaji wa Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro:

**Dhana za Utatuzi wa Mgogoro**

**Usawa:**
Wahusika wote wanapaswa kufahamu jinsi ya kuwasilisha mashaka na jinsi kila mzozo utakavyoshughulikiwa. Mchakato wenyewe sharti uhusishe utoaji maelezo, ushauri na ujuzi unaohitajika ili kutatua migogoro kwa njia ya haki, inayofaa na ya heshima. Wakati mwingine, huenda TNC ikahitaji kutoa nyenzo za ziada, kama vile maelezo, ushauri, au huduma za tafsiri.

**Uwazi:**
Watu wote hufahamishwa kuhusu hatua zilizopigwa pamoja na matokeo; utekelezaji, ufuatiliaji na kufanya uamuzi ni michakato wazi.

**Kusuluhisha na Kupunguza Hatari:**
Athari mbaya zinapaswa kushughulikiwa mapema, ili kuzuia madhara makubwa na mrundiko wa malalamishi.

**Ufuatiliaji wa Kina:**
Japo njia za utatuzi wa mgogoro zinapaswa kuwa madhubuti na zenye kuzingatia wakati, huenda ikachukua muda, ikahitaji subira na ushughulikiaji ili kuweza kutumia njia hizi kwa ufanisi.

Wakati mwingine utatuzi wa mgogoro hutokea katika hali ambapo matukio yanatukea upesi, na wahusika wanaanza kuhisi kuwa mchakato wenyewe unajivuta. Wakati mwingine, utatuzi wa mgogoro hutokea wakati mmoja na vipaumbele vingine, hasa inapochukuliwa kuwa si ya dharura. Ufuatiliaji unapaswa kuendelea kwa nia njema hadi mgogoro utakapotatuliwa kikamilifu.

## Hatua ya Tatu: Endelea Kurejelea na Kubadilisha Mpango

Hakuna Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro ulio timilifu kuanzia mwanzo. Inawezekana kuwa matatizo makubwa na vizuizi vitaibuka mara tu taratibu katika mpango zitakapojaribiwa wakati wa utekelezaji. Katika hali nyingi, hii inaonyesha tu ukweli uliopo badala ya mipango mibaya, lakini jibu linapaswa kuwa, katika hali yoyote ile, mchakato wa kufikiria na usijilinde wa kujifunza na kurekebisha mpango huo ili kushughulikia changamoto mpya zilizoeleweka.

Mchakato unahitaji:



a) **kutambua upungufu na kasoro kwenye mpango ambazo zilibainika wakati wa utekelezaji;**



b) **kuzikubali kama matatizo na kutojaribu kuzisitiri au kuzitetea;**



c) **kuchunguza sababu na athari;**



d) **kubuni mbinu za utatuzi, mikakati ya upunguzaji na mchakato wa kutumia mpango kwa kushirikiana na washirika.**

**Zana zinazotumika kwenye mchakato huu ni pamoja na:**

- Ukaguzi unaofanywa na mfanyakazi wa TNC au washauri wa nje mara kwa mara au unaofanywa kushughulikia matatizo au changamoto zozote zinazoibuka;
- Ukusanyaji wa maoni ya washirika, pamoja na utaratibu unaowaruhusu kutoa maoni bila utambulishi wao kufichuliwa;
- Kuandaa warsha baada ya mpango kukamilika ili kutathmini ilivyokuwa, au kuwa na makongamano ya ukaguzi wakati wote wa mchakato ili kukusanya maoni na kujadili uboreshaji. (Rejelea Moduli ya Ufuatiliaji, Tathmini & Marekebisho ili upate maelezo zaidi kuhusu taratibu kama vile mikutano ya kutathmini.)

Kunapaswa kuwa na juhudi za mara kwa mara ili kutoa uhamamisho kuhusu kuwepo, hali na uwezo wa kufikia Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro. Zana za utatuzi wa mgogoro zinajulikana kwa kutotumiwa kwa sababu tu hakuna mtu anayezijua, au kutotumiwa hadi tatizo linapotokea, wakati hisia ziko juu na ni vigumu kutumia mchakato usiojulikana.

Kuelimisha jamii kuhusu mbinu zinazopatikana, pamoja na ufuatiliaji wa mara kwa mara ikiwa IPLC wanaelewa na kukubali chaguo zilizopo, utasaidia kuwezesha zitumike. Hii inapaswa kuwa juhudi ya kweli na ya mara kwa mara na kutimizwa kwa kutaja taratibu hizi mara kwa

mara wakati wa kurejelea IPLC. Hatua inaweza pia kuondoa unyanyapaa uliopo katika utumiaji wa taratibu za utatuzi wa mgogoro katika miktadha mengine ya jamii.

**Rasilimali: Utatuzi wa Mgogoro**

Viungo vya kuekeleza kwenye taratibu za ushughulikiaji malalamishi na michakato ya uwajibikaji ya mashirika yafuatayo vinapatikana hapa:

- African Development Bank
- African Development Bank
- European Bank for Reconstruction and Development
- Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa
- Inter-American Development Bank
- Shirika la International Fund for Agriculture Development
- Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa
- Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa
- Shirika la Usitawi wa Viwanda la Umoja wa Mataifa
- Benki ya Dunia
- Shirika la Conservation International
- Development Bank of Southern Africa
- Wizara ya Utunzaji wa Mazingira
- Utunzaji wa Mazingira Uchina
- Shirika la International Union for Conservation of Nature
- Shirika la World Wildlife Fund

**Nyenzo za usikilizaji za hiari**

- United States Institute of Peace – Kusikiliza kwa Makini. Nyenzo hii ina PDF ya kupakuliwa inayohusu kanuni msingi ya kusikiliza kwa makini.
  - Kusikiliza
  - Kufafanua
  - Kutathmini
  - Kueleza
  - Kuhimiza
- Mawasiliano Bila Fujo: Makala haya yanaorodhesha na kutoa mifano ya hatua nne za kuwasiliana kwa njia ya maridhiano. Hatua hizi nne ni pamoja na:
  - Kuzingatia ukweli badala ya kupiga chuku au kufanya maamuzi
  - Kutambua hisia, badala ya kutoa mawazo au matarajio nasibu
  - Kugundua matakwa yanayosababisha hisia yako mahususi
  - Toa maombi wazi kulingana na matamanio haya, wala sio madai

Mwongozo wa Sera na Taratibu za The Nature Conservancy, Kuripoti Ukiukajiwa Sheria na Sera (2017) hutoa "utaratibu wa wafanyakazi kuripoti kuhusu masuala ya nia njema kuhusu tuhuma za ukiukaji wa sheria kwa upande wa Uhifadhi, kushirikiana katika uchunguzi wa mahakama, shirika, utekelezaji wa sheria, au taasisi nyingine ya serikali, au kutambua

**Utatuzi wa mzozo kiasili / "upatanisho"**

Mpango wa Kiasilia wa Upatanishi ni mkakati wa Native American Rights Fund, shirika linalohusika na maswala ya haki za kabila.

- Orodha ya Nyenzo
- Video kwenye ukurasa wa "Kuhusu" ulio hapo juu inaelezea malengo makubwa yaliyojadiliwa kwenye moduli hii, yaani, kutumia utatuzi wa mzozo kukabili matatizo kabla yaibuke, kuimarisha jumuiya na kuanzisha mazungumzo kati ya jumuiya mbalimbali.
- "How Indigenous Voices Can Get Lost in Mediation," Rebecca Hiers (Novemba 2018).

**Vitabu vya upatatnisho**

Christopher Moore et al., Mchakato wa Upatanisho: Mikakati ya Utatuzi wa Mzozo

**Indigenous dialogue and storytelling**

Jo-ann Archibald, Indigenous Storywork (2008). Nakala ya PDF inatolewa na mchapishaji

Val Napolean & Hadley Friedland, "An Inside Job: Engaging with Indigenous Legal Traditions Through Stories" (2014)

**Nyenzo zingine**

"Practicing Cultural Safety," from Towards a New Relationship, BC Association of Social Workers (2016)

**3A. Utafiti wa Wenland kuhusu Utatuzi wa Mgogoro**




Wen imeidhinisha mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zilizoganda. Wanavutiwa pia na ufadhili wa kila mwaka wa utunzaji unaotolewa na FrostLock, japo FrostLock haijatoa takwimu halisi — makadirio tu.

Tazama Utafiti

## Orodha ya kukagulia Utatuzi wa Mgogoro

**Katika mchakato mzima wa utatuzi wa mgogoro**

- [ ] Fafanua jinsi TNC inavyohimiza kuaminiana, uwajibikaji na uwazi baina yake na IPLC
- [ ] Shirikiana kuunda mchakato wa kuaminika wa utatuzi wa mgogoro unaochukuliwa kuwa halali na wahusika wote

**Hatua ya Kwanza: Unda Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro**

- [ ] Thibitisha iwapo kuna mchakato wa utatuzi wa mgogoro unaohitajika na serikali au mfadhili na ikiwa IPLC wako tayari kuuzingatia
- [ ] Iwapo IPLC hawakubali kutumia mchakato unaohitajika, shirikiana katika kubuni mchakato mbadala
- [ ] Endapo hakuna mchakato wa utatuzi wa mgogoro unaohitajika na mfadhili au serikali ya nchi husika, au ikiwa kuna moja ambayo inatumika tu kwa malalamishi mahususi, shirikiana na IPLC na mkubaliane kuhusu njia za utatuzi wa migogoro ambazo zinazingatia utamaduni
- [ ] Mkubaliane kuhusu Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro na IPLC unaozingatia Mazungumzo, Upatanisho na Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni

**Mazungumzo**

- [ ] Jifunze kuhusu njia za mazungumzo na taratibu zinazopendekezwa na IPLC
- [ ] Toa mafunzo kwa wafanyakazi wa TNC kuhusu kufahamu na kujifunza mazungumzo
- [ ] Kuwepo na mazingira salama kimwili na kihisia kwa mazungumzo
- [ ] Tenga muda wa mazungumzo; zingatia mapendeleo, mahitaji na masharti ya muda ya IPLC; na utoe maelezo na nyenzo zaidi kama inavyohitajika

## Orodha ya kukaguli ya Utatuzi wa Mgogoro (Imeendelezwa)



**Upatanisho**

- [ ] Ikiwa IPLC wako tayari, jadili michakato yao inayopendelewa ya kutatua migogoro. Baini ikiwa mchakato uliopo wa IPLC ni mwafaka katika utatuzi wa mizozo inayohusisha watu wa nje
  - Iwapo wafanyakazi wa TNC wanahitaji maelezo au hati za ziada nje ya mchakato wa IPLC, TNC inaweza kuomba usaidizi wa IPLC katika kuzipata
- [ ] Amua mwakilishi wa kila mhusika katika mchakato huo na ujumuishe majina yao katika Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro
- [ ] Jadili msimamo wa IPLC kuhusu kutumia watatuzi au wapatanishi wa nje katika kutatua mizozo
  - Iwapo inakubalika, tambua wapatanishi au watatuzi wanaoaminika kisha ujumuishe majina yao katika Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro
  - Ikiwa hairuhusiwi kuhusisha wapatanishi au watatuzi wa nje, jadili na unakili chaguo nyingine ambazo wahusika wote wanakubali kutumia
- [ ] Amua jinsi mchango wa vitambulisho tofauti vya kijamii utakavyosaidia katika mchakato

**Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni**

- [ ] Fafanua Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni na jinsi unavyoweza kutumiwa na wafanyakazi na washirika wa TNC (Angalia Klambatisho cha V na www.nature.org/tnchelpline)

**Hatua ya Pili: Tekeleza Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro**

- [ ] Hakikisha wahusika wanajua kuhusu Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro, kisha ufafanue taratibu, michakato na matokeo
- [ ] Toa masharti dhidi ya kulipiza kisasi
- [ ] Amua kwa pamoja jinsi mchakato wa mgogoro utakavyoandikwa
- [ ] Wasiliana na Mshauri wa Kisheria, Timu ya Kimataifa ya Wenyeji na Jamii za Eneo hilo na timu ya Utofauti Ulimwenguni Usawa na Uhusishaji ikiwa kuna tashwishi
- [ ] Endapo athari mbaya itagunduliwa, tatua kwa haraka na kwa haki ili kuzuia malamishi kuongezeka na hali kuwa mbaya zaidi.

## Orodha ya kukagulia Utatuzi wa Mgogoro (Imeendelezwa)



**Hatua ya Tatu: Endelea Kurejelea na Kubadilisha Mpango**

- [ ] Endesha mchakato wa utatuzi wa mgogoro kwa nia njema, pamoja na ufuatiliaji wa kina hadi wahusika watakaporidhika kuwa mgogoro umetatuliwa
- [ ] Tumia mchakato wa utatuzi wa mgogoro kusaidia katika kuendelea kufunza TNC na IPLC
- [ ] Kagua na usasishe Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro mara kwa mara, hasa wakati kuna mabadiliko muhimu kuhusu timu ya mradi, washirika, mpango wa utendakazi au bajeti ya TNC

## Hati za Kuhifadhi

**Angalia Moduli ya Hati ili upate maelezo zaidi kuhusu hati zinazohitajika**

- [ ] Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro, inajumuisha njia zinazoweza kutumika na jinsi mpango ulivyoundwa kwa pamoja na kushirikiwa na IPLC
- [ ] Hati ya kila mzozo, jinsi ulivyoshughulikiwa na utatuzi wake, pamoja na:
    - Aliyewasilisha malalamishi (ikiwa anajulikana) na wakati, hali ya mzozo, waliohusika na njia zilizotumiwa
- [ ] Matokeo ya mazungumzo, upatanisho na njia nyingine, makubaliano na hatua zinazofuata
- [ ] Marekebisho au masasisho ya Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro kutegemea hali na mafunzo

## Maelezo

[1] [1] Angalia Mwongozo wa CbD 2.0, Kiambatisho cha C: Maswali kuhusu FPIC na Kanuni za Kulinda Maslahi ya Jamii.
https://www.conservationgateway.org/ConservationPlanning/cbd/Pages/default.aspx

[2] Angalia Mwongozo wa CbD 2.0, Kiambatisho cha D: Uzingatiaji wa Haki za Binadamu katika Miradi ya Uhifadhi: Mpango wa The Nature Conservancy.
https://www.conservationgateway.org/ConservationPlanning/cbd/Pages/default.aspx

[3] Angalia https://www.iucn.org/sites/dev/files/iucn_esms_manual.pdf (IUCN); https://www.conservation.org/docs/default-source/gef-documents/20151115-accountability-and-grievance-mechanism.pdf?sfvrsn=92633125_2 (CI); na https://www.worldwildlife.org/publications/wwf-project-complaints-resolution-policy (WWF).



# Utatuzi wa Mgogoro

## 3A. Utafiti wa Wenland:

**Wen wameidhinisha mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi. Wanavutiwa pia na ufadhili wa kila mwaka wa uhifadhi unaotolewa na FrostLock, japo FrostLock haijatoa takwimu halisi — makadirio tu.**

Majadiliano ya kina ya mipango yanaendelea kati ya TNC, FrostLock, Wen na serikali ya Albania.

| **Kwa mfano** | *Mawazo na Mwongozo* |
| --- | --- |
| **1**<br>**TNC inapotoa pendekezo la kuwepo kwa Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi huo, viongozi wa Wen wanasema wamechoka na kuwa Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro si muhimu. *Je, TNC inapaswa kuendelea bila Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro?*** | *Hii inaonyesha umuhimu wa Kutatua Mgogoro mapema. Mchakato tata wa mashauriano unaweza kukatisha tamaa na kusababisha mizozo kwa urahisi. Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro unaweza kusaidia kuzuia usumbufu. Mchakato madhubuti wa utatuzi wa mgogoro unapaswa kutekelezwa kwa kushauriana na unafaa kujumuishwa katika kufanya uamuzi unaofaa. Hata hivyo, kuheshimu haki za binadamu ni mchakato endelevu, na bado kuna fursa ya kuunda mpango husika. TNC inapaswa kupendekeza mashauriano zaidi katika utatuzi wa mgogoro, kwa lengo la kufikia mpango unaokubalika na wahusika wote. Iwapo wahusika wanahitaji muda zaidi kufanya hivi, inakubalika kwa kuwa inaheshimu uamuzi wa kibinafsi.* |

| Kwa mfano | *Mawazo na Mwongozo* |
|---|---|
| **2**<br>**Mabaraza ya Wazee ya Wen inajadiliana na FrostLock kuhusu Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro lakini wanasisitiza kwamba TNC isihusishwe kwa sababu ya kiwango cha juu cha ushirikiano na kuaminiana kilichoko baina yao na TNC. *Je, TNC inapaswa kukubali?*** | *Mpango haupaswi kuonyesha kutoaminiana. Ni njia ya kuhimiza na kudumisha kuaminiana, na matarajio bayana kuhusu utatuzi wa mgogoro ni muhimu katika kuchochea hilo na kutekeleza kanuni kuu ya Uwajibikaji. Kwa hivyo, japo ni jambo zuri, TNC inapaswa kuhimiza kuwepo kwa Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro.* |
| **3**<br>**Wahusika wameandaa Mpango wa kina wa Utatuzi wa Mgogoro, lakini FrostLock inasema kuwa unapaswa kuwa wa kipekee—yaani, kwa kukubali mpango huo, jamii za Wen zinasalimisha haki yao ya kuwasilisha malalamiko yoyote kortini au kwa taasisi nyingine yoyote. *Je, TNC inapaswa kutoa mashaka?*** | *Ndiyo. TNC haipaswi kukataa pendekezo hili. Lengo letu, linalohusisha kanuni za Uwajibikaji, Usawa na Uhusishaji, ni kuimarisha na kuongeza haki, sio kuzidhoofisha. Kwa kuzingatia aina ya mradi, upeo na athari zitakazotokea haziwezi kujulikana. Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro ndiyo hatua ya kwanza ya makubaliano kuhusu jinsi ya kushughulikia mgogoro kwa njia ya madhubuti. Sio utaratibu wa kupunguza dhima au kuzuia usuluhishaji. Sera za kimataifa haziungi mkono kabisa usalimishaji wa njia za utatuzi.* |
| **4**<br>**Sawa na mfano uliotolewa hapo juu, isipokuwa FrostLock iwe inasisitiza tu kwamba wahusika sharti watumie taratibu zilizobainishwa kwenye Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro kabla ya kutumia mbinu nyingine. *Je, TNC inapaswa kutoa mashaka?*** | *Pia, masharti ya kutumia tu taratibu zilizotolewa hayapendekezwi, lakini yanaruhusiwa. Cha muhimu hapa ni kufanya Uamuzi Bila Kushurutishwa. Je, jamii ya Wen inaelewa kikamilifu masharti ya kutumia tu taratibu zilizotolewa pamoja na umuhimu wake, kwa mfano, kuweza kubashirika, ufanisi, uundaji wa rekodi kamili? Iwapo watu waWen wanaombwa wakubali hili kwa sababu huo ndio msimamamo wa FrostLock, kanuni ya Kufanya Uamuzi Bila Kushurutishwa huenda ikahitaji kukaguliwa.* |
| **5**<br>**Watu wa Wen wanasema kuwa mizozo yoyote ambayo haiwezi kutatuliwa kupitia upatanisho sharti iwasilishwe kwa Mabaraza ya Wazee ya Wen ili watoe uamuzi wa mwisho wa wa kubana. Ili kulinda maslahi ya kampuni dhidi ya kuwajibikia dhima isiyojulikana, mawakili wa FrostLock wanaamua kutoendelea kushiriki. *Je, TNC inapaswa kuchukua msimamo upi?*** | *TNC inapaswa kudumisha msimamo wao wa kuunga mkono IPLC kujiamulia wenyewe. Hata hivyo, kujiamulia mwenyewe huenda kukasababisha mambo mengine yatokee. Huenda FrostLock ikahitaji ufafanuzi kuhusu matokeo ya mchakato usiojulikana wa kisheria au unaohusishwa na sheria, nayo watu wa Wen huenda wakataka kuendelea na mpango wenyewe. TNC inapaswa kutafuta jinsi ya kushirikiana na FrostLock ili kuelewa hali inayoweza kutokea hasa endapo Baraza la Wazee litahusishwa, na jinsi ya kushirikiana na Wen kubaini jinsi uamuzi wa Baraza la Wazee ni muhimu kwa watu wa Wen kujiamulia wenyewe.* |

| Kwa mfano | *Mawazo na Mwongozo* |
|---|---|
| | *Huenda kukawa na mpango maalum wa Utatuzi wa Mgogoro unaowasilisha tu aina fulani za mgogoro kwa Mabaraza Wazee.* |
| **6**<br>**Sawa na mfano uliotolewa hapa juu, ila kikundi cha wanawake wa mojawapo ya jamii ya Wen, wanasema kwamba kwa kuwa Mabaraza ya Wazee ni ya wanaume pekee, utaratibu utakaotumika hutawapendelea wanawake.** | *Kimsingi, Tathmini ya Jinsia ifanywe wakati wa mashauriano kwa kutumia Mwongozo wa TNC wa Kujumuisha Usawa wa Kijinsia katika Uhifadhi. Tathmini hiyo ingefaa katika hatua hii ili kufahamu kuhusu usawa wa kijinsia. Inaweza kuonyesha makubaliano fulani katika watu wa Wen kuhusu hali ya usawa wa kijinsia na jinsi ya kuishughulikia. TNC haipaswi kulazimisha maadili yoyote katika mchakato wenyewe kwa kutounga mkono au kujiondoa. Badala yake, TNC inapaswa kujizatiti kuelewa na kutumia mbinu zinazozingatia utamaduni, kwa kuzingatia kanuni zinazongoza mchakato wa Mafunzo na Majadiliano ya Mwanzo. Licha ya hayo, Kanuni na Sera zote za Kulinda Maslahi ni muhimu katika hatua zote za utendakazi wa TNC, na wakati mwingine huenda TNC ikajiondoa kwenye mchakato usio wa usawa na usio jumuishi.* |

**Kiolezo:**

# Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

Kiolezo hii ni kielelezo cha kuanzia kubuni Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro ulioelezwa katika Hatua ya Kwanza ya Moduli ya Utatuzi wa Mgogoro wa Mwongozo. Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro ni muhimu sana katika kila hatua na inapaswa kujumuishwa katika maudhui yaliyopendekezwa katika Moduli ya Mafunzo na Mazungumzo ya Mwanzo na Moduli ya FPIC. Wafanyakazi wa TNC wanahitaji kukumbuka kuwa Kanuni ya Maadili ya TNC inahitaji kuzingatiwa katika utaratibu wowote wa kushughulikia malalamishi ulioidhinishwa na mfadhili au serikali ya nchi husika.

Utayarishaji wa Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro unaweza kuwa mchakato rahisi. Kimsingi, itajumuisha desturi na sera zinazopendekezwa na IPLC. Ikiruhusiwa na IPLC na TNC, mpango unaweza tu kutoa njia zilizopo za kutatua mizozo inayohusisha watu wa nje na jinsi njia hizo zinavyotumika. Maelezo fulani mahususi, kama vile majina ya wapatanishi wanaoaminika, yanaweza kujumuishwa ikiruhusiwa na IPLC.

Kiolezo hii inatoa mifano mitatu ya hali zinazoweza kutokea na vigezo vikuu vya Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro. Pia inajumuisha vigezo kadhaa vya kuzingatiwa na TNC na IPLC wakati wa kubuni njia za kutatua mizozo. Makubaliano kuhusu Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro yanapaswa kufanywa kwa njia mwafaka, inayoweza kujumuisha saini au herufi za mwanzo za majina ya watu, kutumiana barua pepe, kuinua mikono kwenye mkutano, utaratibu au sherehe.

Maelezo utakayojaza kwenye fomu hii **hayatahifadhiwa** ukiyajaza kwenye kivinjari. Jifunze mengi

Mpango:______________________________

Kipindi cha wakati: ______________________________

Tarehe:______________________________

Imesasishwa kuanzia: ______________________________

Imeidhinishwa na:

Jina:______________________

Jina:______________________

Jina: ______________________

Shirika au kikundi:

Jina:______________________

Jina:______________________

Jina: ______________________

# Matukio

## Tukio la 1

Kuna mchakato wa utatuzi wa mgogoro unaohitajika na mfadhili au serikali ya nchi husika na IPLC **wako tayari** kuuzingatia. [Ambatisha hati za mchakato utakaotumika]

## Tukio la 2

Kuna mchakato wa utatuzi wa mgogoro unaohitajika na mfadhili au serikali ya nchi husika, lakini IPLC **hawakubali** kuufuata.

[Ambatisha hati za uamuzi wa IPLC wa kutofuata]

1 Wakati mwingine, huenda TNC na IPLC wakawasilisha ombi maalum kwa serikali au mfadhili. Iwapo IPLC **wanakubali** kufanya kazi na TNC, wahusika wote wanaweza kushirikiana kwenye mchakato mbadala unaojumuisha taratibu zinazopendekezwa na IPLC na zinaoashiria Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi za TNC.

IPLC na TNC zinawasilisha mchakato mbadala kwa serikali au mfadhili na kutayarisha hati za matokeo.

[Ambatisha hati za mchakato mbadala na uamuzi wa serikali au mfadhili]

2 IPLC **wakikataa** kushirikiana na TNC katika mchakato mbadala, huenda mchakato huo ukasistishwa TNC ikiendelea kukusanya maelezo na sababu zilizopelekea IPLC kukataa kuhusika.

[Ambatisha hati za mchakato mbadala na uamuzi wa serikali au mfadhili]

3 IPLC **wasipofuata** utaratibu uliowekwa wa kushughulikia malalamishi, huenda mchakato ukasitishwa. [Ambatisha hati ya kusitishwa kwa mchakato]

## Tukio la 3

Hakuna mchakato wowote wa utatuzi wa mgogoro uliowekwa na mfadhili au serikali ya nchi husika, au kuna mchakato fulani unaotumika tu kwa malalamishi mahususi.

1 IPLC **wanakubali** kushirikiana na TNC kuhusu njia za kutatua migogoro ambazo IPLC wanachukulia kuwa halali na zinazozingatia deturi (angalia Vigezo Muhimu vya Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro).

[Ambatisha hati]

2 IPLC **wakikataa** kushirikiana na TNC katika mchakato wa kushughulikia malalamishi, huenda mchakato ukasitishwa au ukakomeshwa.

[Ambatisha hati]

## Vigezo Muhimu vya Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

**1** Wafanyakazi wa TNC wanajifunza na kufanya mazoezi ya **mazungumzo na stadi za utamaduni** katika kufanya kazi na IPLC. Taja mafunzo, warsha na mikutano mingine:

a.

b.

c.

**2 Taratibu na mbinu zinazopendekezwa na IPLC** za utatuzi wa migogoro kwa kuhusisha watu wa nje:

a.

b.

c.

**3** TNC na IPLC wakikubaliana kuwa Mazungumzo yatakuwa mojawapo ya njia za utatuzi wa mgogoro, taja:

a. Masharti yanayohakikisha wahusika wanaweza kushiriki, vikiwemo vikundi vya kijamii

i. Idadi ya marudio na muda wa vikao vya mazungumzo: ______________________________

ii. Mahali: ______________________________

iii. Muundo: ______________________________

iv. Lugha: ______________________________

b. Njia za kushiriki maelezo na kuhakikisha wahusika wote wamejulishwa mapema kuhusu yatakayojadiliwa ili waweze kujiandaa:

| |
|---|
| |

c. Masharti ya muda na mapendeleo ya IPLC kuhusu mazungumzo, kwa mfano, kutumia sera husika au kushirikisha mwakilishi badala ya mlalamishi:

| |
|---|
| |

d. Kanuni za kulinda usalama wa kimwili na kihisia wa wahusika:

| |
|---|
| |

**4** TNC na IPLC wakikubaliana kuwa Upatanisho utakuwa mojawapo ya njia za utatuzi wa mgogoro, taja:

a. Taasisi, vikao na desturi zinazotumiwa na IPLC kutatua migogoro, ikiwa wako tayari kushiriki maelezo haya:

i. ______________________________

ii. ______________________________

iii. ______________________________

b. Masharti yanayohakikisha wahusika wanashirikishwa kikamilifu, ikijumuisha vikundi vya kijamii

i. Idadi ya marudio na muda wa vikao vya mazungumzo: ______________________________

ii. Mahali: ______________________________

iii. Muundo: ______________________________

iv. Lugha: ______________________________

c. Taarisi, vikao na desturi zinazotumiwa na IPLC kutatua migogoro, ikiwa wako tayari kushiriki maelezo haya:

i. Mwakilishi (wawakilishi) wa IPLC: ______________________________

ii. Mwakilishi (wawakilishi) wa TNC: ______________________________

iii. Wahusika wengine: ______________________________

d. Majina ya wapatanishi wa kuaminika ambao IPLC na TNC zitawasiliana nao ikihitajika:

i. ______________________________

ii. ______________________________

iii. ______________________________

## 4. Imeendelezwa:

e. Ikiwa kuwahusisha watatuzi au wapatanishi si desturi au utaratibu wa kawaida, tumia njia nyingine zinazokubalika na wahusika wote, kwa mfano, mabaraza ya wazee au njia nyingine zisizo rasmi, lakini za hiari:

[Ambatisha hati zinazohusu njia nyingine za utatuzi]

i. ______________________________

ii. ______________________________

iii. ______________________________

f. Maelezo zaidi yanahitajika kuimarisha uelewa wa TNC au kutimiza matakwa ya hati za mpango au mchakato:

| |
|---|
| |

**5.** Mawasiliano kuhusu **Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni** kama njia za utatuzi wa mgogoro:

a. Soma Kiambatisho cha V na www.nature.org/tnchelpline

b. Maelezo kuhusu kutumia Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni:

| |
|---|
| |

## **6.** Kanuni dhidi ya kulipiza kisasi:

a. Taratibu zinazoruhusu na kudumisha usiri wa utambulisho:

b. Taratibu zinazolinda usiri wa maelezo nyeti:

c. Kanuni za kulinda usalama wa kimwili na kihisia wa wahusika:

d. Ujumbe dhahiri kutoka kwa TNC na kuhusu kupigwa marufuku kabisa kwa ulipizaji kisasi:

e. Maonyo kuhusu athari za kulipiza kisasi:

**7.** Kuwasiliana na wahusika wote kuhusu Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro, pamoja na kujumuisha maelezo kuhusu jinsi vitambulisho tofauti vya kijamii zilivyoshughulikiwa ifaavyo kwa kutumia kigezo cha

a. Idadi ya marudio na muda wa mawasiliano:

b. Mahali:

c. Muundo:

d. Maudhui ya mpango:

**8.** Hati kuhusu uundaji na utekelezaji wa Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

a. Hati zinazoonyesha jinsi IPLC na TNC ziliunda mpango:

b. Vigezo vya mchakato wa utatuzi wa mgogoro vitakavyonakiliwa na TNC:

c. Vigezo vya mchakato wa utatuzi wa mgogoro vitakavyonakiliwa na IPLC:

d. Kwa kila mzozo, andika:

i. Mlalamishi, ikiwa anajulikana, na wakati ____________________

ii. Hali ya mgogoro ____________________

iii. Waliohusika na taratibu zilizotumiwa ____________________

iv. Matokeo na hatua zinazofuata ____________________

## **9.** Kagua na usasishe Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

a. Tarehe za kukagua na kusasisha tena:

b. Tarehe za kubadilisha timu, malengo, mpango wa utendakazi au bajeti ya mpango wa TNC au IPLC:

### Mambo ya Kuzingatia katika Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

2. Je, IPLC na TNC ziko tayari kufanya mazungumzo na kushughulikia mashaka?
3. Je, IPLC na TNC wako tayari kushughulikia athari mbaya haraka na kwa haki?
4. Je, IPLC na TNC wako tayari kuzingatia mchakato wa utatuzi wa mgogoro hadi pale ambapo wahusika wataafikiana kuwa mzozo umetatuliwa kikamilifu?
5. Je, TNC inakabiliwa na hatari zipi au inanufaika vipi kwa kushiriki katika mchakato wa utatuzi wa mgogoro wa IPLC? Kutumia taratibu za IPLC kunaashiria uzingatiaji wa juu zaidi wa sera ya IPLC ya kufanya uamuzi wa kibinafsi, hata hivyo TNC inapaswa tu kuzingatia utaratibu wa utatuzi wa mzozo ikiwa ina imani nao.
6. Je, IPLC na TNC wanatumia vipi mchakato wa utatuzi wa mgogoro kuimarisha hali ya kuendelea kujifunza, kuaminiana na usawa katika ushirikiano?
7. Mchakato wa utatuzi wa mgogoro unapotumika, IPLC na TNC wanaweza kuuboresha vipi? Taratibu zinazoweza kutumika ni pamoja na ukaguzi wa kindani au wa nje, maoni kutoka kwa washiriki au semina ya baada ya mpango.

PDF hii imetolewa hasa kwa madhumuni ya kuchapisha au kutumiwa nje ya mtandao. Fomu hii haiwezi kujazwa kidigitali isipokuwa kama imepakuliwa na kufunguliwa katika programu ya PDF kama vile Adobe PDF Reader au Kihakiki (Mac OS). Kwa bahati mbaya, maandishi yaliyoandikwa kwenye fomu hii **hayatahifadhiwa** ukitumia kivinjari kama vile Chrome, Safari au Internet Explorer.



## Moduli ya 4:
# Utekelezaji

Katika moduli hii:

Jifunze jinsi ya kutathmini miradi ambayo tayari inaendelea na upitie moduli za awali

Thibitisha Upya Makubaliano ya Idhini na mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

Amua jinsi ya kuendelea kutumia Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi Fuatilia

jinsi utekelezaji unavyoendelea

**Tafiti za Wenland:**

4A. Utekelezaji

## Utangulizi

Moduli ya Utekelezaji inaelezea jinsi ya kujumuisha Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi katika shughuli za kila siku za mradi, mkakati au mpango wa sera. Baada ya wafanyikazi wa TNC na IPLC kukamilisha mchakato wa kushirikiana na kufikia makubaliano kuhusu jinsi ya kufanya kazi pamoja, moduli hii itakuwa muhimu, hasa kwa mahusiano mapya ya IPLC na katika mipango inayoongozwa na TNC. Wafanyakazi wanapaswa kukagua Moduli ya Mafunzo na Majadiliano ya Mapema, FPIC na Moduli ya Utatuzi wa Mizozo.

## Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi

Utangulizi unahusisha mjadala kuhusu Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zinazotumika katika kushirikiana na IPLC. Tano ni muhimu sana katika utekelezaji:

### Utekelezaji wa Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi

**Uhuru wa Kuchagua na Kujiamulia Mwenyewe:**
Haki ya wenyeji ya kujiamulia wenyewe inapaswa kudumishwa kila wakati. Sharti iendelee kuzingatiwa kuanzia hatua ya kwanza hadi hatua ya utekelezaji.

**Uamuzi Unaofaa:**
IPLC huongoza katika kutoa maelezo ya kiikolojia na kitamaduni. Ili kuunga mkono uamuzi wao, huenda wakaomba usaidizi wa ziada wa kisayansi, kisheria, kisera, au maelezo mengine.

**Usawa na Uhusishaji**
Ushirikiano wa kweli na IPLC unamaanisha kuendelea kutathmini na kushughulikia masuala muhimu ya ushirikiano, kusaidia uongozi wa IPLC katika maamuzi kuhusu ardhi na rasilimali zao, na kuhakikisha ujumuishaji wa vikundi ambavyo huenda vimetengwa.

**Uwajibikaji:**
Uwajibikaji unahitaji mawasiliano mazuri, ndoto ya pamoja, ukaguzi wa mara kwa mara kuhusiana na utekelezaji wa mipango iliyokubaliwa, na kufanya marekebisho kama inavyohitajika.

**Nia Njema:**
Mipango inayotekelezwa kwa uaminifu, uadilifu na kwa kujitolea huimarisha kanuni nyingine zote. Hii ni mojawapo ya nguzo muhimu zaidi katika kupata matokeo ya kudumu kwa watu na katika mazingira.

## Mwongozo

### Hatua ya Kwanza: Sasisha na Uongeze Mipango

Wafanyakazi wa TNC wanapaswa kuwa na nyenzo za kurejelea TNC na IPLC wanapoingia katika hatua ya utekelezaji. Mchakato wenyewe ni rahisi: hatua ya kwanza ni kurejelea moduli za Mafunzo na Majadiliano ya Mwanzo, FPIC na Utatuzi wa Mgogoro.

#### Kwa Timu zilizopitia Moduli za Awali za Mwongozo huu:

Ikiwa timu zimeunda Mpango wa Majadiliano na Mpango wa Ushauri kwa kutumia Mwongozo huu, mipango hiyo inapaswa kukaguliwa wakati wa utekelezaji. Huenda ikawa dhahiri kuwa michakato au masharti fulani inafaa zaidi kuliko mengine. Timu zinapaswa kuzingatia utendakazi unaohimiza majadiliano na ushirikiano zaidi, na kujikita katika utendakazi huo.

Katika hatua hii, maudhui ya mpango yanapaswa kukaguliwa upya ili kuhakikisha kuwa bado yanazingatia Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi. Endapo kuna michakato mingine iliyotumika, kama vile Tathmini ya Athari kwa Haki za Binadamu, inapaswa pia kukaguliwa. Vipaumbele vilivyotambuliwa katika Tathmini ya Haki za Binadamu huenda vikahitaji kuzingatiwa zaidi utekelezaji unapoendelea.

Kwa mfano, hebu fikiria kuhusu mradi wa utunzaji unaofadhiliwa kwa kiasi fulani na shirika la wageni kutoka nchi za nje. Katika majadiliano ya mashauriano, jamii inatambua athari mbaya inayoweza kutokea — usimilishaji wa tamaduni za wenyeji kutokana na idadi kubwa ya watalii na maendeleo ya miundombinu ya kitalii. Katika utekelezaji, timu zinapaswa kuzuia athari hiyo kupitia hatua kama vile kuweka masharti katika idadi ya wageni wanaoruhusiwa kila siku, kujenga barabara na vituo vinavyowazuia watalii kuingia vijijini, na kushirikiana na serikali za mitaa ili kudhibiti ukuaji wa utalii.

Ukaguzi wa Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro pamoja na IPLC pia ni muhimu, kama inavyopendekezwa katika hatua ya 3 ya moduli hio, "Endelea Kurejelea na Kutekeleza Mpango."

### Kwa Timu zilizo katika Hatua ya Utekelezaji na Hazijapitia Moduli za Awali za Mwongozo huu:

Timu za TNC zinaweza kurejelea Mwongozo huu kwa mara ya kwanza wakati tayari katika hatua ya utekelezaji. Timu zinaweza kukagua moduli za awali na kutathmini kwa makini jinsi mapendekezo kuhusu makubaliano, maelewano na uimarishaji wa uhusiano yanaweza kujumuishwa.

Sharti timu itumie hatua za FPIC kwenda mbele (na ikiwezekana kwa kurejelea matukio ya awali) na ishirikiane na IPLC katika kuunda Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro. Timu inapaswa pia kujaribu kubashiri athari zisizotarajiwa. Hasa kwa mikakati isiyojumuishwa katika Mfumo wa IPLC wa Ajenda ya Majadiliano Yanayoshirikiwa, ni vyema kukagua Moduli ya Mafunzo na Majadilano ya Mwanzo, ili kuhakikisha uelewa mzuri wa athari zinazoweza kutokea.

### Haki za Binadamu Zinazohusishwa na Awamu ya "Chukua Hatua" kwenye CbD 2.0

Pamoja na kurejelea tena mwongozo na nyenzo za moduli za awali, maswali yafuatayo kuhusu haki za binadamu yanayohusiana na Conservation by Design 2.0, Awamu ya 4: Chukua Hatua,[1] yanaweza kusaidia katika awamu ya utekelezaji:

**Je, hatua zipi zinahitaji kuchukuliwa? (CbD "Rasimu ya Makubaliano")**

**Vidokezo**

Wakati wa utekelezaji, masuala mapya huenda yakaibuka baada ya ukaguzi wa mipango na michakato ya kujihusisha, mashauriano na utatuzi wa mgogoro.

**Je, majukumu ya kila mhusika ni yepi? (CbD "Rasimu ya Makubaliano")**

**Vidokezo**

Utekelezaji huenda ukahitaji michakato mipya ya kushauriana na kufanya maamuzi. Uamuzi wa awali uliotolewa na wasimamizi wakuu kuhusu kuidhinisha mchakato wa utekelezaji huenda ukafuatiwa na uamuzi wa muda mfupi unaopaswa kujumuisha IPLC endapo

wataamua kushiriki (rejelea Hatua ya Pili katika moduli hii). Uamuzi wa muda mfupi huenda usiwe rasmi au unaweza kukabidhiwa viongozi wa kieneo.

Kadri mpango unavyozidi kuendelea na kubadilika, uthibitishaji wa ziada wa idhini huenda ukahitajika ili kutimiza matakwa ya FPIC. Mchakato na Mpango wa Ushauri wa FPIC unapaswa kukaguliwa ili kuhakikisha athari zote zinazoweza kutokea zinashughulikiwa utekelezaji ukiendelea.

**Je, majukumu na ratiba ya mpango ni zipi? ("Rasimu ya Mpango wa Kazi" ya CbD)**

**Nyenzo**

Ikiwa wafanyakazi wanaunda mpango kamili wa kazi kwa ajili ya mradi wao, Kituo cha Ushirikiano wa Uhifadhi hutoa mwongozo kuhusu upangaji wa kazi, ikijumuisha kiolezo cha jumla wa mpango wa kazi. Kanuni za Usawa na Uhusishaji ni muhimu katika kuhakikisha ushirikiano wa kudumu katika awamu hii.

**Je, uboreshaji upi unahitajika? (Mchakato wa CbD wa "Kutambua Maboresho Yanayoweza Kufanywa")**

**Vidokezo**

Kuimarisha na kudumisha uwezo wa IPLC ni muhimu katika juhudi za uhifadhi wa muda mrefu. Huenda IPLC wakahitaji utaalamu au usaidizi wa kisayansi, kisheria, usimamizi wa kifedha, sera au usaidizi mwingine wakati wowote.

Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu tamaduni, mbinu shirikishi na stadi nyingine ni muhimu katika kudumisha haki na kukuza ushirikiano na IPLC. Maelezo zaidi yanapatikana kwenye Moduli ya Mafunzo na Majadiliano ya Mwanzo, na "Yaliyomo kwenye sehemu ya Ujuzi Unaohitajika" katika Moduli ya FPIC.

Timu inapaswa kuzingatia kigezo cha kukuza uwezo wa TNC na IPLC wakati wa kukadiria bajeti na idadi ya wafanyakazi.

**Nyenzo**

Huduma ya Learning Network on Capacity Development "inalenga kukuza na kuwezesha ushiriki wa masomo, ukuzaji wa uwezo na utekelezaji wa mabadiliko ya kuboresha utendakazi katika viwango vya kimataifa, kieneo na kimkoa." Wanaoongoza ni pamoja na FAO na UNDP.

Huduma ya Network for Strong Voice, Choice and Action (VCA Network) kwenye intraneti ya CONNECT ya TNC inatoa fursa ya kushirikiana na kujifunza kutoka kwa wenzako.

**Je, nyenzo zipi zinahitajika? ("Rasimu ya Bajeti" ya CbD)**

**Vidokezo**

TNC inapaswa kufidia IPLC kwa juhudi zao na muda waliotenga katika mpango.

Hii inaweza kujumuisha muda wa kuhudhuria mikutano, kusafiri, huduma za tafsiri na gharama nyingine husika. Usawa katika kushiriki unaweza kumaanisha kufanya mikutano ya ziada ya wanawake au vikundi vingine vya kijamii.

Ikiwa mradi haujafadhiliwa kikamilifu, TNC na IPLC zinaweza kuamua kushirikiana katika utekelezaji wa kiawamu — mbinu ya Mpango Mbadala. Mradi ukisitishwa au ukisimamishwa kutokana na ukosefu wa fedha, TNC na IPLC wanapaswa kukubaliana kuhusu matarajio na mipango ya dharura, pamoja na hali zisizotarajiwa.

**Nyenzo**

Shirika la Partners for Dignity & Rights lina ukurasa wenye maelezo na nyenzo kuhusu bajeti za kufadhili utekelezaji wa haki za binadamu.

**Je, mpango utafuatilia vipi? (CbD "Ufuatiliaji")**

Angalia Hatua ya 3 katika moduli hii hapa chini, pamoja na Moduli ya Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho.

**Je, mpango utakamilika wakati fulani, na ukikamilika, taratibu za kukamilisha au kukabidhi mradi kwa wahusika wengine ni zipi?**

Taratibu za kukamilisha au kukabidhi mradi kwa wahusika wengine zinapaswa kujadiliwa kabla ya wakati wa mpito kuwadia. Taratibu hizi zinapaswa kuendelea kudumisha Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zilizobainishwa katika Mwongozo huu, kwa kuzingatia uwezo na vipaumbele vya IPLC.

Timu zinapaswa kuzingatia kila swali hapa juu na kubaini ikiwa mipango yao ya makubaliano na mashauriano yanakithi mahitaji ya kuendelea ushirikiano. Ikiwa haitimizi masharti, michakato na mipango sharti irekebishwe ipasavyo.

## Hatua ya Pili: Rejelea Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi, na Makubaliano ya Idhini

Mara kwa mara, timu za TNC zinapaswa kukagua uzingatiaji wao wa Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi. TNC na IPLC wanapaswa pia kuendelea kukagua Makubaliano ya Idhini, ili kuhakikisha kuwa sheria na masharti ya idhini bado yanatumika. Kimsingi, ukaguzi huu unapaswa kufanywa wakati wowote kuna: 1) uamuzi muhimu; 2) mabadiliko ya wafanyakazi wa TNC au IPLC; au 3) awamu mpya katika mpango.




Muundo, hati na mara ambazo ukaguzi umefanyika zinapaswa kufuata sheria na masharti ya Makubaliano ya Idhini.

Huu ni mchakato endelevu na wala sio tukio la wakati mmoja. Katika mpango wote, taratibu nyingi muhimu, kubwa na ndogo, hutoa majukumu kwa TNC au IPLC. **Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi** zinahitaji IPLC kuwajibikia majukumu hayo wanapoimarisha lengo la kujiamulia wenyewe.

Katika utekelezaji, timu ya TNC inaweza kuchukulia baadhi ya maamuzi kuwa ya kawaida, pengine kwa sababu halali, na huenda kukawa na uwezekano wa kupuuza maamuzi hayo kwa sababu ya kukosa muda wa kutosha au ukosefu wa fedha. Lakini kuzingatia **Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi** kunaweza kuchukua muda zaidi ili kufanya uamuzi unaofaa, mchakato thabiti wa FPIC na ushirikiano unaozingatia usawa na uhusishaji. Kutenga muda na rasilimali katika juhudi hii hakupaswi kuchukuliwa kama mzigo, bali jitihada za kuimarisha uhusiano wa muda mrefu na matokeo bora kwa watu na mazingira.

## Hatua ya Tatu: Fuatilia Athari Muhimu

Ufuatiliaji, mafunzo endelevu, urekebishaji, utambuzi na utatuzi wa mizozo ni muhimu katika kutimiza Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi na kudumisha uhusiano thabiti na IPLC. Ufuatiliaji unapaswa kuwa kigezo kikuu katika matokeo ya Tathmini ya Athari kwa Haki za Binadamu au mashaka mengine yaliyobainishwa kuwa muhimu au yanayohitaji kushughulikiwa. Soma Hatua ya 3 katika Moduli ya FPIC na Hatua ya 3 katika Moduli ya Utatuzi wa Mgogoro. Suala hili pia ni muhimu katika Moduli ya Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho. Ufuatiliaji haupaswi kuchukuliwa kuwa mchakato unaotamatisha mpango. Unapaswa kujumuishwa katika mchakato mzima wa utekelezaji.

### 4A. Utekelezaji wa Utafiti wa Wenland

Mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi unaendelea. FrostLock itafanya majaribio ya utunzaji katika sehemu 25 za ardhi zenye udongo jalidi upande mwa kaskazini. Mpango huo ni pamoja na ufadhili wa Kamati za Usimamizi wa Mazingira ili kufuatilia usafi wa maji na athari nyingine zinazoweza kutokea katika miji iliyo karibu na maeneo ya majaribio, ambayo nyingi yazo ni miji ya Wen.

Tazama Utafiti

## Orodha ya kukagulia Utekelezaji

### Hatua ya Kwanza: Sasisha na Uongeze Mipango

☐ Kwa timu za TNC ambazo zimepitia moduli za awali: Sasisha Mipango ya Majadiliano, Mashauriano na Utatuzi wa Mgogoro ili kujumuisha maamuzi, majukumu na michakato mpya ya mashauriano

☐ Kwa timu za utekelezaji za TNC ambazo zimepitia moduli za awali:

- Kagua Moduli ya Mafunzo na Majadiliano ya Mwanzo ili kutambua athari zinazoweza kutokea
- Tekeleza FPIC kuendelea mbele (na ikiwezekana, kwa kurejelea matukio ya awali), kama ilivyoelezwa kwenye Moduli ya Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema, na Baada ya kuelewa Hiari
- Unda Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

☐ Jadiliana na IPLC kuhusu majukumu, muda wa utekelezaji na bajeti ya mpango

☐ Shirikiana kuunda mipango ya muda mfupi na ya muda mrefu ili kuimarisha uwezo wa IPLC na TNC na kuwa na wafanyakazi wa kutosha

### Hatua ya Pili: Rejelea Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi, na Makubaliano ya Idhini

☐ Fanya mikutano, mafunzo na mashauriano ya ziada wakati wa mchakato mzima wa utekelezaji, kulingana na Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi na Makubaliano ya Idhini, kuhakikisha mahitaji yanatathminiwa na yanaendelea kujumuishwa

### Hatua ya Tatu: Fuatilia Athari Muhimu

☐ Katika mchakato mzima wa utekelezaji, fuatilia athari muhimu zilizobainishwa kwenye Tathmini ya Athari kwa Haki za Binadamu au tathmini nyingine wakati wa mchakato wa FPIC (soma Moduli ya FPIC na Moduli ya Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho)

## Hati za Kuhifadhi

**Angalia Moduli ya Hati ili upate maelezo zaidi kuhusu hati zinazohitajika**

- [ ] Kwa timu za TNC ambazo zimepitia moduli za awali: Mipango ya Majadiliano, Mashauriano na Utatuzi wa Mgogoro iliyosasishwa, ikijumuisha:

  - Vigezo vinavyopaswa kushughulikiwa katika utekelezaji
  - Wajibu na majukumu
  - Michakato ya mashauriano na uamuzi wakati wa utekelezaji
  - Majukumu na ratiba
  - Bajeti
  - Kanuni kuhusu ufuatiliaji na kukuza uwezo

- [ ] Kwa timu za utekelezaji ambazo hazijapitia moduli za awali:

  - Maelezo kuhusu tathmini, wanaoathirika au athari zozote zilizotambuliwa zinazoweza kutokea, kwa mujibu wa Moduli ya Mafunzo na Majadiliano ya Mwanzo
  - Mpango wa kutekeleza hatua za FPIC kuendelea mbele (na ikiwezekana, kwa kurejelea matukio ya awali),
  - Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

- [ ] Maelezo kuhusu mikutano, majadiliano na uamuzi wa kukagua upya na kujumuisha Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi na Makubaliano ya Idhini katika mchakato mzima wa utekelezaji, kwa mfano, michakato ya kujifunza, mafunzo, mashauriano ya ziada

- [ ] Maelezo kuhusu michakato ya ufuatiliaji na matokeo, kulingana na masuala yaliyobainishwa kwenye Tathmini ya Athari kwa Haki za Binadamu au tathmini nyingine zinazotekelezwa wakati wa mchakato wa FPIC (Rejelea Moduli ya FPIC na Moduli ya Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho)

## Maelezo

[1] The Nature Conservancy (2016). Mwongozo wa Conservation by Design 2.0 {Toleo la 1.0, Machi 2016}: https://www.conservationgateway.org/ConservationPlanning/cbd/Documents/CbD2.0_Guidance%20Doc_Version%201.pdf. Angalia kurasa za 101-103.




# Utekelezaji

## 4A. Utafiti wa Wenland:

© Mark Godfrey/TNC

**Mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi unaendelea. FrostLock itafanya majaribio ya utunzaji katika sehemu 25 za ardhi zenye udongo jalidi upande mwa kaskazini. Mpango unajumuisha utoaji wa ufadhili kwa Kamati za Usimamizi wa Mazingira ili ziweze kufuatilia usafi wa maji na athari nyingine zinazoweza kutokea katika miji iliyo karibu na maeneo ya majaribio, ambayo nyingi yazo ni miji ya Wen. Kwa kushirikiana na Wen, kipande cha ardhi cha ekari 800,000 kisichokuwa na makazi ya watu kimetengwa kuwa Eneo la Usimamizi wa Uhifadhi. TNC itasimamia eneo hilo kwa miaka mitano ya kwanza, kisha itakabidhi usimamizi kwa shirika mpya linalofadhiliwa na Wen baada ya kipindi hicho kukamilika, au wakati shirika hilo jipya litakapokuwa tayari.**

Tathmini ya Jinsia ilifanywa wakati wa mashauriano. Watu wote — makundi ya wanawake ya Wen pamoja na Mabaraza ya Wen — walikubaliana kuwa hadhi ya wanawake katika jamii ya Wen iko chini, hasa katika kuhusishwa kufanya uamuzi.

Mradi wa FrostLock unahitaji ushirikiano mkubwa na jamii za Wen, na tathmini ya Jinsia ilipendekeza kuwa utekelezaji unapaswa kushughulikia suala la usawa wa kijinsia, na kwa namna fulani, suala la taasubi ya kijinsia, linalohusiana na usawa katika utoaji wa rasilimali na majukumu kati ya wanaume na wanawake. (Ili upate maelezo zaidi kuhusu Masuala ya Jinsia rejelea Mwongozo wa TNC wa Kujumuisha Usawa wa Kijinsia katika Uhifadhi.)

Wanawake wa Wen walipendekeza kuwa uanachama wa Kamati ya Usimamizi wa Mazingira uwe tofauti na Mabaraza ya Wen. Walielezea kuhusu kunyimwa uwakilishi katika maswala ya umma, ikijumuisha hali ambapo waliruhusiwa kushiriki lakini wakakabiliwa na upinzano mkubwa kutoka kwa wanaume kupitia upigaji kura kwenye Mabaraza ya Wen. Juhudi zao zingine za kupata nafasi za uongozi zimepingwa vikali na kukashifiwa na wanaume.

Mabaraza ya Wen zimebuni utaratibu utakaotumiwa na TNC kusimamia Kamati za Usimamizi wa Mazingira kwa kutoa usaidizi wa kiufundi na kuwachagua wajumbe kati ya walioteuliwa na wanajamii. Kikundi cha wanawake wa Wen, cha Wenza, kinasisitiza kuwa sheria ya uwakilishi sawa wa kijinsia inajumuishwe, lakini pendekezo hilo linakataliwa na Mabaraza ya Wen.

| Kwa mfano | *Mawazo na Mwongozo* |
| --- | --- |
| **1**<br>**Kwenye Eneo la Usimamizi wa Uhifadhi sehemu kadhaa zimetengwa kwa ajili ya kufanyiwa majaribio. FrostLock inaandaa utaratibu wa kuripoti utakaotumiwa na TNC kufuatilia sehemu zitakazofanyiwa majaribio, kisha matokeo yatashirikiwa tu na FrostLock. Inadai kuwa sehemu hizi haziwaathiri wanajamii wa Wen na kwamba hawahitaji kuhusishwa. *Je, TNC inapaswa kukubali?*** | *Hapana. Watu wa Wen wanadai kwamba wao ndio wenyeji na wanamiliki eneo nzima la Wen tangu jadi. Hata wanajamii wasiposisitiza kuhusu msimamo wao, TNC haipaswi kupuuza hili. Kwani, hatua ya TNC ya kuichukulia eneo hilo kuwa si sehemu ya Wen inayoonyesha kuwa mashaka ya wenyeji ya kujiamulia wenyewe hayazingatiwa.* |
| **2**<br>**Uanachama kwenye Kamati za Kieneo za Usimamizi wa Mazingira unakuwa kiini cha migogoro. Mabaraza hayajaridhika kufuatia kusalimisha mamlaka yao ya kusimamia bajeti za Kamati, hasa katika ukodishaji na ununuzi. Wanaanza kujaribu kuwa na ushawishi kwenye Kamati kwa kutumia mbinu za awali. Kabla ya uteuzi kufanywa, mabaraza pia yanaomba TNC ishiriki nao orodha ya walioteuliwa, japo hii hairuhusiwi kwenye utaratibu husika. Mabaraza yanasema kuwa yanafahamu jamii vyema hivyo yanaweza kuteua waliohitimu zaidi. *Je, TNC inapaswa kukubali ombi la Mabaraza?*** | *Kanuni nyingi zinahitaji kuzingatiwa katika hali hii. TNC sharti ijaribu kuzizingatia kwa kushirikiana na Wen, na pia kuwajibikia vitendo na kanuni zetu. Ni muhimu kuheshimu Uamuzi wa Kibinafsi kama ilivyobainishwa na Mabaraza ya Wen, japo mchakato uliobuniwa, kwa kuidhinishwa na Mabaraza, una mahitaji yake ya Usawa na Uhusishaji. TNC ina jukumu la kuonyesha Nia Njema kwa jamii yote ya Wen. Kushiriki na Mabaraza orodha ya walioteuliwa kunaweza kuwa jambo nzuri ikiwa inaruhusiwa kwenye utaratibu na itawezesha TNC kupata ushauri na maarifa kutoka kwa Mabaraza.*<br>*Lakini TNC haipaswi kukiuka utaratibu. Iwapo kuna mgogoro usioweza kutatuliwa, TNC inapaswa kupendekeza kuwa mchakato utathminiwe upya kupitia mchakato wa uwazi na kamili wa FPIC.* |
| **3**<br>**TNC inapokagua orodha ya walioteuliwa, wanaume wanaonekana kuhitimu zaidi kulingana na uzoefu wa juu unaotokana na uongozi wao katika jamii na ufahamu wao wa eneo lao na wanyamapori, unaotokana na uzoefu wa uwindaji, ambao ni shughuli inayotekelezwa na wanaume pekee. *Je, TNC inaweza kuwachagua wanawake walioteuliwa licha ya kuwa na uzoefu wa chini?*** | *Ndiyo. Usawa na Uhusishaji ni kanuni za msingi katika utendakazi wa TNC, na uteuzi wa Kamati za Usimamizi wa Mazingira unaweza kuonekana katika muktadha wa makubaliano ya Mabaraza ya Wen na washikadau wengine kuwa usioshugulikia usawa wa kijinsia na kwamba mpango huo unapaswa kuzingatia masuala ya jinsia inapowezekana.*<br>*Pia, uzoefu wa uongozi na uwindaji zimejikiza katika kigezo cha jinsia katika jamii ya Wen. Kutegemea vigezo hivi kutaegemeza upendeleo wa kijinsia katika mfumo mpya, Kamati za Usimamizi wa Mazingira, hivyo kuendeleza na kupuuza zaidi mashaka kuhusu usawa wa kijinsia. Mawasiliano wazi kuhusu uteuzi wa wanawake ni fursa ya kuhimiza kuaminiana na kujifunza pamoja kwa TNC na Wen.* |

| **Kwa mfano** | *Mawazo na Mwongozo* |
|---|---|
| **4**<br>**Wanawake kutoka jamii kadhaa wanawaeleza wafanyakazi wa TNC kwamba hawatajiteua kuwa wanachama wa Kamati isipokuwa wanachama wengine wa kamati wawe wanawake, kwa sababu wanaamini wanaume wote watapiga kura kwa njia sawa kwamba ushiriki wao katika Kamati utapuuzwa. *Je, TNC inapaswa kufanya wanawake kuwa wengi Zaidi katika Kamati za Usimamizi wa Mazingira ili kuwahimiza kushiriki?*** | *Hii ni hali tata. Mabaraza ya Wen yalikubali kuwa kuna tatizo la usawa wa kijinsia na kwamba mpango huo unapaswa kushughulikia masuala ya jinsia, lakini pia walikataa wazo la kutenga idadi mahususi ya nafasi kwa watu wa jinsia moja. TNC ikikubali kutenga idadi mahususi ya nafasi kwa watu wa jinsia moja, itakinzana na uzingatiaji wetu wa mamlaka ya IPLC. Hata hivyo, mabaraza ya wanaume pekee ndiyo yaliyopiga kura kupinga pendekezo la uwakilishi wa kijinsia.*<br><br>*TNC inapaswa kuzuia kutokea kwa hali ya upande mmoja kushinda na upande mwingine kutoridhika, na badala yake kushauriana na mabaraza ili kupata suluhisho inayoshirikisha watu wote, kama vile kuweka sera za kuhimiza wanawake kushiriki au kujadili upya suala la uwakilishi wa kijinsia kwa kuzingatia malengo ya msingi.* |
| **5**<br>**Kamati za Usimamizi wa Mazingira zipo, na mojawapo ya majukumu yao ni, kutathmini malalamishi kuhusu athari kwa mazingira, kama vile uchafuzi wa maji, kisha kuyawasilisha kwa FrostLock na TNC. FrostLock inaweka huduma ya usaidizi ya simu. Mwaka mmoja baadaye, TNC inasikia kwamba FrostLock inatuma wawakilishi kuchunguza malalamishi ya wapiga simu moja kwa moja, na wakati mwingine inachukua hatua kama kuweka vichungi vya maji na kuwafidia wapigaji simu wakikubali kutia saini makubaliano ya kutofichua siri. *Je, TNC inapaswa kuchukua hatua gani, yoyote ile?*** | *TNC inapaswa kuchukua hatua. Ingawa TNC haihusiki moja kwa moja katika vitendo vya FrostLock, inahusika katika mradi kwa jumla.*<br><br>*Tunapaswa kutumia uwezo wetu kuzuia utekelezaji wowote unaokwenda kinyume na Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi. Makubaliano ya kutofichua siri muktadha huu ni yanahusishwa na ukiukaji wa haki za binadamu kwa sababu huenda yakasababisha unyanyasaji, na kushurutisha IPLCs watie saini kwenye makubaliano ya kutofichua siri ili kupata faida fulani ni kinyume na kanuni za Uwajibikaji na Uwazi.*<br><br>*Lakini hata ikiwa FrostLock imeondoa kanuni hiyo, kujihusisha moja kwa moja na wanaopiga simu kupitia huduma ya usaidizi ni kutoheshimu mamlaka ya Kamati za Usimamizi wa Mazingira. Kuhusika moja kwa moja pia huenda kukaathiri ukusanyaji na ufuatiliaji wa data hivyo kusababisha upotoshaji au kutojulikana kwa tatizo kubwa. Ili kuwezesha IPLC wajiamulie wenyewe, TNC inapaswa kusaidia Kamati katika kupinga hatua ya FrostLock ya kujihusisha moja kwa moja na wanaopiga simu kupitia huduma ya usaidizi na kupendekeza njia mbadala. Rejelea Moduli ya Utatuzi wa Mgogoro ili upate maelezo zaidi.* |



Moduli ya 5:

# Kuandika hati

Katika moduli hii:

Jifunze vigezo vitano muhimu vya kuandika hati vizuri

Tambua maudhui unayohitaji kujumuisha kwenye faili ya hati

Teua muundo wa hati unaoweza kufikiwa na unaoafiki

**Utafiti wa Wenland:**

5A. Utatuzi wa Mgogoro

## Utangulizi

**Moduli ya Hati inatoa muktadha, madhumuni na viwango vya kuandika hati za mradi. Mapendekezo maalum yametolewa katika sehemu ya "Hati za Kuhifadhi" katika kila moduli.**

Kihistoria, kutomakinikia rekodi kunahusishwa na utepetevu wa kuhifadhi faili na nia ya kuficha ukiukaji wa haki za binadamu. Hati isiyozingatia masilahi ya wengine—rekodi inayoonyesha tu uzoefu, mitazamo, masilahi na lugha ya mtunza rekodi—hutumika kushurutisha, kukandamiza na kunyamazisha wenyeji

Rekodi inayostahiki sio tu kamili na sahihi bali pia iliyoundwa na kudumishwa kupitia ushirikiano wa TNC na IPLC. IPLC nyingi hutumia mawasiliano ya mdomo, kwa hivyo faili ya hati inayozingatia utamaduni inaweza kuwa katika miundo mingine kando na hati zilizoandikwa, ambayo huenda ikajumuisha rekodi za sauti, video za simu mahiri, picha zenye manukuu au mawasiliano ya barua pepe.




Hati zinaweza kuwa tofauti kwa IPLC na miradi mbalimbali.

Hata hivyo, sharti hati ziwe kamili na zizingatie mwongozo uliotolewa katika moduli hii. Kwa kuzingatia haki za binadamu, kuandika hati kwa uangalifu hutoa ithibati kwa TNC na IPLC kutathmini ikiwa utendakazi wao unazingatia Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi.

Mchakato jumuishi wa kuandika hati husaidia kudumisha mawasiliano, uhusiahji na kukuza uhusiano kwa kuhakikisha kuwa watu wote wanaelewa masuala yaliyoshughulikiwa, hatua zilizochukuliwa, na sheria na masharti ya makubaliano yoyote. Hati pia huwasaidia wafanyakazi wa TNC au wakaguzi wa nje kukagua kazi.

Kupeana hati kunaashiria makubaliano kuhusu mchakato na matokeo, uzoefu na utendakazi. Wahusika wanapokubaliana kuandika hati au kuweka kukumbuka kuhusu msimamo, tukio au makubaliano fulani, wanathibitisha mchakato na umuhimu wake—kuwasikiliza wengine na kusikilizwa.

## Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi

Utangulizi unahusisha ufafanuzi wa Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zinazotumika katika ushirikiano wa usawa. Tano ni muhimu sana katika utekelezaji:

### Kanuni na Sera Muhimu za Kulinda Maslahi Zinazotumika katika Kuandika hati

**Majadiliano na Awali na Uhusiano Shirikishi**
Kuwa na uzoefu sawa ni kigezo madhubuti kwa wahusika wote kujifunza, kuaminiana na kuimarisha ushirikiano.

**Uwajibikaji:**
Rekodi zilizohifadhiwa hutumika kama ithibati kwa wasimamizi na wahusika kuwajibikia matendo yao. Rekodi za awali zinatuwezesha kujifunza kutokana na matukio yaliyopita na kufanya maamuzi bora katika siku zijazo.

**Usawa:**
Hati inajumuisha faili zinazohusu makubaliano ya mgao wa faida, hatua za usawazishaji wa mamlaka na ufikiaji wa rasilimali. Mchakato wenyewe wa kuandika hati unapaswa kuzingatia kanuni ya Usawa kwa kufuata mifumo na sera za IPLC, pamoja na mbinu zinazopendelewa.

**Uhusishaji:**
Kuandika hati kunapaswa kujumuisha misimamo na mitazamo ya vitambulisho tofauti vya kijamii. Kuandika hati kunaweza kubainisha haja ya kushughulikia suala la ushiriki na huenda ukaboresha uhusishaji.

**Mashauriano Muhimu:**
Kuandika hati kwa njia inayofaa huhakikisha kuwa TNC na IPLC wana maelezo kamili kuhusu makubaliano pamoja na wahusika — hii ni sehemu muhimu ya mchakato thabiti unaoendelea wa mashauriano.

## Mwongozo

Kuandika hati kunapaswa kuanza katika hatua ya mwanzo na kuendelea katika hatua zote. Inapaswa kushughulikia mahitaji ya TNC na IPLC, na utayarishaji wake sharti uzingatie lugha, muundo, kiwango cha masomo, ufikiaji wa mtandao, na desturi na mapendeleo. Usaidizi wa kiufundi au ukuzaji wa uwezo unaweza kuhitajika ili kuhakikisha ushiriki wa IPLC, na wafanyakazi wa TNC huenda wakahitaji kuboresha ufahamu wao wa aina za hati zinazopendelewa na IPLC.

Timu zinapaswa kulenga kuwa na hati kamili ya michakato na matokeo, ili kuhimiza mawasiliano, uwajibikaji na kuaminiana. Taratibu za kuandika hati ni tofauti katika miradi mbalimbali, lakini sharti timu zitimize viwango vilivyoelezwa hapa chini: thabiti, ukamilifu, ushirikishaji, uzingatiaji wa haki, na upatikanaji.

Timu zinapoanza mchakato wa kuandika hati zinapaswa kurejelea Tathmini ya Athari kwa Haki za Binadamu au masuala mengine yaliyotambuliwa kufikia sasa. Mambo muhimu na masuala nyeti yanayohitaji kushughulikiwa zaidi. Vigezo vitano muhimu vya kuandika hati ni:

### Vigezo Vitano muhimu vya Kuandika Hati

**Thabiti:**
Mara nyingi maelezo ya kina huwa bora. Ni vigumu kubashiri jinsi faili za hati zilizohifadhiwa zitakavyotumika baadaye, na maudhui yanayochukuliwa kuwa yasiyohitajika huenda yakaishia kuwa muhimu. Lakini kuandika kunapaswa kujumuishwa kwenye mfumo huu thabiti, kwa sababu faili yenye maelezo mengi mno huwa kubwa, yenye maudhui yasiyohitajika na yasiyo muhimu. Ili kushughulikia haya mawili, kagua mara kwa mara rekodi iliyohifadhiwa, kisha upange na ufupishe maudhui.

**Ukamilifu:**
Ni muhimu kuwa utaratibu unashughulikia moduli, hatua na michakato yote. Faili yenye maudhui kuhusu mashauriano ya FPIC lakini haina hati kuhusu mpango au utekelezaji wa awali si kamilifu.

**Ushirikiano na ushughulikiaji wa maadili:**
Kuandika hati ni mchakato jumuishi. IPLC wanapaswa kufanya uamuzi wao binafsi kuhusu maudhui yatakayojumuishwa, muundo wa rekodi, jinsi ya kutumiwa, kufikiwa na kuhifadhiwa. Hati inapaswa kushughulikia mahitaji na vipaumbele vya TNC na IPLC.

**Uzingatiaji wa haki:**

Kuandika sharti kuzingatie haki, sera na mchango wa IPLC, na hasa sharti

kuheshimu na kulinde haki za IPLC kuhusiana na ujuzi na hakimiliki.

**Ufikiaji:**
Faili za hati sharti ziweze kufikiwa na TNC na IPLC kwa urahisi. Ni muhimu pia kuruhusu umma au watu wengine kufikia maelezo, lakini sharti faragha ilindwe.

### Nyenzo Muhimu za Kujumuisha kwenye Faili za Hati

**Utafiti tangulizi:**
Utafiti tangulizi ulifanywa ili kutambua IPLC wote wanaoweza kuathiriwa (utafiti unaotegemea nyenzo zilizopo, mashauriano na wataalam, kuwasiliana na wanajamii) kama ilivyoelezwa katika Hatua ya Kwanza katika Moduli ya Mafunzo na majadiliano ya Mwanzo. Maelezo ya utafiti, nyenzo, maelezo ya mkutano na nakala za nyenzo zilizotolewa na wataalamu zinapaswa kujumuishwa.

**Mpango wa Kujihusisha:**
Mpango wa Kujihusisha kwa kila IPLC, na maelezo kuhusu jinsi mpango huo ulivyobuniwa na kushirikiwa. Rejelea Hatua ya Pili katika Moduli ya Mafunzo na Majadiliano ya Mwanzo.

**Maandalizi ya mashauriano:**
Maandalizi ya mashauriano, pamoja na ujuzi wa timu ya TNC, mahitaji ya FPIC na sheria zozote husika za nchi hiyo, kwa kuzingatia kuwa TNC inafuata mchakato wa FPIC ambao huenda ukapita mipaka ya mfumo wa kisheria. Angalia Hatua ya Kwanza katika Moduli ya FPIC.

**Mpango wa Ushauri:**
Mpango wa Ushauri, ikijumuisha nyenzo zinazofafanua kuhusu:

1. jinsi mpango ulivyoundwa kwa ushirikiano na kisha kushirikiwa
2. vikao, mikutano na hafla zilizofanyika, na nyenzo husika
3. muhtasari kuhusu jinsi maelezo yatakavyoshirikiwa, ikiwemo lugha na miundo inayopendelewa. Angalia Hatua ya Kwanza katika Moduli ya FPIC.

**Makubaliano ya Idhini:**
Makubaliano ya Idhini (ikiruhusiwa) yanayoonyesha utaratibu ulioafikiwa, mashaka na mapendekezo ya IPLC, waliohudhuria mikutano, na mpango wa kukagua makubaliano mara kwa mara, pamoja na maelezo ya mkutano, kama ilivyoelezwa katika hatua ya Tatu katika Moduli ya FPIC.

**Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro:**
Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro unaofafanua utaratibu na masharti ya kutatua mizozo, na nyenzo zinazoelezea kuhusu: (a) jinsi mpango uliundwa kwa ushirikiano na IPLC; na (b) rekodi ya kila mzozo na jinsi ulivyotatuliwa. Rejea Hatua ya Kwanza katika Moduli ya Utatuzi wa Mgogoro.

**Mipango Iliyosasishwa ya Majadiliano na Mashauriano:**
Mipango Iliyosasishwa ya Majadiliano na Mashauriano utekelezaji unapoanza, kama ilivyofafanuliwa katika Hatua ya Kwanza katika Moduli ya Utekelezaji, hasa athari kwa haki za binadamu na mashaka muhimu yaliyotambuliwa wakati wa mashauriano, kama ilivyofafanuliwa kwenye Moduli ya FPIC.

****Timu ambazo tayari ziko katika hatua ya utekelezaji:**
Timu ambazo tayari ziko katika hatua ya utekelezaji zinapaswa kuzingatia kikamilifu utaratibu ulioelezwa hapa juu, ikiwemo:

- Maelezo kuhusu tathmini na wanaoathirika, kulingana na Moduli ya Mafunzo na Majadiliano ya Mapema
- Mpango wa kufuata hatua za FPIC kwenda mbele (na ikiwezekana, kwa kurejela matukio ya awali) kwa kuzingatia Moduli ya FPIC
- Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro kulingana na Moduli ya Utatuzi wa Mgogoro

**Ufuatiliaji wa Athari kwa Haki za Binadamu**
Ufuatiliaji wa Athari kwa Haki za Binadamu zikiwemo sera zilizobuniwa kwa kuzingatia Hatua ya Kwanza kwenye Moduli ya Kufuatilia, Kutathmini na Kurekebisha, ili kushughulikia masuala muhimu na athari kwa haki za binadamu. Shughuli zinazotekelezwa kwa kuzingatia Hatua ya Pili na ya Tatu ya Moduli ya Kufuatilia, Kutathmini na Kurekebisha zinapaswa kunakiliwa kikamilifu, ikijumuisha madokezo ya mikutano ya tathmini.

### Suala Muhimu: Muundo

Rekodi zinapaswa kuwa rahisi kuandaa, kushiriki na kuhifadhi kwa njia salama. Kukubaliana kuhusu hifadhidata ya kushiriki maelezo na IPLC (kwa mfano, folda ya Box) kunaweza kusaidia kuhifadhi faili zote mahali pamoja. Kwa matukio au maamuzi muhimu, maelezo yasiyo ya faragha yanapaswa kushirikiwa na IPLC wote, ili kuhimiza uwazi na uaminifu. Wafanyakazi wanapaswa kushirikiana na IPLC kutambua ni nani anayepaswa kushiriki maelezo haya na kwa njia gani.

Wafadhili wa kimataifa, serikali au wahusika wengine huenda wakawa na masharti maalum kuhusiana na hati, kama vile makubaliano, kumbukumbu za mkutano au orodha ya waliohudhuria iliyotiwa saini. Wakati mwingine, rekodi zinaweza kuhifadhiwa kwa njia bunifu zaidi, kama vile kutumia simu mahiri kunasa video ya mkutano au sherehe, kutumia rekodi ya sauti kama ithibati, picha zenye manukuu, ujumbe wa WhatsApp au mazungumzo ya sauti, ripoti iliyoandikwa, orodha zenye vitone, wimbo, au picha za mkutano au makubaliano. Sharti pawe na makubaliano na IPLC kuhusu muundo wa hati.

Kuandika kunapaswa kushughulikia mahitaji ya TNC na IPLC. TNC inaweza kuhisi kuwa maelezo fulani yanahitaji kunakiliwa, kwa mfano, ripoti ya mfadhili au kumbukumbu ya wanatimu. Endapo IPLC wanapendelea muundo tofauti, miundo yote miwili inaweza kutumika, mradi uwazi udumishwe, na toleo lililoandikwa halitashurutisha IPLC.

### Suala Muhimu: Kazi ya Ziada

Inahitaji jitihada kuunda faili kamili kwa madhumuni ya utendakazi na kushughulikia haki za binadamu, lakini shughuli hii inaweza kurahisishwa. Kwa mfano, Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro unaweza kuwa muhtasari mfupi wa chaguo zilizo katika Moduli ya Utatuzi wa Mgogoro, pamoja na masharti ya ziada kama inavyohitajika. Katika mradi mdogo, Makubaliano ya Idhini yanaweza kuwa muhtasari wa ukurasa mmoja

wa mchakato na sheria na masharti Madokezo ya mkutano wa mashauriano yanaweza kuwa picha pamoja na orodha ya wahusika na mambo na maamuzi muhimu yaliyofanywa.

Ikihitajika, wasimamizi wanapaswa kuongeza idadi ya wafanyakazi ili kutekeleza kazi zaidi, lakini utaratibu wa kuandika hati unaweza kuwamzuri na wa kina, mradi ibiniwe na kutekelezwa kwa ushirikiano na IPLC.

**Suala Muhimu: Usiri**

Uwazi ni muhimu katika kudumisha usawa na uaminifu kati ya TNC na IPLC. Lakini si rahisi kutumia kanuni hii kwa wahusika wengi. Ni muhimu kudumisha usiri katika hali fulani, kwa sababu wenyeji wana hakimilikikuhusiana na simulizi na desturi zao. Wanaweza kuamua kushiriki maelezo haya na TNC kama sehemu ya mchakato wa mashauriano, lakini TNC sharti iheshimu uamuzi wa IPLC wa kutoyashiriki. Kwa maelezo zaidi kuhusu haki za uvumbuzi wa mali ya IPLC, angalia Hatua ya Tatu ya Moduli ya Mafunzo na Majadiliano ya Mwanzo. Kanuni za usiri zinaweza kutekelezwa katika maelezo nyeti, kama vile mikakati ya kisiasa ya IPLC, usimamizi wa ndani, au maelezo kuhusu uwekaji mipaka.

Usiri huenda ukahitajika katika uhusiano na wahusika wa nje na kwenye IPLC. Ikiwa kuna mzozo kati ya kundi moja au makundi mengine au unaohusisha kundi linaloweza kuathirika kwa urahisi, kukusanya maelezo kunahitaji kuwa ya siri. Mambo yanapaswa kushughulikiwa kwa kutathmini Kanuni na Sera ya Kulinda Maslahi na mwongozo mara kwa mara katika Moduli za FPIC na Utekelezaji. Wanachama wa, Timu ya Kimataifa ya Wenyeji na Wanajamii Asilia, wa VCA Network na Mawakili pia wanawez kutoa ushauri.

**Suala Muhimu: Masuala ya Sheria**

Kawaidai mashirika hurekodi shughuli, maelewano, misimamo na maamuzi yanayoweza kutumiwa katika ukaguzi, majadiliano ya baadaye, au hata kesi katika hali zisizotarajiwa. Hati hii ni muhimu katika kulinda TNC kwa mujibu wa sheria. Wasimamizi wanapaswa kushauriana na Mawakili kama inavyohitajika katika sera na taratibu za TNC.

Katika kuzingatia Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi, kuandika kunapaswa kufanikisha mawasiliano na ushirikiano madhubuti, na wala sio kuendeleza maslahi binafsi. Moduli zilizoko katika Mwongozo huu na hati husika, zinapaswa kuendelea kutekelezwa. Kwa mfano, FPIC, haipatikani tu mara moja; inatathminiwa mara kwa mara kadri hali zinavyobadilika. Endapo IPLC wataomba marekebisho yatekelezwe, TNC haitasisitiza kwa kushikilia masharti ya makubaliano, lakini inapaswa kuchukulia ombi hili kuwa sehemu muhimu katika mchakato wa kuimarisha uhusiano. Wakati mwingine, IPLC wanaweza kuhitajika kusitisha au kukomesha uhusiano ambao IPLC wanachukulia kuwa hautimizi mahitaji yake tena.

### Nyenzo: Kuandika hati

**Video ya kitabu cha hadithi kinachohusu Mikakati Mwafaka ya Kitaifa nchini Australia**

Watu wa Warlpiri wa Jangwa la Tanami wamebadilisha toleo ya Kiingereza la mpango wa usimamizi wa Sehemu Asili Iliyohifadhiwa ya Tanami kuwa kitabu cha hadithi cha kidijitali: misururu ya video, rekodi za sauti na video za uhuishaji kwa lugha ya Kirlapiri. Tovuti ina nyenzo hizi pamoja na toleo la Kiingereza.

**Zingatia kwa Makini FPIC ua Kuandika hati**

Shirika la Equitable Origin na Roundtable on Sustainable Biomaterials lina mwongozo kuhusu ithibati inayokubalika ya michakato ya FPIC katika Ripoti ya Mradi ya, Kuwezesha FPIC Kupitia Viwango vya Hiari ya Julai 2018. Mfumo huu unadumisha mbinu bora za utunzaji wa raslimali, zilizobuniwa na wenjeyi. Ziliundwa ili kuwezesha uzalishaji wa nishati kwa njia inayofaa, lakini zinaweza kutumiwa katika uhifadhi. Kwa mfano, katika Mfumo wa Utaratibu wa Ufuatiliaji wa FPIC uliowasilishwa katika Kiambatisho cha 3 cha Ripoti ya Mradi, sehemu inayohusu Maadili ya FPIC (kurasa 101-103) inaweza kutumika kufafanua zaidi Hati za kuhifadhi za Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa katika Mwongozo huu.

### 5A. Hati ya Utafiti wa Wenland




Mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi unapoendelea, timu ya TNC inafanya ukaguzi wa rekodi kulingana na Mwongozo, kutathmini maelezo ambayo timu imekuwa ikikusanya wakati wote wa mchakato.

Tazama Utafiti

## Orodha ya kukagulia ya Kuandika hati

- [ ] Kuanzisha mbinu za kuandika hati zinazowezesha mawasiliano, uaminifu na uwajibikaji. Hati inapaswa kushughulikia mahitaji ya TNC na IPLC, sharti uzingatie lugha, muundo, kiwango cha masomo, ufikiaji wa mtandao, na desturi na mapendeleo.

- [ ] Rejelea upya Tathmini ya Athari kwa Haki za Binadamu au mashaka mengine tata yaliyotambuliwa wakati wa mashauriano, na kuyazingatia zaidi wakati wa kuandika hati

- [ ] Kuhakikisha kuwa hatua za kuandika hati zinazingatia na kulinda haki za IPLC za kupata taarifa na kumiliki hakimiliki, na zinajumuisha kanuni za usiri inapohitajika

- [ ] Katika kipindi chote cha mpango, kuhakikisha kuwa rekodi zinahifadhiwa mara kwa mara na kwa ukamilifu, kwa njia sahihi na inayoweza kudhibitiwa.

- [ ] Kuimarisha uwezo wa TNC na IPLC wa kuendesha ushirikiano na kuelewa mbinu za kuandika hati zinazolingana na desturi husika

## Hati za Kuhifadhi

**Nyenzo muhimu za kujumuisha kwenye faili ya hati (angalia hapa juu):**

- [ ] Utafiti tangulizikutambua IPLC wote wanaoweza kuathiriwa
- [ ] Mpango wa Kujihusisha kwa kila mshirika wa IPLC
- [ ] Maelezo ya maandalizi ya mashauriano
- [ ] Mpango wa Ushauri
- [ ] Makubaliano ya Idhini
- [ ] Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro
- [ ] Mipango Iliyosasishwa ya Kujihusha na Ushauri
- [ ] Kwa timu ziilizo katika hatua ya utekelezaji na hazijapitia moduli za awali, toleo lililorekebishwa, lililoboreshwa la lililo hapo juu, pamoja na:
    - Maelezo ya tathmini na athari zozote zinazoweza kutokea au watu walioathiriwa
    - Mpango wa kutekeleza hatua za FPIC kuendelea mbele, (na ikiwezekana kwa kurejelea matukio ya awali)
    - Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro
- [ ] Viashiria vya ufuatiliaji wa haki za binadamu, shughuli na maelezo




© Patrick Cavan

# Kuandika hati

## 5A. Utafiti wa Wenland:

**Mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi unapoendelea, timu ya TNC inafanya ukaguzi wa rekodi kulingana na Mwongozo, kutathmini maelezo ambayo timu imekuwa ikikusanya wakati wote wa mchakato. Faili ya hati inajumuisha:**

- Faili ya utafiti ikiwa ni pamoja na makala yaliyonakiliwa na kubandikwa, makala mengine ya masomo yaliyopakuliwa, maelezo ya wafanyakazi na barua pepe zenye hati zilizoambatishwa zilizotumwa na maprofesa wa Mafunzo ya Asili wa vyuo vikuu vya eneo husika.

- Barua pepe za utangulizi zilizoshirikiwa na wafanyikazi wa TNC, anwani ya mwanajamii wa Wen na wanachama wawili wa Baraza la Wen Camp, na madokezo yaliyoandikwa wakati wa mkutano na washiriki wa Baraza.

- Barua pepe zilizoshirikiwa na wanachama zaidi wa Baraza la Wen, wakipanga kuhusu TNC kufika mbele ya Baraza. Barua pepe ya awali ya TNC inayoeleza uelewa wa mfanyakazi kuhusu jinsi ya kushirikisha jamii na kuomba maoni kuhusu njia zilizopendekezwa za ushiriki. Majibu kadhaa (“ni mazuri!”) kuashirikia kuwa yameidhinishwa.

- Faili ya mashauriano, inayojumuisha: masula ya kushughulikia, vidokezo vya vinavyoonyesha tarehe za mikutano, masuala yaliyoangaziwa na maelezo mafupi kuhusu maafikiano; diski za hifadhi zenye video za vikao; nakala za kumbukumbu rasmi, maamuzi na mawasiliano na Baraza; nakala za baadhi ya ripoti mashauriano na wahusika wengine; nakala za mabango na nyenzo za matangazo kuhusu vikao vya mashauriano; nakala za ramani na matini yaliyotumika kwenye vikao vya mashauriano; rasimu na nakala iliyotekelezwa ya Makubaliano ya Mpango inaonyesha wazi idhini ya Wen; makala ya habari kuhusu mashauriano.

- Mpango wa kurasa tatu wa Utatuzi wa Mgogoro na barua pepe iliyotumwa na TNC kwa kikundi cha wanachama wa Baraza, ikisema, "Hili ndilo toleo la mwisho la mpango tuliojadili wakati wa kikao cha mashauriano mnamo Julai 21; tujulishe ikiwa una maoni au marekebisho yoyote na mnaombwa mshiriki na watu wengi katika jumuiya zenu.”

- Mawasiliano yanayohusiana na masuala ya uanachama wa Kamati za Usimamizi wa Mazingira.

| Kwa mfano | *Mawazo na Mwongozo* |
| --- | --- |
| **1**<br>**Hii ni timu mpya ya mradi, na wana hamu ya kujua ikiwa wametayarisha faili zote za hati zinazohitajika. *Ni sehemu gani inaweza kuboreshwa zaidi?*** | *Faili ya timu inaweza kuboreshwa, lakini inatosheleza na inonyesha juhudi za kuandika yanayoashiria uhusiano imara na Wen. Kwa miradi mingi ambapo IPLC ina uwezo mdogo wa kiufundi au usimamizi, faili inaweza kuwa ndogo na inayotegemea sana maelezo na memo za TNC zenye rekodi ya mazungumzo na makubaliano.*<br><br>*Hati chache zinazoweza kujumuishwa kwenye faili:*<br><br>• *Mpango wa Kujihusisha ulipaswa kuwa rasmi zaidi, lakini hatua hii si rahisi mwanzoni mwa ushirikiano.*<br>• *Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro ulipaswa kukubaliwa kwa uwazi zaidi: Timu ya TNC ilipaswa kuthibitisha kuwa mpango umesomwa, umeeleweka, umekubaliwa, na unafanyiwa hamisisho kwenye jamii.*<br>• *Licha ya faili ya mashauriano kuonekana kuwa thabiti, muhtasari wake huenda usitosheleze mahitaji ya mchakato huu changamano na wa kina.* |
| **2**<br>**rostLock imekuwa ikihifadhi rekodi za mradi na mashauriano. Katika hafla ya utiaji saini, FrostLock kwa ujasiri inatoa kwa Mabaraza nakala 34 zilizoandaliwa vizuri za ripoti, kumbukumbu na manukuu, wakisema kuwa hizo ni nyenzo muhimu zaidi za kihistoria. Kisha Frostlock wanawaomba viongozi wa Wen kutia saini hati ya kuthibitisha kuwa nakala hizo ni "rekodi kamili ya mkutano." *Je, TNC inapswa kuwa na mashaka yoyote?*** | *Ndiyo. Kwanza, kanuni za Uamuzi Unaofaa na Nia Nema zinalinganishwa na kutafuta saini za IPLC au uidhinishaji mwingine wa hati au nyenzo ambazo IPLC hawafahamu kwa kina na kwa undani. Kuomba Wen kuidhinisha hati ambayo hawajaikagua ni kana sawa na kuwaomba watie saini mkataba ulioandikwa kwa lugha wasiyofahamu. Pili, ikiwa kutakuwa na rekodi rasmi ya mkutano, Wen wanapaswa kushirikishwa, au kusimamia mchakato wa kuiunda.* |

| **Kwa mfano** | *Mawazo na Mwongozo* |
| --- | --- |
| **3**<br>**FrostLock iliwaarifu wawekezaji wake kwamba tathmini za kiufundi zinaonyesha kuwa kuna uwezekano kuwa teknolojia yake ya utunzaji itafaulu. Tathmini za kiufundi, zilizofichuliwa wakati wa mashauriano, hazikinzani na hii, hata hivyo: Watathmini wanakadiria uwezekano wa kufaulu kuwa asilimia 51. Frostlock haingependa tathmini zijumuishwe kwenye rekodi ya umma kwa sababu zina maelezo ya haki miliki. Wakati suala la uwezekano wa kufanikiwa lilipoibuka wakati wa mashauriano, Wen walisema kwamba watazidi kuunga mkono mpango hata ikiwa kuna uwezekano mdogo tu wa ufanisi. *Je, TNC inapaswa kukubali ombi la FrostLock la kutojumuisha rekodi fulani?*** | *Ombi la FrostLock linaweza kupuuzwa, lakini halionekani kuwa na tatizo kubwa. Uwazi ni sehemu muhimu ya Uwajibikaji, na kutofumbua maelezo ya umiliki ni kinyume na hili. FrostLock haionekani kuwa inawapotosha wawekezaji, na uhusiano wao na wawekezaji sio jukumu la TNC au Wen. Inaonekana kwamba watu wa Wen wanafahamu kuhusu uwezekano wa mpango kufaulu na hilo ndilo wanahitaji ili ili kufanya uamuzi.* |
| **4**<br>**Sawa na ilivyoelezwa hapa juu, lakini maelezo ambayo FrostLock ingependa yasijumuishwe kwenye rekodi yanahusu aina ya kemikali zinazotumiwa kuchimba na kudhibiti. Kemikali kadhaa ni mpya bado zinaendelea kufanyiwa majaribio. *Je, ombi hili linapaswa kukubaliwa licha ya kuwa halifuati kanuni?*** | *Ukiukaji huu unaweza kuchukuliwa kuwa unaoathiri ufanisi wa rekodi ya umma.*<br><br>*Migogoro kuhusu sera za umma inaendelea kote ulimwenguni na inahusu haki ya umma kujua elementi zilizo kwenye kemikali zinazotumiwa uchimbaji. Madhumuni moja ya rekodi ya umma ni kuruhusu Wen na washikadau wengine kurejelea uamuzi kulingana na maelezo mapya — yanayoweza kuibuka kutokana na majaribio yanayoendelea. TNC na Wen wanapaswa kujaribu kuafikiana kuhusu maelezo yasiyofaa kufumbuliwa lakini pia shari wazingatie mahitaji ya uhifadhi rekodi. Huenda kanuni inaruhusu watafiti wachache tu kufahamu kuhusu kemikali.* |
| **5**<br>**Mabaraza yanaarifu TNC kwamba hayana idhini yoyote kuhusiana na rekodi, kama vile kuishiriki na jamii. Wanapanga tu kuiweka kwenye faili katika afisi kuu ya Baraza. *Je, inapswa kuishia hapo?*** | *TNC haina rasilimali za kutosha, lakini timu inaweza kuratibu njia za ufikiaji wa rekodi, kwa mfano kwa kuwa na tovuti ya kumbukumbu, kupakia hati na video za muhimu za vikao, au kuandika muhtasari wa ukurasa mmoja kuhusu mchakato. Ikiwa mchakato wa mashauriano ulikuwa wa kihistoria na ulihusisha kukusanya simulizi za Wen, kuweka matarajio, na kusikiliza ahadi za FrostLock na TNC, kunaweza kuwa na sababu nyingi za kuwafanya wamiliki na wadau kukagua upya mchakato huo. Kutayarisha nyenzo zote pia husaidia katika kuendelea kujifunza.* |



Moduli ya 6:

# Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho

Katika moduli hii:

Jifunze jinsi ufuatiliaji wa matokeo unaweza kudumisha haki za binadamu

Buni viasharia vikuu vya utendakazi na ufanisi ili kufuatilia uzingatiaji wa Kanuni na Sera za Kulinda

Kusanya maoni, yatathmini kisha utekeleze mabadiliko kama inavyohitajika

**Vielelezo vya Utafiti wa Wenland:**

6A. Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho

## Utangulizi

**Moduli hii inatoa mwongozo kuhusu kufuatilia, kutathmini na kurekebisha utendakazi wa TNC ili kuzingatia haki za binadamu katika kufanya kazi na IPLC. Huu ni mchakato wa kuendelea kujifunza na kuboresha kupitia uchanganuzi wa matokeo na athari za shughuli zetu.**

Ufuatiliaji, tathmini na marekebisho ni vigezo vya haki za binadamu, na pia zana muhimu katika usimamizi wa miradi. Kama ilivyofafanuliwa katika Moduli ya FPIC na Utatuzi wa Mgogoro, kuheshimu haki za binadamu za IPLC kunamaanisha kuchukua hatua za kuzuia athari mbaya kwa haki za binadamu, kutambua na kupunguza athari, na kuelewa na kuimarisha michakato na sera zinazolinda haki za binadamu za IPLC.

# Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi

Utangulizi unajumuisha ufafanuzi wa Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zinazotumika na IPLC katika ushirikiano wa usawa. Tano ni muhimu hasa katika ufuatiliaji, tathmini na marekebisho:

### Kanuni na Sera Muhimu za Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho

**Kufanya Uamuzi Baada ya kuelewa:**
Lengo ni kuendelea kujifunza na kuboresha. Suluhu inaweza kupatikana endapo timu zitashughulikia hali kwa haraka na kwa njia inayofaa. Matokeo mazuri yanaweza kupatikana na kuchochewa mpango ukiendelea.

**Mashauriano Muhimu:**
Mchakato wa mashauriano unapaswa kuzingatia mashaka na vipaumbele vya IPLC, ambavyo vinapaswa kuzingatiwa katika kubuni viashiria vya Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho.

**Usawa na Uhusishaji**
Kutokana na msemo maarufu, "kinachotathminiwa hutekelezwa," ni muhimu kujumuisha maoni ya watu mbalimbali katika kubuni mfumo wa kutathmini uzingatiaji wa haki za binadamu kwenye TNC.

**Uwajibikaji:**
Uwajibikaji unaweza kuzingatiwa wahusika wanapowajibika matendo yao kulingana na maelezo yanayotolewa na mfumo madhubuti wa Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho.

**Nia Njema:**
Ufaafu wa waelezo yanayotolewa na mfumo madhubuti wa Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho unategemea vile yanavyotumika. Usimamizi wa utendakazi unaozingatia haki za binadamu unahitaji utekelezaji wa kanuni kupitia ushirikiano na uwajibikaji.

## Uzingatiaji wa Haki za Binadamu za IPLC

Moduli hii inazingatia ufuatiliaji, tathmini na marekebisho ya jinsi mpango unavyoathiri haki za binadamu za IPLC. TNC pia imetayarisha nyenzo kuhusu mifumo, masharti na viashiria vya uhifadhi na ustawi wa binadamu,[1] yanayopaswa kutumika kufuatilia malengo na matokeo ya mpango. Timu za TNC zinapaswa kufahamu kuwa kuna mifumo mipana ya kufahamu jinsi mpango unavyoshughulikia malengo ya uhifadhi na ustawi wa jamii, lakini lengo haswa ni kuhakikisha juhudi za TNC za kuheshimu na kulinda haki za binadamu za IPLC wanatathminiwa, wanaeleweka na kutumiwa kama nyenzo ya kujifunza kwa marekebisho yanayoendelea. Kwa hivyo, ni muhimu kuelewa upeo wa Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho yaliyofafanuliwa katika Mwongozo huu, ikilinganishwa na mifumo mingine.

### Mfumo Unayofaa Kuzingatia

**Athari za mchakato wa mpango:**
*Tumia Mwongozo huu.* Mwongozo huu hasa unazingatia wahusika na utekelezaji wa mpango — yaani, mchakato. Hivyo basi, ufuatiliaji tunaojadili katika moduli hii unahusu kuhakikisha kuwa mchakato unaheshimu na kuzingatia haki za binadamu kulingana na Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zilizotajwa katika Mwongozo huu. Kwa mfano, je, kuna kiwango cha juu cha ushiriki wa IPLC na vitambulisho vya kijamii vinavyowahusisha? Je, kujiamulia mwenyewe unahimizwa

kutokana na jinsi shughuli zinavyotekelezwa?

**Athari zisizotarajiwa za mpango huo:**
*Tumia Mwongozo huu na mifumo mingine ya TNC.* Cha msingi zaidi kuhusiana na haki za binadamu ni jukumu la kutodhuru. Kwa hivyo Mwongozo unapozingatia jinsi mpango unavyotekelezwa, tungependa pia kuhakikisha kuwa shughuli na matokeo ya mpango huo hayana athari mbaya kwa haki za binadamu, hata ikiwa nia ni nzuri. Kwa kurejelea mfano wa mradi wa uhifadhi unaofadhiliwa na shirika la wageni kutoka nchi za nje katika Moduli ya Utekelezaji, ni nini kitachotokea ikiwa idadi ya watalii na athari za miundombinu ya utalii inafanya iwe ngumu kwa IPLC kudumisha desturi zao? Ni muhimu kushirikiana na IPLC kutambua mapema mashaka haya nyeti na kubuni viashiria na michakato mwafaka ya ufuatiliaji ili kuyaelewa na kuyazuia kutokea. Wafanyakazi wa TNC wanapaswa kurejelea moduli hii pamoja na mifumo mingine pana ya tathmini, ikijumuisha Mfumo wa TNC wa Maoni, Uamuzi na Hatua.

**Malengo ya mpango:**
*Rejelea taratibu zingine za TNC.* Wakati wa kushirikiana na IPLC katika kuweka malengo na kanuni husika za mpango, ni muhimu sana kurejelea taratibu nyingine, kama vile Mfumo wa TNC wa Maoni, Uamuzi na Hatua, unaojumuisha mwongozo kamili kuhusu kuweka kanuni za uhifadhi na ustawi wa binadamu, pamoja na kanuni za usawa.

## Mwongozo

### Hatua ya Kwanza: Buni Viashiria

**Kiolezo: Viashiria vya Haki za Binadamu**

Angalia Kiolezo cha Viashiria vya Haki za Binadamu

Ni muhimu kwa TNC na IPLC kubuni viashiria pamoja, kwa kuzingatia vitambulisho vya kijamii ambavyo huenda vimetengwa. Moduli ya Mafunzo na Majadiliano ya Mwanzo ina mwongozo kuhusu mbinu zinazozingatia desturi ili kuhakikisha kuna uhusishaji. Ufuatiliaji ukifanywa vyema, matokeo yanaweza kuwa muhimu kwa IPLC kwa madhumuni mengine zaidi ya mpango huo.

Viashiria na taratibu za ufuatiliaji zinapaswa kuundwa, kujumuishwa na kutekelezwa pamoja na vigezo vingine vya mpango. Utaratibu jumuishi hutoa data bora inayokusanywa kwa wakati, kwa kutumia mbinu bora na inayoweza kutumika kwa muda mrefu zaidi. Utaratibu huu huwezesha maarifa na matokeo ya mapema kutumika katika kuendeleza utekelezaji.

Katika hatua ya kwanza ya kuunda viashiria, TNC na IPLC wanapaswa kurejelea Tathmini ya Athari kwa Haki za Binadamu au mashaka mengine nyeti kama sehemu ya Mchakato wa FPIC. Fikiria kufanya tathmini mpya ya Athari kwa Haki za Binadamu iwapo hakuna tathmini imefanywa au ikiwa tathmini

iliyopo ni ya zamani. Athari zozote zinazopewa kipaumbele au mashaka muhimu yanapaswa kuchukuliwa kuwa viashiria maalum vinavyofuatiliwa kwa muda. Hii inapaswa kusaidia TNC na IPLC kujibu maswali muhimu kama vile:

**Maswali Muhimu kuhusu Ufuatiliaji Unaoendelea**

Je, malengo, vipaumbele na mashaka muhimu ya IPLC ni yepi kuhusu mpango?

Je, mpango unaweza kuathiri vipi nyenzo au desturi za msingi za IPLC?

Je, ni masuala gani ya utata yaliyotokea wakati wa mashauriano?

Je, matarajio yepi ya IPLC kuhusiana na mpango yalichangia uamuzi mwafaka na FPIC?

Majibu ya maswali haya yatasaidia timu kubuni viashiria vyao muhimu vya haki za binadamu na kuelewa vyema vipaumbele na matarajio ya ufuatiliaji. Timu zitaweza kushughulikia hali zisizotarajiwa zinapotokea na kuhakikisha kuwa IPLC wanahisi kwamba kujiamulia wenyewe kunapewa kipaumbele katika mchakato wa utekelezaji. Kwa mfano, hebu rejelea tena mradi wa utunzaji unaofadhiliwa na shirika la kigeni.  Usilimishaji wa kushinikiza ulitambuliwa kuwa athari hasi, kutotokana na ongezeko la watalii.[2] Viashiria vya kufuatilia **athari za mpango zisizotarajiwa** huenda zikajumuisha:




**Idadi ya wageni** | **Shughuli ya usalama** | **Shughuli za kibiashara** | **Kujihusisha katika jamii** | **Athari zilizobainishwa**

- idadi ya wageni – data kutoka vituo vya wanaowasili au mauzo ya tiketi
- shughuli za usalama – zilizoripotiwa kwa maafisa wa polisi wa eneo au mamlaka za manispaa
- shughuli za kibiashara – zinazoendeshwa serikali za eneo hilo, vyama vya wafanyabiashara, au wanajamii
- wanajamii kujihusisha na watalii – uchunguzi wa kiwango cha maisha na idadi na wanajamii
- athari mahususi zilizobainishwa, kama vile kelele, takataka au athari kwa wanyamapori wanaohusishwa na watalii kutoka kwa data ya utafiti au ripoti.

Chanzo kingine cha kufahamu viashiria ni mizozo au migogoro inayoibuka. Mizozo haiwezi kuepukika, na badala ya kuzua wasiwasi, inapaswa kuchukuliwa kuwa fursa za kuhimiza uwazi na kujenga uhusiano na ILC.

Kupitia utatuzi wa mizozo, TNC inaweza kuthibitisha uzingatiaji wake wa Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi, hasa Nia Njema na Wenyeji Kujiamulia Wenyewe.

Kuchunguza mzozo, jinsi unavyoibuka na jinsi unavyoshughulikiwa kunaweza kudhihirisha yanayohitaji kuangaziwa. Hata baada ya mzozo kutatuliwa, inaweza kudokeza mambo yanayopaswa kufuatiliwa mara kwa mara.

Viashiria vya kufuatilia **athari za mpango** zinaweza kutolewa kwenye orodha za mambo ya kushughulikia zilizo kwenye kila moduli katika Mwongozo. Ni muhimu kujumuisha viashiria vyote visivyo na mapendeo na vilivyo na mapendeleo (mtazamo) – na timu zinapaswa sifa za kiashiria kinachostahiki, kwa mfano, SMART na SPICED[3]. Viashiria visivyo na mapendeleo huwezesha uchambuzi usiwe na ubaguzi kutokana na matarajio au uzoefu. Viashiria vyenye mapendeleo huonyesha uzoefu na tabia, na kuhakikisha maoni ya IPLC yanasikika.

Kama ilivyo katika aina zote za viashiria, chacha ni bora zaidi. Ili kuhakikisha uwazi na uwezekano, TNC na IPLC wanapaswa kushirikiana katika kubuni viashiria vichache mahususi vinavyoonyesha mashaka muhimu yanayohitaji kushughulikiwa. Kwa mradi mdogo wa eneo maalum unaohusisha IPLC mmoja, viashiria vitatu vya haki za binadamu vinatosha. Kwa miradi au mipango mikubwa ya sera inayohusisha wahusika wengi na ina wataalamu wa kufuatilia na kutathmini mara kwa mara, huenda kukahitajika viashiria kumi au zaidi vya haki za binadamu.

**Kidokezo: CbD 2.0 Ufuatiliaji Shirikishi**

Mwongozo wa CbD 2.0 unahimiza ufuatiliaji unaoshirikisha jamii na unahimiza kuajiriwa kwa wanakandarasi ili kujaza nafasi zilizopo (angalia kurasa za 96-97). Wakati wa ufuatiliaji wa mbinu inayozingatia haki za binadamu, wanakandarasi wanapaswa kuwa na uzoefu na ujuzi wa kushirikiana na IPLC katika utendakazi.

**Nyenzo: Viashiria Muhimu vya Shirika la Danish Institute for Human Rights**

Shirika la Danish Institute for Human Rights lina viashiria vinavyoweza kurejelewa (haswa Sehemu ya B, Athari kwa Jamii, Kifungu cha 2 na 3: Usimamizi wa Ardhi, na Afya na Usalama wa Mazingira, ukurasa wa 68-82). Angalia Muhtasari wa Tathmini ya Uzingatiaji wa Haki za Binadamu, Danish Institute for Human Rights (2006). Hata hivyo, wafanyakazi wanapaswa kufahamu kuwa viashiria na vigezo vingi vilivyoelezwa hapa vinaweza kutumika tofauti na ilivyo kwenye mipango ya TNC, nyingi yazo hutumika katika kampuni za kibinafsi, na baadhi yao hayazingatii kanuni na Sera za Kulinda Maslahi zilizo katika Mwongozo huu.

## Hatua ya Pili: Kusanya na Utathmini Maoni

Pamoja na kuwepo kwa viashiria na uzingatiaji wa haki za binadamu, TNC na IPLC wanapaswa kushirikiana katika ufuatiliaji na ukusanyaji wa data kwa muda uliobainishwa kwa kutumia njia zinazofaa. Wanaoathirika zaidi ndio wanaweza kubaini vyema zaidi ikiwa data ni sahihi, ni wakilishi na yenye maana. Data inaweza kukusanywa kwa njia kadhaa:



Kutumia data iliyopo



Kupata takwimu za idadi ya watu



Kuwahoji wanachama wa IPLC

Kutumia data iliyopo (mbadala); kuchunguza idadi ya watu katika kipindi mahususi; na kuhoji wanachama wa IPLC kuhusu ujuzi wao.

Kama ilivyo katika ufuatiliaji, tathmini na marekebisho yote yanayofanywa, ukusanyaji wa data kulingana na viashiria vilivyowekwa unapaswa kuanza kabla ya shughuli kuanza ili kuweka kigezo cha ulinganisho. Ikiwa tayari mpango unaendelea, timu zinapaswa kuanza ukusanyaji wa data haraka iwezekanavyo.

TNC na IPLC wanapaswa kushirikiana kubuni mbinu za kuchambua data inapokusanywa, na kubaini nyenzo zinazohitajika kwa tathmini. Nyenzo za nje zinaweza kutoa mbinu na taratibu za kutathmini ya data zinazoafiki mpango, data na bajeti iliyopo ya timu. Tathmini Bora inaelezea zaidi ya mbinu 300 za tathmini, zilizoainishwa katika vikundi viwili vikuu katika awamu saba tofauti. TNC pia ina utaalam mkubwa wa kindani kuhusu tathmini ya data, na wafanyikazi wanaweza kuwasiliana na Timu ya Kimataifa ya Wenyeji na Jamii za Eneo hilo ili kupata usaidizi.

Ni kawaida kwa tathmini kufanyika mara mbili wakati wa mpango. Ya kwanza hufanyika wakati wa utekelezaji, na hujulikana kama tathmini ya muda mfupi, na kawaida hujumuisha kaguzi mbili za katikati ya mpango, nayo ya pili hufanyika utekelezaji ukikamilika, na hujulikana kama tathmini ya muda mrefu, na mara nyingi hulinganisha viashiria kabla na baada ya mpango. Kwa mipango mikubwa au ya muda mrefu, mchakato wa awamu nyingi unaweza kufaa zaidi, na unaweza kujumuisha tathmini ya muda mrefu katika awamu tofauti.

Upeo wa tathmini utategemea masharti ya muda na bajeti. Njia bainifu sio bora kila wakati, hasa ikiwa zinatenga IPLC ambayo ujuzi na maarifa yake ni muhimu katika kuelewa data. Mkutano wa kila mwaka wa kutathmini ni muhimu. Wakati wa mkutano wa kufanya tathmini, IPLC na TNC hukagua viashiria vyao vya haki za binadamu, Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi kwenye Mwongozo huu na orodha ya mambo ya kushughulikia katika kila moduli ili kuhakikisha kanuni zinazingatiwa. Pia hutathmini tena kiini cha kutekeleza mabadiliko kisha kufanya marekebisho. Hii inajulikana kama kujifunza kupitia awamu mbili (hapa chini). Mikutano ya tathmini inaweza kufanywa wakati wa utekelezaji na katika tathmini ya mwisho ili kufanya marekebisho.




## Hatua ya Tatu: Kufanya Marekebisho

Kwa kutumia maarifa yanayotokana na data inayofuatiliwa, IPLC na TNC wanaweza kuanza kazi chamamano na ya ubunifu ya kurekebisha mchakato ili kushughulikia athari zozote kwa haki za binadamu au matatizo yatakayojitokeza. Hata ikiwa hakuna matatizo, timu inaweza kuboresha na kuoanisha vyema mpango na vipaumbele vya IPLC. Matokeo ya ufuatiliaji yanaweza kuonyesha timu mambo yanayostahili kubadilishwa, yanayopaswa kuimarishwa au kuendelea kutekelezwa. Ni muhimu kurejelea jinsi IPLC na TNC zilivyoshirikiana kubuni mbinu zinazozingatia haki za binadamu, zilivyotatua mizozo, zilivyoboresha usimamizi na kuongeza mpango.

TNC inapaswa kushirikiana na IPLC juu katika kufanya marekebisho. Watu wanaathirika ndio wanaofaa zaidi kubaini ikiwa mabadiliko yanayopendekezwa yanaafiki

Katika kushughulikia mashaka ya IPLC au athari mbaya kwa haki za binadamu, marekebisho kama vile sera za ziada za kulinda maslahi zinatosha endapo zitatekelezwa kwa uvumilivu, kwa nia njema na kwa kutumia nyenzo. Hata hivyo, kunaweza pia kuwa na mashaka yanaoonyesha kutoridhika, kutokuelewana, kasoro za kimfumo au upinzani mkuu unaoweza kusababisha IPLC na TNC kuhoji ufaafu au umuhimu wa mradi fulani. Katika hali hizi, huenda kukawa na haja ya kurejea kwa mazungumzo na mashauriano. TNC na IPLC wanaweza kuamua kuwa ili kuzingatia Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi, mpango unahitaji kufutiliwa mbali. Bila shaka, upunguzaji upeo au shughuli za mpango sharti ufanyike kwa kushirikiana kwa karibu na IPLC ili kuepuka hali ya wahusika kujiondoa ambayo huonyesha ukosefu wa nia njema.

**Kuzuia Athari na Kufanya Marekebisho**

Mchakato wa Kuzuia Ukiukaji wa Haki za Binadamu ulioelezwa katika Moduli ya FPIC unaweza kutumika katika kuzuia hatari na kufanya marekebisho. Mchakato Kuzuia Ukiukaji wa Haki za Binadamu unajumuisha:

1. Kutathmini athari halisi na zinazoweza kutokea kuhusiana na haki za binadamu
2. Kuzuia athari mbaya zilizobainishwa katika mchakato wa tathmini
3. Kufuatilia ushughulikiaji na matokeo ya kanuni za kuzuia athari
4. Kuwasiliana na wamiliki na wadau wote husika jinsi athari zinavyoshughulikiwa

Hoja ya 3 ya mchakato wa Kuzuia Ukiukaji wa Haki za Binadamu uliofafanuliwa hapa juu inaunda mchakato wa kurejelea matokeo unaotumia mifumo ile ile ya ufuatiliaji na tathmini inayotumiwa kutambua mashaka au athari mwanzoni ili kutathmini ufanisi wa kanuni ya kuzuia athari. Hoja ya 4 inaunda mchakato cha kuangazia matokeo ya baadaye kwa kuongeza wahusika na wadau (sawa na wajibu wa usiri) wanaoweza kufuatilia mchakato unaoendelea na kuchangia maoni.

Kwa kurejelea tena mfano wa mradi wa uhifadhi unaofadhiliwa na shirika la kigeni, ikiwa matokeo ya ufuatiliaji yanaonyesha idadi ya wageni wanaoruhusiwa haizingatii vipaumbele vya IPLC vya kijamii na vya mazingira, timu inaweza kuamua kupunguza zaidi idadi ya wageni wanaoruhusiwa kwa siku. Ikiwa mahojiano na IPLC yanaonyesha upungufu huu, awamu nyingine ya mahojiano itafanywa baada ya muda ili kutathmini jinsi masharti mapya yanavyotumika, nayo matokeo yatashirikiwa waziwazi kwenye jamii.

**6A. Utafiti wa Wenland wa Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho**

Mradi wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi umekuwepo kwa miaka tatu, na data ya awali ya utunzaji inaonyesha kuwa kuna ufanisi. Malalamishi kuhusu athari za ujenzi (kelele) yametufikia, lakini hakuna thibitisho kuwa mradi unaathiri mazingira.

Tazama Utafiti

## Orodha ya kukagulia ya Ufuatiliaji, Ttahmini na Marekebisho

Pamoja na maelezo yaliyo hapa chini, wafanyikazi wa TNC wanapaswa kurejelea hatua husika mwishoni mwa kila moduli, inayojumuisha mchakato kamili wa ufuatiliaji, tathmini na marekebisho.

### Hatua ya Kwanza: Buni Viashiria

- [ ] Buni viasharia mahususi vya athari kwa haki za binadamu vinavyoonyesha malengo, mashaka muhimu na vipaumbele vya IPLC kulingana na Tathmini ya Athari kwa Haki za Binadamu au masuala yanayohitaji kushughulikiwa yaliyobainishwa kupitiaa tathmini au michakato mingine.
- [ ] Rejelea michakato ya kujihusisha iliyopo au iliyowekwa na IPLC

### Hatua ya Pili: Kusanya na Utathmini Maoni

- [ ] Anzisha mifumo ya ufuatiliaji na ukusanyaji data kwa muda mahususi kwa kutumia njia zinazofaa, ukizingatia michakato iliyopo ya ushirikiano ya IPLC
- [ ] Buni mbinu, ukizingatia tathmini zote za muda mfupi na za muda mrefu (kwa mfano, mikutano ya tathmini ya katikati na mwisho wa mpango)

### Hatua ya Tatu: Kufanya Marekebisho

- [ ] Tekeleza mabadiliko kama inavyohitajika, kulingana na matokeo ya tathmini

## Hati za Kuhifadhi

**Angalia Moduli ya Hati ili upate maelezo zaidi kuhusu hati zinazohitajika.**

- [ ] Viashiria vya ufuatiliaji wa Haki za Binadamu
- [ ] Mbinu za kukusanya data na matokeo
- [ ] Nyenzo zinazoelezea mbinu za tathmini na madokezo ya utekelezaji wa mbinu hizi
- [ ] Taratibu maalum kufanya marekebisho na mipango kuhusu jinsi ya kutekeleza

## Maelezo

[1] Wasiliana na Nicole DeMello (ndemello@tnc.org) ili upate maelezo zaidi kuhusu Mfumo wa TNC wa Sauti, Uamuzi na Hatua za Hatua za TNC, anaotoa mwongozo kuhusu uhifadhi na viashiria vya ustawi wa binadamu, ikijumuisha viashiria kuhusu usawa. Mfumo wa TNC wa Maoni na Uamuzi, au “Mfumo wa VCA” unafafanua jinsi TNC inavyoshirikiana na IPLC katika utunzaji na uundaji wa malengo ya kudumu.

[2] Pata maelezo zaidi kuhusu mfano huu katika Moduli ya Utekelezaji

[3] “Japo hakuna sheria zilizowekwa za kuchagua viashiria, mwongozo mmoja maarufu ni kutumia ufupisho 'SMART': viashiria vinapaswa kuwa Mahususi, Vinavyoweza Kupimika, Vinavyoweza kutimizwa na vya kutekelezwa, Vinavyostahiki, na Vinavyoweza kutekelezwa kwa muda mahususi. Mwongozo huu unaambatana haswa na viashiria vya upimaji. Ufupisho mwingine uliopendekezwa hivi majuzi ni ‘SPICED’: Kutemea Hali Mahususi, Kushirikisha, Kufasiriwa, Kutumika kwa Njia Anuwai, Kuwezesha na Kuwa Sahili. SMART inaelezea sifa za viashiria vyenyewe, nayo SPICED inahusiana zaidi na jinsi viashiria vinapaswa kutumiwa.” Kutokana na Tathmini Bora — Zana ya Ufikiaji Sawa, Ufuatiliaji na Tathmini Shirikishi, Moduli ya 2: Kuweka Malengo na Viashiria.
https://www.betterevaluation.org/sites/default/files/EA_PM%26E_toolkit_module_2_objectives%26indicators_for_publication.pdf
https://connect.tnc.org/sites/lands/indigenous/SitePages/Human%20Well-Being%20Measures.aspx




# Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho

## 6A. Utafati wa Wenland:

**Mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi umekuwepo kwa miaka tatu, na data ya awali ya utunzaji inaonyesha kuwa kuna ufanisi. Malalamishi kuhusu kelele za ujenzi yametufikia, lakini hakuna thibitisho kuwa mradi unaathiri mazingira.**

Matukio yafuatayo yametokea:

- Vikundi mbalimbali vya Jamii za Wen vimezungumza na TNC kuhusu kutoridhika kwao. Hawataji athari halisi, lakini wanasema ikuwa idadi ya Waalbania walio katika sehemu ya kaskazini imeongezeka, na Wen hawajihisi nyumbani. Wanaeleza TNC kuwa wangekuchukua hatua nyingine wangekuwa na uwezo.
- Ushiriki wa wanawake katika Kamati za Usimamizi wa Mazingira umepungua. Wanaodai kuwa shinikizo kutoka kwa Mabaraza na wanaume wengine katika jamii ilifanya iwe vigumu kwa wanawake kushiriki. TNC pia imesikia kuhusu unyanyasaji wa kisasi na ukatili wa kijinsia, lakini hakuna malalamishi rasmi yaliyowasilishwa
- Matatizo ya watalii kufurika, ambapo mzozo unatokana kufuatia watalii kumiliki raslimali zilizoko, yameibuka. Maeneo ambako teknolojia ya utunzaji inatumika yanatembelewa sana, na idadi ya wanaozuru huongezeka wakati wa sherehe za Wen za majira ya joto. Kwa muda mrefu jamii za Wen zimesisitiza kuwa wageni wasiruhusiwe kuingia Wend wakati wa sherehe zao, lakini serikali ya Albania imekataa kuchukua hatua yoyote na kulichukulia kuwa suala tofauti. FrostLock vile vile haiko tayari kuchukua hatua.

| **Kwa mfano** | *Mawazo na Mwongozo* |
|---|---|
| **1**<br>**Kwa kuzingatia uwekezaji wote na FrostLock, wazee wa Wen wazee hawana uhakika ikiwa wanafaa kuondoa idhini yao kuhusiana na mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi, au walifaa kufanya hivyo awali. *Je, kuna hakuna yoyote wanayoweza kuchukua kutokana na kutoridhika kwao sasa?*** | *Kwa upande mmoja, Kuheshimu Kujiamulia Mwenyewe hakumaanishi kuwa Wen hawana wajibu wa kutimiza ahadi zao. Lakini si haki kushinikiza sana Wen kutokana na matokeo mabaya ambayo hawangeweza kubashiri, hasa inapoathari pakubwa uamuzi wa kibinafsi.* |

| **Kwa mfano** | *Mawazo na Mwongozo* |
|---|---|
| | *Kwa upande wake, TNC inaweza kukataa ubatilishaji idhini lakini bado iruhusu Wen ya kubatilisha idhini yao na kuwajibikia matokeo, ikiwa hatua hiyo ni muhimu kwa kujiamulia mwenyewe. Hali kama hii huonyesha pengo katika mchakato wa mashauriano na elimu ya jamii inayohitajika katika kufanya Uamuzi Unaofaa. Suala la idhini linaweza kuwekwa kando ili kutatua kiini cha matatizo kinachosababisha kutoridhika. Kauli ya "tungeifanya kwa njia tofauti" inaweza kurejelea masuala maalum ya utekelezaji yanayoweza kushughulikiwa, au baadhi ya mabadiliko ambayo wanajamii wangependa lakini wanahisi kuwa hawana uwezo wa kuomba yatekelezwe. TNC inapaswa kufanya mashauriano upya ili kutambua matatizo, na kushirikiana na FrostLock katika kuzingatia mchakato madhubuti wa FPIC, unaojumuisha ukaguzi wa mara kwa mara, haswa maelezo au mabadiliko mapya yanapotokea.* |
| **2**<br>**Timu ya ufuatiliaji ya TNC inagunda kuongezeka kwa tofauti za kijinsia kwenye Kamati za Usimamizi wa Mazingira lakini inaongeza kuwa zana pekee ya TNC, yenye mamlaka ya uteuzi, haijafaulu. Na japo TNC imesikia kuhusu athari za usawa wa kijinsia kwa uanachama wa Kamati kwenye Vikundi vya Kijamii, hakuna data inayothibitisha hili. Isitoshe, TNC haina idhini ya kufuatilia wala kuingilia kati mizozo ya kindani ya kijamii. *Je, hii ni tathmini inayofaa?*** | *Hapana. Uchunguzi zaidi unahitajika. Madai hayo yanaonyesha athari kwa haki za binadamu zinazotokana na Kamati za Usimamizi wa Mazingira na hivyo, mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi. Hii inahitaji kushughulikiwa sawa na vile athari za mazingira zingeshughulikiwa.*<br><br>*Wanawake Wen wamewahi kutafuta usaidizi kutoka kwingine, na jamii ya Wen kwa jumla imekubali kuwa kuna tatizo la usawa wa kijinsia, na Mabaraza ya wanaume yamekubaliana kushughulikia suala hili wakati wa utekelezaji. Hata hivyo, kutokana na tetesi kuwa udhalilishaji, ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia unaendelea, TNC inapaswa kufanya juhudi zaidi kupata habari, ikiwemo kurejelea Mwongozo wa TNC wa Kujumuisha Usawa wa Kijinsia katika Uhifadhi, na inapaswa kutafuta washirika wenye ujuzi. Msingi muhimu na wajibu wa serza zote za kulinda maslahi ni kutodhuru.* |
| 3<br>**Ikiwa serikali ya Albania inafahamu kuhusu suala la ongezeko la wageni kutoka nchi za nje na haijachukua hatua yoyote, je, TNC inapaswa kutoshughulika?** | *NC inapaswi kuendelea kuwajibikia hali hii. Ongezeko kubwa la watalii ni matokeo ya moja kwa moja ya mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi (angalia UNDRIP, Kifungu cha 12, kinacholinda haki ya faragha kwa sehemu muhimu za kidini na kitamaduni).* |

| **Kwa mfano** | *Mawazo na Mwongozo* |
| --- | --- |
| | *Lakini ilikuwa vigumu kubashiri athari hii. Japo FrostLock na TNC hawana uwezo wa kupiga marufuku utalii, wote wawili wanapaswa kutumia uwezo na rasilimali ili kuzuia tatizo. Mipango ya kuhamasisha zinaweza kuundwa ili kuelimisha watalii kuhusu kuheshimu faragha ya watu wa Wen, au eneo la maonyesho au jumba la makumbusho linaweza kujengwa mbali na mahali ambapo sherehe zinafanyika.* |
| **4**<br>**Shirika la Wen lililoteuliwa kuchukua usimamizi wa Eneo la Usimamizi wa Uhifadhi kutoka kwa TNC limekwama. Hakuna aliyeajiriwa, hakuna mipango iliyowekwa— na huenda shirika halitakuwa tayari kabla ya muda uliowekwa wa miaka mitano. Mfanyakazi wa TNC apendekeze kuwa timu isiwe na haraka kushawishi shirika hilo, kwani hii itawezesha TNC kuendeleza usimamizi wa shughuli kwenye eneo la uhifadhi, kama vile kusimamia Wendbok ambaye ni kulungu wa nchi za baridi. *Je, hii inakubalika, kwani TNC haina wajibu wowote wa kusaidia uanzishaji wa shirika la Wen?*** | *TNC haiwezi kushurutishwa chini ya Mkataba wa Mpango kusaidia uanzishaji wa shirika la Wen, hatahivyo, Nia Njema na Uamuzi wa Kibinafsi unaweza kutusukuma kuchukua hatua zaidi. Kuwajibikia Eneo la Usimamizi wa Uhifadhi kunaweza kuwasaidia watu wa Wen kuthibitisha kuwa mpango wa utunzaji wa sehemu za ardhi zenye udongo jalidi unazingatia kujiamulia mwenyewe.*<br><br>*TNC ikipuuza hili, huku ikiendelea kutekeleza shughuli zake, inaweza kusababisha hali ya kutokuaminiana kati yao na Wen na huenda mpango wote ukakataliwa. Ni halali kwa TNC kutaka kushughulikia wanyama wa Wendbrok, hata hivyo wanaweza kutumia njia za uwazi zaidi na za kushirikiana.* |

**Kiolezo:**

# Viashiria vya Haki za Binadamu

Kiolezo hiki ni mwanzo wa kubuni viashiria vya haki za binadamu vilivyoelezwa katika Hatua ya Kwanza katika Moduli ya Ufuatiliaji Tathmini na Marekebisho kwenye Mwongozo. TNC na IPLC walishirikiana katika kubuni tathmini ya athari kwa haki za binadamu katika Hatua ya Pili katika Moduli ya FPIC. Viashiria vinazingatia ufuatiliaji wa athari za haki za binadamu katika mpango, kwa mfano, kiwango cha ushiriki unaostahiki, kujiamulia mwenyewe na masuala mengine yaliyomo katika Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi, pamoja na athari zozote zisizotarajiwa katika mpango.

Kiolezo hiki pia kinajumuisha maswali ambayo TNC na IPLC wanapaswa kuzingatia wakati wa kuunda viashiria. Makubaliano kuhusu viashiria yanapaswa kufanywa kwa njia mwafaka, inayoweza kujumuisha saini au herufi za mwanzo za majina ya watu kwenye hati, kutumiana barua pepe, kuinua mikono kwenye mkutano, utaratibu au sherehe.

Kwa mwongozo kuhusu vigezo vya viashiria thabiti, rejelea Kanuni za VCA za TNC na mwongozo wa kuunda viashiria ambavyo ni SMART na SPICED.

(https://www.betterevaluation.org/sites/default/files/EA_PM%26E_toolkit_module_2_objectives%26in dicators_for_publication.pdf).

Maelezo utakayojaza kwenye fomu hii **hayatahifadhiwa** ukiyajaza kwenye kivinjari. Jifunze mengi

Mpango:______________________________

Kipindi cha wakati: ______________________________

Tarehe:______________________________

Imesasishwa kuanzia: ______________________________

Imeidhinishwa na:

Jina:______________________________

Jina:______________________________

Jina: ______________________________

Shirika au kikundi:

Jina:______________________________

Jina:______________________________

Jina: ______________________________

**1. Athari kwa haki za binadamu au masula muhimu yanayohitaji kushughulikiwa**

Kagua tena matokeo ya Tathmini ya Athari kwa Haki za Binadamu au mashaka mengine yanayohitaji kushughulikiwa yaliyotambuliwa katika sehemu ya mchakato wa FPIC katika Moduli ya Pili. Ikiwa TNC na IPLC zimeunda Mpango wa Ushauri kwa kutumia kielelezo kilichotolewa, rejea kwenye orodha ya athari zinazoweza kutokea za haki za binadamu kwenye mpango huo ili kuongoza sehemu hii.

i. Athari chanya zinazoweza kutokea na ambazo ni halisi:

ii. Athari mbaya zinazoweza kutokea na ambazo ni halisi ikijumuisha ukali, uwezekano na sababu za hatari:

iii. Hatua zinazopendekezwa za kuzuia athari mbaya zinazoweza kutokea na zile halisi:

iv. Mpango wa kufuatilia majibu na matokeo na kuwasiliana jinsi athari zinavyoshughulikiwa:

## 2. Maelezo zaidi, ikiwa hayajajumuishwa kwenye athari zilizoorodheshwa hapa juu:

a. Malengo, vipaumbele na mashaka muhimu ya IPLC kuhusiana na mpango:

b. Jinsi mpango unavyoweza kuathiri nyenzo au desturi za msingi za IPLC:

c. Masula tata zaidi yanayofanyiwa mashauriano:

d. Matarajio ya IPLC kuhusiana na mpango yaliyochangia uamuzi mwafaka na FPIC:

## 3. Masuala muhimu kutokana na orodha ya mambo ya kushughulikia katika kila moduli

Kagua hatua zilizo mwishoni mwa kila moduli kwenye Mwongozo, ukiangalia majibu muhimu ya maswali yaliyoulizwa.

a. Moduli ya Kwanza – Mafunzo na Majadiliano ya Mwanzo:

b. Moduli ya Pili – Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa:

c. Moduli ya Tatu – Utatuzi wa Mgogoro:

d. Moduli ya Nne – Utekelezaji:

e. Moduli ya Tano – Kuandika hati:

f. Moduli ya Sita – Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho:

**4. Viashiria vya kufuatilia athari za mpango zisizotarajiwa, kulingana na ukaguzi wa moduli ya 1 na 2 hapa juu**

a. Kiashiria cha 1:

b. Kiashiria cha 2:

c. Kiashiria cha 3:

**5. Viashiria vya kufuatilia athari za mpango zisizotarajiwa, kulingana na ukaguzi wa moduli ya 3 hapa juu**

a. Kiashiria cha 1:

b. Kiashiria cha 2:

c. Kiashiria cha 3:

d. Kiashiria cha 4:

e. Kiashiria cha 5:

**Maswali ya Kuzingatia Wakati wa Kubuni Viashiria:**

- Je, TNC na IPLC wana mpango wa kushirikiana katika kukusanya na kutathmini maoni?
- Je, TNC na IPLC wana mchakato wa kubaini shughuli zinazopaswa kubadilishwa, kuendelezwa na zile za kuimarishwa, kulingana na maoni yaliyopokelewa?
- Je, TNC na IPLC wanapanga kushiriki vipi matokeo ya ufuatiliaji, tathmini na marekebisho na wamiliki na wadau, kwa njia inayozingatia usiri?

PDF hii imetolewa hasa kwa madhumuni ya kuchapisha au kutumiwa nje ya mtandao. Fomu hii haiwezi kujazwa kidigitali isipokuwa kama imepakuliwa na kufunguliwa katika programu ya PDF kama vile Adobe PDF Reader au Kihakiki (Mac OS). Kwa bahati mbaya, maandishi yaliyoandikwa kwenye fomu hii **hayatahifadhiwa** ukitumia kivinjari kama vile Chrome, Safari au Internet Explorer.

### Kiambatisho cha I

# Juhudi za TNC

Kwenye Kiambatisho hiki:

Fahamu juhudi za TNC za kuzingatia haki za binadamu na ushirikiano wa usawa

Fahamu kanuni na viwango vya kimataifa vilivyotumika kwenye Mwongozo huu

Pitia vifungu vya UNDRIP ambavyo ni kiini cha Kanuni na Sera tisa za Kulinda Maslahi

TNC ina maono na maadili ambayo yamebainishwa kupitia sera bora za Mwongozo za kuheshimu na kuhimiza haki za binadamu na ushirikiano wa usawa na IPLC. Uzingatiaji wa viwango vya kimataifa na mwongozo wa ndani ulioongoza kazi hii ni pamoja na:

Zinatumika pakubwa kwenye TNC

- Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji
- Kanuni ya Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa:
- Kanuni Zinazosimamia Mpango wa Uhifadhi Kuhusiana na Haki za Binadamu
- Maadili ya TNC, haswa Heshima kwa Watu, Jamii na Tamaduni
- Kanuni ya Maadili ya TNC, hasa Kutunza Mazingira Yetu
- Mwongozo wa Conservation by Design 2.0

Utaratibu unaozingatia haki za binadamu katika uhifadhi ni unaashiria Maadili ya TNC. Jitihada zetu za kuheshimu na kudumisha haki za IPLC zinahitaji tufuatilie matokeo ya uhifadhi ambayo ni ya usawa, ya kushirikiana na yanayofaa.

Kanuni ya Maadili ya TNC inafafanua utendakazi unaozingatia maadili. Hii inajumuisha:

- umuhimu wa usaidizi na maoni kutoka kwa IPLC katika kufanya maamuzi
- kuheshimu wenyeji pamoja na tamaduni zao zote kokote tunakofanya kazi
- kudumisha haki za binadamu kwa watu wote katika shughuli zetu — kote ulimwenguni
- kufahamu kuwa malengo na azimio letu kamwe hazipaswi kuwa muhimu zaidi ya haki za watu wanaoishi katika jamii tunazozihudumia

Shirika la The Nature Conservancy ni mwanachama mwanzilishi wa Mpango wa Uhifadhi wa Haki za Binadamu, na linafanya kazi pamoja na mashirika mengine sita ya kimataifa ya uhifadhi kujumuisha haki za binadamu katika sera na desturi za uhifadhi. Hili linatekelezwa kwa kuzingatia kanuni nne kuu:

- Kuheshimu haki za binadamu
- Kulinda haki za binadamu katika mipango ya uhifadhi
- Kulinda wanaoathirika zaidi
- Kuhimiza usimamizi bora

Mwongozo wa Conservation by Design 2.0[1] uliotolewa na TNC mwaka wa 2016 unafafanua kuhusu uhusiano kati ya watu na mazingira. Unapendekeza njia jumuishi zaidi katika uhifadhi na sera za kulinda maslahi zinazohusiana na usawa, ustawi wa watu na haki za binadamu. Mwongozo huu hubadilisha ahadi na malengo kuwa hatua za utekelezaji, na itakuwa sehemu ya utekelezaji wa CbD 2.0 katika shirika lote.

Pia tunajitahisi kuzingatia Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji. UNDRIP inachukuliwa kama nyenzo ya kina zaidi ya kimataifa kuhusu haki za pamoja na za kibinafsi za jamii asilia, na inatambua haki za wenyeji na uwezo wao wa kufanya maamuzi [2]. UNDRIP iliidhinishwa na Bunge Kuu la Umoja wa Mataifa mnamo 2007 na ina Vifungu 46 zinazoelezea haki hizi na jinsi zinapaswa kushughulikiwa wakati wa kushirikiana na jamii asilia.

Vifungu vikuu vya UNDRIP ambavyo vimetumika kuunda kanuni za Mwongozo huu ni:

- Kifungu cha 18: haki ya kushiriki katika kufanya uamuzi unaoathiri haki za IPLC
- Kifungu cha 19: haki ya kufanya kazi kupitia taasisi zao wenyewe katika michakato ya Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa
- Kifungu cha 23: haki ya kuamua na kubuni vipaumbele vinavyohusu afya, makazi, na mipango mingine ya maendeleo
- Kifungu cha 24: haki ya kupata dawa zao za kienyeji na haki sawa ya kupata kiwango cha juu zaidi cha afya ya mwili na akili
- Kifungu cha 25: haki ya kudumisha na kuimarisha uhusiano wa kiroho na ardhi na maji yao
- Kifungu cha 26: haki ya kumiliki, kutumia na kukuza ardhi, rasilimali na maeneo yao
- Kifungu cha 29: haki ya uhifadhi na utunzaji wa ardhi na rasilimali zao na ulinzi dhidi ya vifaa hatari katika maeneo yao
- Kifungu cha 31: haki ya kudumisha, kudhibiti na kuendeleza desturi na mila zao, pamoja na maarifa na mali yao ya uvumbuzi
- Kifungu cha 32: haki ya kubaini vipaumbele vya maendeleo na matumizi ya ardhi
- Kifungu cha 40: haki ya migogoro kutatuliwa haraka na kwa njia ya usawa

TNC inaunga mkono kikamilifu kanuni ya Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa, ambayo inadhihirisha haki ya jamii asilia kufanya uamuzi wa kibinafsi. Kujiamulia Mwenyewe hulinda uhuru wa jamii asilia kuhusiana na utambulisho wao, utamaduni na vipaumbele vya maendeleo. Hii inategemea uwezo wa wenyeji wa kujitawala, kuishi katika ardhi zao, kudumisha utamaduni wao na kujilinda dhidi ya ushawishi unaotokana na wakoloni au jamii nyingine tawala. Oviedo et al. (2000) wanafafanua kuhusu haki zinazohusiana na haki ya kujiamulia mwenyewe i katika uhifadhi na usimamizi wa maliasili:

- Haki kuhusiana na ardhi ya urithi na rasilimali
- Udhibiti wa ardhi na rasilimali na haki za usimamizi
- Kujitawala kupitia taasisi na mamlaka za kindani
- Kujiendeleza (kujichagulia maendeleo)
- Idhini ya mapema kuhusu shughuli za uhifadhi na maendeleo
- Haki za kushiriki faida
- Haki ya wenyeji ya kufahamishwa na mali yao ya uvumbuzi kulindwa [3]

## Maelezo

[1] Angalia kurasa za 16-19 na Viambatisho vya C na D.

[2] Ripoti ya Mwandishi Maaalum kuhusu Haki za Wenyeji, James Anaya, Shirika la Umoja wa Mataifa. Nakala ya A/HRC/9/9 (2008), kifungu cha 85: Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji: "[L]inaonyesha maafikiano, katika kiwango cha kimataifa, kuhusu haki za msingi za jamii asilia, kwa kutegemea vyanzo anuwai vya sheria za kimataifa za haki za binadamu. Azimio lenyewe ni matokeo ya mchakato wa kina uliojumuisha maoni yaliyotolewa na wenyeji, na unaashiria na kuhimiza uzingatiaji wa haki za binadamu kwa jumla, kama inavyofasiriwa na kutumiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa na mashirika ya mikataba ya kieneo, na pia kuhusu viwango vilivyoendelezwa na asi na michakato mingine husika."

[3] Oviedo et al. (2000) Wenyeji na Jamii za Eneo hilo za Ulimwengu na Uhifadhi wa Eneo la Kiikolojia: Njia Jumuishi ya Kuhifadhi Utofauti wa Kibiolojia na Kitamaduni Ulimwenguni. WWF & Terralingua. http://d2ouvy59p0dg6k.cloudfront.net/downloads/EGinG200rep.pdf

### Kiambatisho cha II

# Faharasa ya Maneno Muhimu

Kwenye Kiambatisho hiki:

Fafanua maneno muhimu zinadhihirisha lengo la Mwongozo huu

### Usawa:

Mifumo, asasi na sera za haki na usawa zinazohakikisha watu wote wana ufikiaji kamili wa mamlaka na rasilimali ili waweze kufikia uwezo wao na kustawi. Usawa unahitaji kutambua athari za ubaguzi wa rangi, kutengwa, na kuondoa vizuizi vyote vya kushiriki, kupata fursa na kujiamulia mwenyewe.[1]

### Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa

Kiwango cha kisheria cha kimataifa kinachotathmini ikiwa mwingiliano na uamuzi unaoathiri IPLC unahusisha desturi bora za kulinda haki ya wenyeji ya kujiamulia wenyewe.[2]

- Kujitolea kunamaanisha idhini inayotolewa bila kulazimishwa, vitisho au ujanja.
- Inayotolewa mapema inamaanisha kwamba idhini inapaswa kuombwa sio tu mapema kabla ya idhini yoyote au kuanza kwa shughuli, lakini katika hatua za mwanzo za maendeleo ya mradi, kabla ya maamuzi muhimu kufanywa.
- Baada ya kuelewa inamaanisha kwamba IPLC anaweza kufikia taarifa yote muhimu kuhusu kusudi la mradi, ukubwa, upeo na kipindi cha muda wake, wanaoweza kuwa washiriki athari. Mchakato sharti uruhusu muda wa kuchunguza na kufuatilia masuala ya msingi.
- Idhini inamaanisha uamuzi halali wa pamoja unaofanywa na IPLC, kwa kutumia michakato yake ya kawaida ya kufanya uamuzi.

### Jinsia

Jinsia inahusu majukumu na wajibu na majukumu ya wanaume, wanawake na jinsia zingine zilizoko katika familia, jamii na tamaduni zetu. Dhana ya jinsia pia inahusisha matarajio kuhusu sifa, uwezo nzuri na tabia bainifu za jinsia tofauti. Mtu hujifunza majukumu na matarajio ya kijinsia. Yanaweza kubadilika baada ya muda fulani, kutofautiana kati ya tamaduni, na kuathiriwa na vigezo vingine ya kijamii kama vile kabila au tabaka. Kuelewa vigezo vya kijinsia katika muktadha mahususi ni muhimu katika kuelewa utumiaji mamlaka.[3]

### Data ya jinsia mbalimbali

Maelezo yaliyokusanywa kupitia utafiti au mahojiano ambapo watu wa jinsia tofauti wanahojiwa kando kando. Hii ni muhimu katika hali ambapo jinsia tofauti zinaweza kuwa na uzoefu, maarifa, vipaumbele, mahitaji, au tabia tofauti.[4]

**Haki za binadamu**

Watu wote wana haki, bila kujali utaifa, mahali pa kuishi, jinsia, mwelekeo wa kingono, asili ya kitaifa au kabila, rangi, dini, lugha, umri, uwezo au hadhi nyingine yoyote. Sisi sote tuna haki sawa za binadamu bila kubaguliwa.[5]

**Uzingatiaji wa haki za binadamu katika uhifadhi**

Kujumuisha kanuni na viwango vya haki za binadamu katika sera, upangaji, utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha kuwa uhifadhi unaheshimu na kudumisha haki hizi. Kwa kutumia njia hii, haki za binadamu na uhifadhi huimarisha mpango na huwa kichocheo cha utendakazi.[6]

**Ustawi wa watu**

Hali ambapo mahitaji ya mtu yanatimizwa, mtu anaweza kufanya kazi kwa njia inayostahili ili kutimiza malengo yaliyowekwa na ameridhika.[7]

**Wenyeji na jamii za eneo hilo**

Watu na jamii ambazo zina uhusiano mkubwa na mandhari yao ya asili, ambayo wanategemea kwa ajili ya ustawi wa kitamaduni, kiroho, kiuchumi na kimwili. Wakazi wa asili na wahamiaji ambao wana uhusiano wa karibu na mandhari vile vile huchukuliwa kama IPLCs. TNC inatambua haki za watu wote wenyeji kama ilivyoorodheshwa katika sheria za kimataifa. Katika Mwongozo huu, “IPLC” hutumiwa kurejelea watu wote ambao ni wenyeji na jamii zote za eneo hilo.[8]

**Haki za binafsi na za watu wote**

Mikataba mingi ya haki za binadamu inaonyesha dhana ya ubinafsi wa haki na wenye haki; kwa mfano, haki ya kupata elimu au haki ya kuishi ni haki ya kila mtu. Kwa wenyeji wengi, utambulisho hauwezi kutenganishwa na kikundi ambacho mtu yuko. Kwao, haki za watu wote, kama vile haki ya kujiamulia mwenyewe au haki ya kumiliki ardhi kama jamii, ni muhimu. [9]

**Haki za hakimiliki**

Haki anazopewa watu kuhusiana na ubunifu wake.[10] Kwa mujibu wa Azimio la Mataatua la Haki za Mali za Utamaduni na Uvumbuzi za Wenyeji, wenyeji wanapaswa kubainisha wenyewe mali yao ya utamaduni na uvumbuzi.[11]

**Watu**

Hali ya wingi “Watu” inatambua kuwa jamii inayorejelewa inajumuisha vikundi vingi. Kwa mfano, “Mtu Asilia” (umoja) inaweza kumaanisha kila mtu binafsi au mtu wa jamii fulani, ilhali “Watu” (wingi) inaonyesha vikundi tofauti ya jamii asilia.”[12] Kiambishi tangulizi “wa” mwanzoni mwa “watu” kinaonyesha kuwa ni vikundi vingi na kinaashiria haki zao za pamoja, haswa haki ya kujiamulia mwenyewe. Shirika la Umoja wa Mataifa liliidhinisha neno “wenyeji” mnamo 2002 kwenye Kongamano la Kimataifa la Maendeleo Yasiayoaathiri Mazingira, lililofanyika Kimberley, nchini Afrika Kusini.[13]

**Sera za Kulinda Maslahi**

Kanuni, sera, vigezo, taratibu, mifumo na mwongozo wa utendakazi unaosaidia kuhakikisha kuwa muundo na utekelezaji wa mpango unazuia, unapunguza au unafidia athari hasi.[14]

**Kujiamulia mwenyewe**

Haki ya kujiamulia mwenyewe ni kanuni ya msingi ya sheria za kimataifa. Imejumuishwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa na Mkataba wa Kimataifa kuhsu Haki za Kiraia na Kisiasa, na Mkataba wa Kimataifa kuhusu Uchumi, Haki za Jamii na Utamaduni. Kifungu cha 1, aya ya 1 katika Mikataba hii kinasema kuwa: “Watu wote wana haki ya kujiamulia wenyewe. Kwa mujibu wa haki hiyo, wanaweza kuamua hali yao ya kisiasa na kufuata malengo yao ya kijamii, kiuchumu uchumi wao, kijamii na kitamaduni jinsi wapendavyo.”[15] Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji (pamoja na sheria nyingine muhimu za kimataifa) inajumuisha haki ya wenyeji ya kujiamulia wenyewe katika sheria ya kimataifa.

**Vitambulisho vya kijamii**

Katika Mwongozo huu, tunatumia "vitambulisho vya kijamii" ili kuhimiza ujumuishaji katika mbinu zetu za uhifadhi zinazozingatia haki za binadamu. Vitambulisho hivi vzinajumuisha:

- tamaduni
- utambulisho wa kuwa mwenyeji, ikijumuisha makao, utamaduni na uhusiano wa kifamilia
- mbari na kabila
- dini au imani za eneo hilo
- jinsia
- asili ya taifa au eneo
- umri, ikijumuisha vijana na wazee
- uwezo na hali ya ulemavu
- hisisa za kimapenzi
- utambulisho wa kijinsia
- hali ya uanajeshi na mwanajeshi aliyestaafu
- lugha
- elimu, pamoja na uwezo wa kusoma na kuandika
- hali ya kiuchumi, ikiwemo tabaka
- eneo la kijiografia, pamoja na msimu au umbali
- hali ya uhamiaji au visa
- rekodi ya jinai
- hadhi nyingine iliyolindwa kisheria

## Maelezo

[1] Ufafanuzi unarejelea The Nature Conservancy in Washington's Equity Statement & Definitions (2019).

[2] Ufafanuzi unarejelea: Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa. (2016). Idhini ya Kujitolea, Inayotolewa Mapema na Baada ya kuelewa: Haki ya jamii asilia na desturi nzuri kwa wenyeji: http://www.fao.org/3/a-i6190e.pdf

[3] Ufafanuzi unarejelea: Mfumo wa UNESCO wa Utekelezaji wa Masuala ya Jinsia: http://www.unesco.org/new/fileadmin/MULTIMEDIA/HQ/BSP/GENDER/PDF/1.%20Baseline%20Definitions%20of%20key%20gender-related%20concepts.pdf

[4] Y. Masuda, mawasiliano ya kibinafsi, Juni 13, 2015.

[5] Ofisi ya Kamishna wa Tume Kuu ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu. Je, haki za binadamu ni nini? Ilitolewa Juni 17, 2015 kutoka http://www.ohchr.org/EN/Issues/Pages/WhatareHumanRights.aspx

[6] Campese, J., Sunderland, T., Greiber, T. na Oviedo, G. (wahariri.) 2009 Uzingatiaji wa haki: Kuchunguza masuala na fursa za uhifadhi. CIFOR na IUCN. Bogor, Indonesia.

[7] Shirika la The Nature Conservancy. Mwongozo wa Conservation by Design 2.0 (toleo la 2016): https://www.conservationgateway.org/ConservationPlanning/cbd/Documents/CbD2.0_Guidance%20Doc_Version%201.pdf

[8] T-Roots, TNC 2015. Ufafanuzi huu umetolewa kwenye vyanzo vifuatavyo:

UNEP na EDO NSW. (2013). Kanuni za Kijamii za Utunzaji wa Mazingira: Mwongozo kwa Waundaji Sera UNEP, Nairobi na EDO NSW, Sydney.

Corrigan, C. na Hay-Edie, T. 2013. 'Zana ya uhifadhi kwa wenyeji na jamii za eneo hilo: kukuza uwezo na kushiriki maelezo na wenyeji na jamii za eneo hilo kuhusu maeneo yaliyohifadhiwa (ICCA)' UNEP-WCMC, Cambridge, Uingereza.

Rey, D., Roberts, J., Korwin, S., Rivera, L., na Ribet, U. (2013) Mwongozo wa Kuelewa na Kutekeleza UNFCCC REDD Pamoja na Sera za Kulinda Maslahi. Client Earth, London, Uingereza.

Mkutano wa Wataalamu Wanaowakilisha Jamii Husika kuhusiana na Kipengee cha 8(j) na Vipengee Husika vya Mkataba wa Utafauti wa Kibaolojia, (Montreal, tarehe 7 Julai 2011) Mwongozo wa Mazungumzo Kuhusu Jamii Husika kwa Mujibu wa Mkataba wa Utafauti wa Kibaolojia, UNEP/CBD/AHEG/LCR/1/2, p.1.

[9] Buppert, T., & McKeehan, A. (2013). Mwongozo wa utumiaji idhini ya kujitolea, inayotolewa mapema na baada ya kuelewa: Mwongozo wa Shirika la Conservation International: https://www.conservation.org/docs/default-source/publication-pdfs/ci_fpic-guidelines-english.pdf?sfvrsn=16b53100_2. Ofisi Husika ya Kamishna wa Tume Kuu ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu: Maswali yanayoulizwa sana kuhusu uzingatiaji wa haki za binadamu katika utendakazi wa shirika (2006): http://www.ohchr.org/Documents/Publications/FAQen.pdf.

## Maelezo (Imeendelezwa)

[10] Shirika la Biashara Ulimwenguni:
https://www.wto.org/english/tratop_e/trips_e/intel1_e.htm

[11] Azimio la Mataatua kuhusu Utamaduni na Haki za Hakimiliki ya Wenyeji. (1993):
https://www.wipo.int/export/sites/www/tk/en/databases/creative_heritage/docs/mataatua.pdf

[12] https://indigenousfoundations.arts.ubc.ca/terminology/

[13] https://www.un.org/esa/socdev/unpfii/documents/SOWIP/en/SOWIP_web.pdf, ukurasa wa 102)

[14] Wongbusarakum, S., Myers Madeira, E., na Hartanto, H. (2014). Kuimarisha manufaa ya kijamii ya mipango endelevu ya kimazingira: Mwongozo wa kuimarisha na kufuatilia matokeo ya ustawi wa binadamu. Shirika la The Nature Conservancy, 10:
https://www.conservationgateway.org/ConservationPractices/PeopleConservation/SocialScience/Documents/TNC%20Guidebook%20draft%20070814%20-%20for%20office%20print.pdf

[15] https://www.iwgia.org/en/focus/land-rights/330-self-determination-of-indigenous-peoples.html

### Kiambatisho cha III

# Mchakato wa Uamuzi wa FPIC

Moduli ya 2:

Mchakato wa Uamuzi wa FPIC

### Kiambatisho cha IV

# FPIC – Maswali Yanayoulizwa Sana

Kwenye Kiambatisho hiki:

Kagua kwa undani zaidi baadhi ya maswali tata kuhusu FPIC

**Je, ni nini hufanya uhusiano kati ya binadamu na mazingira kuwa thabiti?**

Kuelewa chanzo cha uhusiano na thabiti kati ya binadamu na mazingira kunahitaji mchakato wa kusikiliza, kujifunza na kuthamini mtazamo wa IPLC. Baadhi ya viashiria vya uhusiano thabiti ni pamoja na:

- Maeneo yanayochukuliwa na wanajamii kuwa muhimu zaidi
- Maeneo ambayo hali ya uhusiano ni anuwai, yaani, ardhi ni mahali pa kuishi, kulima au kuwinda na pia inahusishwa na historia ya mababu wa jamii, utamaduni, maisha ya kiroho na utambulisho wao.

Kuhusiana na jamii ya Saramaka, jamii zilizoundwa mwanzoni na watu waliotorokea utumwa kwenye miji ya pwani na kukimbilia "maeneo ya ndani ya nchi [Suriname] ambapo walianzisha jamii zinazojitegemea." IACHR ilisikia simulizi nyingi kuhusu jinsi watu walivyoishi kwenye ardhi na maana yake kwa jamii hiyo. Ilitambua kwamba "utambulisho wa Wasaramaka na ardhi zinahusiana na vita vyao vya kihistoria vya kutorokea utumwa, inayojulikana kama 'mara ya kwanza.' takatifu"

**Je, kuna chanzo cha kurejelewa kuhusu kinachohitajika katika FPIC?**

Hakuna chanzo kinachoelezea FPIC kikamilifu. Badala yake, kuna kanuni za msingi, kama vile mashauriano na idhini ya kujitolea, inayotolewa mapema na baada ya kuelewa. Mikataba inaongeza upekee, kama vile maamuzi ya kortini ambayo yanazingatia ikiwa mchakato wa FPIC ulifuatwa katika kesi fulani, na miongozo kama hii inajaribu kujumuisha yote pamoja.

**Je, chanzo cha FPIC ni nini?**

FPIC imekana na mchakato unaojulikana kama sheria ya kimila ya kimataifa. Sawa na sheria za kawaida nchini Marekani na Uingereza, sio tu suala la sheria na kanuni, lakini hubadilika baada ya muda kutokana na majimbo, maamuzi ya mahakama na taarifa zingine zinazotolewa na asasi za mamlaka. Hii inajumuisha sera zilizoidhinishwa na taasisi muhimu kama vile Benki ya Dunia na hata wadau katika asasi za kiraia kama vile TNC. Vyanzo vinapoendelea kubadilika ndivyo FPIC hubadilika pia. Hivyo basi, TNC iko chini ya sheria ya kimila ya FPIC na inaweza pia kuchangia mabadiliko ya FPIC.

1. Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji haishurutishi lakini linachukuliwa kuwa sehemu muhimu sana ya sheria ya kimataifa, haswa kwa kuwa nchi nne tu ambazo mwanzoni zilipinga azimio hili zimebadili msimamo wao na sasa zinaliunga mkono.
2. Mkataba wa Shirika la Kimataifa la Wafanyakazi Kifungu cha 169 kuhusu ya Wenyeji na Wanajamii Asilia, mkataba wa kisheria uliopitishwa na nchi 22, umetumika kama marejeleo katika maamuzi mengi ya mahakama.

Mahakama ya Haki za Binadamu ya Marekani imekuwa ikijihusisha na haki za wenyeji na FPIC, sawa na mahakama za nchi kadhaa, kama vile Kanada na Kolombia, zinazochukuliwa kuwa wataalam.

### Je, FPIC ndiyo sheria—au ni wazo nzuri tu?

Ni vigumu kutenganisha kati ya sheria inayoshurutisha (sharti ufanye kitu la sivyo kuna matokeo hasi) na sheria isiyoshurutisha (unapaswa kufanya kitu) katika kiwango cha kimataifa.

Wengine wanasema kuwa sheria zote za kimataifa zina sifa ya kutoshurutisha. Kwa hali yoyote, kupitishwa kwa FPIC na wahusika anuwai hufanya FPIC kuwa sheria mseto, hata ikiwa haishurutishi kisheria katika hali zote. Serikali, taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali leo zinatambua kuwa ukiukaji wa sheria mseto kama vile FPIC mara nyingi utasababisha matokeo mabaya zaidi kuhusiana na kuaminika na uwezo wa taasisi. TNC ni mwanachama mwanzilishi wa Mpango wa Uhifadhi wa Haki za Binadamu na imejiunga na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali yanayohusika na mazingira kudumisha FPIC.

### Je, wenyeji na jamii za eneo hilo huchukuliwa sawa?

FPIC ilitengenezwa kwa kuwazingata wenyeji, yaani, watu ambao wameishi mahali fulani tangu jadi, wamenusurika ukoloni na ubeberu, na wamedumisha utamaduni wao.

Watu wengi asilia walipata kiwewe enzi za ukoloni na baada ya ukoloni, pamoja na:

- Kufurushwa
- Watu kufariki ya kutokana na vita au magonjwa
- Watoto kupelekwa shule za bweni
- Marufuku ya kuzungumza lugha zao na kuendelea na mila ya kitamaduni na kiroho
- Vizuizi vikali kuhusu matumizi ya ardhi yao

Sawa na kwa wenyeji, TNC pia inazingatia sheria za ulinzi zinazohitajika kwa jamii mbalimbali ambazo huenda zikaathirika. Kwa sababu ya aina ya kazi tunayofanya, TNC inazingatia kudumisha uhusiano thabiti na mazingira ya asili.

Kama chifu mmoja wa Saramaka, Wazen Edwards, alivyosimulia: “Mababu zetu walipokimbilia msituni walienda bila chochote. Walijifunza jinsi ya kuishi, mimea ya kula, jinsi ya kujikimu pindi walipofika msituni.” Kutokana na hali hii, Wasaramaka waligundua kuwa ardhi haijawapokea tu, bali pia iliwasaidia na kuwakomboa. Iliwafundisha jinsi ya kuwa huru. Hivyo basi, ingawa jamii za Wasaramaka hazikuwa "asili," hata kwenye bara la Amerika Kusini, IACHR ilizingatia na kuendeleza sheria kuhusu haki za wenyeji katika madai yao.

### Ipi “kati ya” mashauriano na idhini?

Vipengele vitatu vya kwanza vya FPIC-mapema, kwa hiari, kwa kufahamishwa-vimeongezwa na kukuzwa kwa muda ili kulinda kipengee cha msingi ambacho ni: idhini.

Hii inaonyesha kuwa FPIC hupelekea utoaji wa idhini madhubuti na mwafaka. Hata hivyo baadhi ya vyanzo vimeondoa idhini kwenye mchakato kwa kuweka kiwango kuwa “mashaurino ya mapema, kwa hiari na kwa kufahamu.”[1]

Toleo hili la FPIC, linalojulikana kama Mashauriano-FPIC, linategemea vigezo vya mapema, hiari na kwa kufahamu vya FPIC, lakini uamuzi hufanywa na anayeendesha mashauriano wala sio yule anayeshauriwa.

Mashauriano-FPIC yana wakosoaji. Lakini ni rahisi sana kulichukuliwa kuwa toleo la chini la FPIC. Mashauriano yanaweza kuendeleza idhini ya wenyeji wanaohusika, na ikikubalika jinsi ilivyo na kutekelezwa kikamilifu, inaweza kuwa zana muhimu ya ulinzi.

Inaweza pia kuepuka baadhi ya utata kuhusu mahitaji ya idhini, ambayo wakati mwingine huchukuliwa katika

siasa za kitaifa kama mamlaka ya wenyeji yanayopuuza masuala nyeti ya utumiaji wa ardhi na uamuzi kuhusu maliasili.

Mfumo wa sheria wa Kanada unategemea sana Mashauriano-FPIC lakini imethibitisha katika miaka ya hivi majuzi kuwa ina uwezo wa kulinda haki za kujiamulia wenyewe za wenyeji wakikabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa sekta ya mafuta, gesi na mabomba. Wanaharakati wakuu asilia wameunga mkono wazo la mwingiliano changamano kati ya idhini na mashauriano.[2] Profesa James Anaya, mwasisi wa sheria za kimataifa za haki za wenyeji ambao wamehudumu vipindi viwili kama Mwandishi Maalum wa Umoja wa Mataifa anyeshughulikia masuala ya Haki za Wenyeji, ameelezea kuwa haki ya wenyeji ya kujiamulia wenyewe "n[i] zaidi ya kufahamishwa na kusikika lakini si haki kuu isiyoweza kubatilishwa."[3]

Mojawapo ya sababu zinazofanya iwe vigumu kutenganisha idhini na mashauriano ni kuwa wenyeji wana misimamo tofauti, kwa hivyo kuchukulia kuwa idhini ya wenyeji haiwezi kubatilishwa kunaweza pelekea jamii moja ya wenyeji kukinzana na jamii jirani. Na haki ya wenyeji ya kujiamulia wenyewe daima hukinzana na mamlaka ya utawala yanayotekelezwa katika mataifa ya kisasa. Kwa kuzingatia hili, mahakama, watunga sera na wataalamu, pamoja na wale wanaowaunga mkono sana wenyeji, wamebuni mbinu kadhaa za kusawazisha ushindani, kuhakikisha uhalali wa mashauriano na kulinda kiini cha idhini.

Si dhahiri jinsi njia hizi zinavyotumika kwa mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile TNC, lakini muhimu kuzingatia juhudi za TNC za kupata idhini kamili kutoka kwa IPLC zilizoathiriwa kabla ya kuendelea na mpango wowote.

Inawezekana kuwa juhudi za TNC za kutumia utaratibu unaotegemea idhini hazitasuluhisha kila mzozo kati ya jamii zilizoathiriwa. Lakini hali hizo zinapotokea, japo ni nadra, zinaweza kushughulikiwa moja baada ya nyingine. TNC inatambua uhalali wa michakato yote ya FPIC na Ushauri-FPIC, mradi kanuni za msingi na nia njema zinadumishwa, lakini tumechagua kushikilia utaratibu unaotegemea idhini.

## Maelezo

[1] Kwa mfano, kiwango hiki kilitumika katika IFC ya mwaka wa 2006 kwenye Kiwango cha Utendaji kwa wenyeji na kilirejelewa kwenye toleo la 4.10 la Sera ya Uendeshaji wa Benki ya Dunia. Kwa mfano, https://policies.worldbank.org/sites/ppf3/PPFDocuments/090224b0822f89d5.pdf. Katiba ya kihistoria ya mwaka wa 2008 ya nchi ya Ekwado, ambayo pia ililinda haki za mazingira, ilijumuisha Mashauriano- FPIC kwenye katiba katika kifungu cha 57, aya ya 7. Kama ilivyojadiliwa hapa, mfumo wa katiba na sheria za kawaida za Kanada zinazohusu kulinda ardhi asilia na haki za kujiamulia mwenyewe zinahitaji Mashauriano-FPIC.

[2] Toleo la 4.10 la Sera ya Uendeshaji wa Benki ya Dunia pia ni mfano mzuri wa uhusiano huu changamano. Japo sera yenyewe inahitaji "mashauriano ya mapema, ya hiari free na yanayostahiki," sera inapendekeza zaidi kwamba "[B]enki ikague mchakato na matokeo ya mashauriano yaliyofanywa na mkopaji ili kuthibitisha kuwa Jamii za wenyeji zilizoathirika zinaunga mkono mradi huo" na kwamba "[B]enki haiendelei kuandaa mradi ikiwa haiwezi kuthibitisha kuwa jamii zinaunga mkono."

[3] S James Anaya na Sergio Puig, Kudhibiti Mamlaka ya Serikali: Wajibu wa Kushauriana na Wenyeji, 67 U. Toronto L.J. 435 (2017).

### Kiambatisho cha V

# Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni

Kwenye Kiambatisho hiki:

Pata anwani ya ofisi ya Maadili na Utekelezaji ya TNC Fahamu jinsi ya
kuwasilisha malalamishi
Fahamu hatua zinazofuata baada ya kuwasilisha malalamishi

**Wasiliana na Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni za TNC**

**Tovuti ya Huduma za Usaidizi:**
nature.org/tnchelpline

**Huduma ya usaidizi:**
Nambari ya Simu: (800) 461-9330 (Marekani)
SMS: 571-458-1739 (Marekani)
Tembelea tovuti ya huduma ya usaidizi ili upate nambari za simu za kimataifa

**Anwani ya Barua:**
4245 N. Fairfax Drive
Suite 100
Arlington, VA 22203

Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni umeundwa ili kupokea na kutatua mashaka kuhusiana na madai ya ukiukaji wa TNC kuhusiana na:

- Kanuni ya Maadili ya TNC;
- Sera na Taratibu za TNC, ikijumuisha Kanuni na Sera za Kulinda Maslahi katika Mwongozo huu;
- Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Wenyeji;
- Mpango wa Uhifadhi wa Kanuni za Haki za Binadamu; au
- Mkataba wa Idhini wa IPLC.

Wafanyakazi wa TNC wanapaswa kukumbuka kuwa kila mfanyakazi anawajibikia kibinafsi uzingatiaji wa Kanuni za Maadili, Sera na Taratibu za TNC.

**Kutolipiza Kisasi**

TNC hairuhusu ulipizaji kisasi wa aina yoyote, ikiwemo unyanyasaji, vitisho, vitendo vinavyoathiri mfanyakazi kwa njia hasi, au aina nyingine yoyote ya kulipiza kisasi, dhidi ya wafanyakazi ambao kwa nia njema wanaripoti ukiukaji wa sheria, wanashiriki katika uchunguzi, au wanatambua ukiukaji wa Kanuni za Maadili ya TNC. Mfanyakazi yeyote anayelipiza kisasi atachukuliwa hatua za kinidhamu, zinazojumuisha hadi kuachishwa kazi.

**Wanaoweza Kuwasilisha Malalamishi**

Jamii yoyote, shirika au mtu binafsi anaweza kuwasilisha malalamishi kama mwathiriwa. Shirika au mtu binafsi ambaye ameruhusiwa na mwathiriwa anaweza kuwasilishwa malalamishi kwa niaba yake kama mwakilishi. Malalamishi yanaweza kuwasilishwa bila kumtambulisha aliyewasilisha na yatashughulikiwa kwa usiri kadiri iwezekanavyo, na yatafumbuliwa tu kwa wanaohusika.

**Kuwasilsha Malalamishi**

Mwathiriwa au mwakilishi wake wanaweza kutumia Huduma ya Usaidizi ya TNC kuwasilisha malalamishi kwa lugha wanayopendelea. Mwathiriwa au mwakilishi wake ataulizwa maelezo yafuatayo yatakayotumiwa na Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni kufanya uchunguza wa kina:

- Jina na anwani
- Mradi maalum au mpango husika, ikijumuisha mkoa, nchi na anwani ya kieneo ya TNC
- Tarehe inayokadiriwa au halisi ambapo tukio linaloripotiwa lilitokea
- Ukiukaji unaodaiwa kutokea na madhara ambayo yanatokana na ukiukaji huo
- Maelezo au hati zingine zozote muhimu, ikiwa zinapatikana
- Hatua zilizochukuliwa kufikia sasa kusuluhisha tatizo, ikijumuisha mawasiliano na TNC kwenye kiwango cha mradi au Kitengo cha Biashara
- Ikiwa kuna masharti kuhusiana na usiri

**Mchakato wa TNC wa Maadili na Kufuata kanuni**

1. Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni hupokea malalamishi na kubaini ustahiki.
2. Ndani ya saa 48, Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni itathibitisha kuwa imepokea mashaka.
3. Ndani ya siku nne za kazi baada ya kupokea malalamishi, Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni itatathmini ustahiki kisha itatoa majibu kwa aliyeathiriwa au mwakilishi wake kuhusu ustahiki wa malalamishi yaliyowasilishwa. Inawezekana kuwa malalamshi hayo yanapaswa kushughulikiwa na mtu mwingine au idara tofauti ya shirika. Katika hali hizo, TNC itawasilisha malalamishi kwa mhusika anayefaa kisha itamjulisha mwathiriwa au mwakilishi wake.
4. Ikiwa malalamishi yanastahiki, Afisa Mkuu wa Maadili na Utekelezaji Kanuni atajulisha timu ya mradi wa TNC na Msimamizi wa Kitengo cha Biashara kadri inavyowezekana bila kukiuka usiri, na pia atamjulisha mwathiriwa au mwakilishi wake kisha ataanzisha uchunguzi kulingana na taratibu za uchunguzi za TNC na masharti maalum kwa kufanya kazi na IPLC.
5. Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni pia itaarifu Ofisi ya Utofauti Ulimwenguni, Usawa na Uhusishaji, Afisa wa Masuala ya Hatari, wakili husika wa TNC na viongozi wengine wakuu kama inavyostahili.
6. Kufuatia uchunguzi, Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni itaandaa rasimu ya matokeo, njia inayopendekeza ya utatuzi, hatua za kuchukuliwa na muda wa kuzitekeleza kisha itaziwasilisha kwa mwathiriwa au mwakilishi wake, timu ya mradi wa TNC na msimamizi wa Kitengo cha Biashara. Kila mhusika atakuwa na siku tano za kazi kujibu pendekezo la Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni.
7. Ndani ya siku tano za kazi baada ya kupokelea majibu au tarehe ya makataa ya kutoa majibu, Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni inaweza kurekebisha rasimu ya pendekezo na kisha itatoa uamuzi kwa mwathiriwa au mwakilishi wake, timu ya mradi wa TNC na msimamizi wa kitengo cha biashara. Timu ya mradi wa TNC, msimamizi wa Kitengo cha Biashara na mwathiriwa wanatarajiwa kuchukua hatua zilizobainishwa katika uamuzi.

8. Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni itafuatilia utekelezaji wa hatua zinazopaswa kuchukuliwa na itawasiliana na mwathiriwa mara kwa mara kama ilivyoainishwa katika mpango.

### Kiambatisho cha VI

# Orodha za kukagulia

Moduli ya 1:

Orodha za kukagulia Mafunzo na Majadiliano ya Mwanzo

Moduli ya 2:

Orodha za kukagulia za FPIC

Moduli ya 3:

Orodha za Kukagulia za Utatuzi wa Mgogoro

Moduli ya 4:

Orodha za kukagulia Utekelezaji

Moduli ya 5:

Orodha za kukagulia Kuandika hati

Moduli ya 6:

Orodha ya kukagulia ya Ufuatiliaji, Tathmini na Marekebisho

## Kiambatisho cha VII

# Hati za Kuhifadhi

Moduli ya 1:

Hati za Kuhifadhi

Moduli ya 2:

Hati za Kuhifadhi

Moduli ya 3:

Hati za Kuhifadhi

Moduli ya 4:

Hati za Kuhifadhi

Moduli ya 5:

Hati za Kuhifadhi

Moduli ya 6:

Hati za Kuhifadhi

### Kiambatisho cha VIII

# Violezo

Moduli ya 1:

Kiolezo cha Mpango wa Kujihusisha

Moduli ya 2:

Kiolezo cha Mpango wa Ushauri wa FPIC

Moduli ya 3:

Kiolezo cha Mpango wa Utatuzi wa Mgogoro

Moduli ya 6:

Kiolezo cha Viashiria vya Haki za Binadamu

### Kiambatisho cha IX

# Shukrani

Timu ya Kimataifa ya Wenyeji na Jamii za Eneo hilo, Utofauti, Timu ya Utofauti Ulimwenguni, Usawa na Uhusishaji ziliongoza uundaji wa Mwongozo huu, kwa kushirikiana na Timu ya Kimataifa ya Sheria ya TNC. Wafanyakazi na washirika wa TNC kote ulimwenguni walichangia maudhui. Toleo la kwanza lilifanyiwa majaribio na timu na washirika wa TNC nchini Brazil, Indonesia na Nature United/Emerald Edge kwa muda wa miezi 18. Yaliyojitokeza wakati wa majaribio pamoja na ukaguzi uliofuata ziliboresha Mwongozo sana.

The Nature Conservancy inawashukuru sana watu wote waliochangia katika uundaji wa Mwongozo huu na ingependa kutoa shukrani za dhati: Eduardo Barnes, Michelle Beistle, Ivar Busatto (Operação Amazônia Nativa), Ruth Castro, Laurel Chun, Rane Cortez, Luis Davalos, Eric Delvin, Nicole DeMello, Maria Estrada, Ofisi ya Maadili na Utekelezaji Kanuni ya TNC, Edenise Garcia, Gathering Voices Society (led by William Nikolakis, na Ngaio Hotte na Alanna Spence), David Hinchley, Claire Hutton, Connor Lee, Craig Leisher, Hilda Lionata, Michael Looker, Erin Myers Madeira, Allison Martin, Adrienne McKeehan (Shirika la Conservation International), Susi Menazza, Patricia Mupeta-Muyamwa, Jessica Musengezi, Crystal Nelson, Karen Oliveira, Aaron Marr Page (Forum Nobis), Michael Painter (Wildlife Conservation Society), Katherine Pflaumer, Luke Preece, James Puerini, Kleber Santos (Coordenação das Organizações Indígenas da Amazônia Brasileira), Rosita Scarborough, Randi Shaw, Helcio Marcelo de Souza, Ian Thompson, Steven Victor, Kristin Walker (Shirika la Conservation International), Joenia Wapichana (Wakili), David Wilkie (Wildlife Conservation Society), Johnny Wilson, Heather Wishik na Kikundi cha Women in Nature Employee Resource Group cha TNC.

Mwongozo huu umefanikishwa na udhamini wa mfadhili asiyejulikana pamoja na Roger na Margot Milliken.

---

Nature United ni shirika tangu la Kanadi la shirika kubwa zaidi ulimwenguni la uhifadhi.

Nature United ina miongo mitatu ya utendakazi nchini Kanada na inajitahidi kuhakikisha kuwa nchini Kanada watu wanahusika katika masuala ya mazingira na kuwa ikolojia, jamii na uchumi zinastawi.

Shirika letu linashirikiana na Wenyeji na jamii za eneo hilo, serikali, viwanda na makundi mengine kubuni njia mpya za kupata mustakabali wa kudumu; kuendeleza maridhiano; na kuhifadhi maumbile ambayo ndiyo msingi wa maisha yote Duniani. Na usaidizi wa shirika kubwa zaidi la uhifadhi ulimwenguni, tunaleta ujuzi wa juu zaidi wa kisayansi, uvumbuzi na rasilimali nchini Kanada.

natureunited.ca

Nature United